# GOMA MAGOTINI

ABUBAKAR NKUNDWASON

©MWANDISHI
Abubakar Nkundwason
Chapisho la kwanza; Februari, 2025.

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inaruhusiwa kuhamishwa kwa namna yoyote ile, iwe ya kimaandishi au kielektroniki bila ridhaa ya maandishi kutoka kwa mwandishi. Kukiukwa kwa agizo hili ni uvunjwaji wa sheria.

Msanifu kurasa: Maua Mshana
Mhariri: Joe Lwebagaramu.
Wasiliniana nami:
WhatsApp: +255 753 905 099
Kimechapishwa na: Simulizi Africa Publishers.
Dar es Salaam.

ISBN: 978-9912-42-678-0

## SHUKURANI

Shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, Muumba wa viumbe vyote kwa wema na ukuu wake hata kuniwezesha kufanikisha kutoka kwa kitabu hiki.

Shukurani pia kwa wazazi wangu, marehemu baba yangu Athuman R. Nkundwason pamoja na mama yangu Hamida H. Mussa. Kwa yale yote ambayo wazazi wangu wameyafanya kwa ajili yangu; kujitolea, upendo wao na mengine mengi; hakika sioni jema la kufanya hata liwe malipo, zaidi ya kuwapenda, kuwaenzi na kuwaombea dua siku zote za maisha yangu.

Shukurani za dhati pia kwa mke wangu kipenzi, Sumaiya S. Chowo. Hakika mke wangu umekuwa mwema mno kwangu; katika yote tutashikamana na moyoni mwangu nimekupa makao ya uhakika.

# 1

*November, 2009,*
Beijing, China.

Jioni ilikuwa imeshuka polepole juu ya anga la Beijing, huko Uchina, ikiacha mwanga hafifu wa taa za mitaani zikimulika barabara zilizojaa wanafunzi waliokuwa wakitembea kwa haraka. Chuo kikuu cha Tsingua, kikiwa na majengo yake marefu ya kisasa na barabara zake zenye miti ya minazi, kilionekana tulivu kwa nje, lakini ndani yake hali ilikuwa tofauti.

Katika kona moja ya uwanja wa chuo, vikundi vya wanafunzi wa Kiafrika na wengineo walikusanyika kimya kimya, macho yao yakiangaza huku na kule kwa tahadhari. Hatua zao zilikuwa nzito, nyuso zao zikionyesha mchanganyiko wa hofu na hasira.

Na hiyo yote ilitokana na vuguvugu la maandamano lililofukuta chini kwa chini kufuatia tukio la mwalimu mmoja aitwaye Bolin Chaoxiang, kumtemea mate, binti mwenye asili ya Afrika kutoka taifa la Mali, kwa madai kuwa binti huyo alimkanyaga mbwa wake. Mbali na kumtemea mate, mwalimu huyo Chaoxiang alimdhalilisha kwa kumtukana matusi mengi huyo msichana ikiwa ni pamoja na kumuita sokwe mtu!

Kitendo hicho, kilitafsiriwa kuwa ni kitendo cha kibaguzi na jamii ya wanafunzi wenye asili ya Kiafrika. Kikapewa nguvu na mashuhuda wake waliotoa shuhuda kuwa binti huyo alimkanyaga huyo mbwa kwa bahati mbaya, alipokuwa akirudi nyuma wakati anacheza na wenzake.

Lakini pia, picha jongefu za tukio hilo, zilizopatikana kwenye kamera zilizofungwa katika eneo la chuo hicho, zilionyesha kuwa; kitendo cha Fanta Seydoe hakikuwa cha makusudi. Na

wazungumziaji wa suala hilo, wengine walikwenda mbali na kusema kuwa, hata kama kitendo hicho kingekuwa cha makusudi, Bolin Chaoxiang, hakupaswa kufanya kitendo alichokifanya. Kulikuwa na namna nyingine ya kumuwajibisha Fanta Seydoe.

Tukio lenyewe lilikuwa hivi: wakati msichana huyo akiwa anacheza na kufanya mizaha na wenzake; mwalimu Chaoxiang pamoja na mbwa wake, walikuwa wanatembea kuelekea uelekeo huo waliokuwepo. Ndipo Fanta, akiwa anaonyesha umahiri wake wa namna alivyokuwa na uwezo wa kuusakata muziki wa *Afro Pop,* kwa bahati mbaya alikosea hatua, akajikuta anapepesuka na kumkanyaga mbwa huyo. Shida ikaanzia hapo!

Hata hivyo, jamii ya wanafunzi wenye asili ya Afrika, wakishirikiana na wanafunzi wa mataifa mengine waliokuwa wanapinga masuala ya ubaguzi, walikuja juu wakishinikiza uongozi wa chuo hicho, umchukulie hatua mwalimu Bolin Chaoxiang.

Anawezaje kumdhalilisha na kumfanyia ubaguzi wa namna hiyo mwanafunzi mwenzao ati kisa amekanyaga mbwa wake na tukio lenyewe si la makusudi?

Ni kweli kwamba; mbwa, akiwa ni miongoni mwa kundi la wanyama wana haki zao. Na haki zao zinapaswa kulindwa kama vile haki za viumbe wengine. Lakini kwa kitendo kilichotendeka, hakikuwa cha kukiuka haki za mnyama huyo, bali lilikuwa ni tukio la bahati mbaya. Wanafunzi walikuja juu. Juu kweli kweli ukifuatia matukio ya namna hiyo hayakuwa mageni hapo Uchina. Wakalaani kitendo hicho kiasi cha kupeleka malalamiko yao kwenye uongozi wa chuo.

Lakini, katika namna ya kushangaza, siku tatu zimepita uongozi wa chuo hicho upo kimya, kitendo kilichowachukiza mno wanafunzi, ndipo hapo walipopanga maandamano. Na sasa sekeseke la maandamano limepamba moto.

*****

Biruse Othuman Seyunguson; ndiye alikuwa kinara haswa wa hayo maandamano. Biruse, alikuwa ni kijana mwenye umri wa

miaka 21, mwenye asili ya Tanzania na mtoto wa kachero mkubwa mwenye heshima kubwa kwenye medani ya usalama barani Afrika, marehemu Othuman Seyunguson.

Kijana huyu mrefu, mwenye mwili uliojengeka vyema kutokana na mazoezi ya viungo aliyopenda kufanya, ambaye hupendelea kukata nywele zake zote na kuacha kichwani upaa ama maarufu kwa jina la *zungu la unga,* alikuwa ni maarufu chuoni hapo kutokana na kariba yake ya kupenda michezo; na mchezo uliomtambulisha kwa wengi ulikuwa ni wa mbio za riadha na kutokana na kufahamika na kuheshimika kwake, alipoamua kulibeba suala hilo la maandamano, alipata muitikio mkubwa.

Katika majira haya ya saa moja za jioni, Biruse, pamoja na wenzake waliokuwa wamejipanga kwa ajili ya maandamano; waliuhadaa uongozi wa chuo hicho kwa kusambaza taarifa kwa wanafunzi wengine kuwa maandamano yatafanyika asubuhi ya siku inayofuata, lakini kumbe kulikuwa na mpango mwingine kabambe.

Biruse alikuwa amevipanga vikundi takribani vinne vya wanafunzi wenye asili ya Afrika, Urusi, Izrael na Amerika, kwa ajili ya maandamano hayo; na mipango yao ilikuwa ni kuvamia maeneo muhimu ya chuo hicho usiku huo na kuharibu miundombinu kwa kiasi kikubwa.

Kama kusema kwa maneno wamejitahidi kusema kuonyesha hawakubaliani na vitendo hivyo vya kibaguzi. Na kwakuwa wahusika wamechagua kutokuwasikiliza na kuwapuuzia, sasa wameamua kuchukua hatua za kuonyesha vitendo, pengine wahusika wataona na kutambua kuwa masuala hayo ya ubaguzi hayatakiwi kabisa duniani hasa katika zama hizi ambapo ustaarabu wa dunia umepiga hatua kubwa kwenye masuala ya kibinadamu na haki zake. Huo ndio ulikuwa msukumo wao!

Na katika mpango wao huo, wa maandamano na kuharibu mali za chuo, Biruse alipanga kutumia maarifa aliyonayo katika teknolojia, akisaidiana na mpenzi wake Zinaeda, mwanadada mwenye asili ya Urusi, kuingia kwenye *'systeam'* ya umeme ya mji huo wa Beijing, ili

kuzima umeme kwa muda wa dakika kumi, kitendo walichofahamu kingesababisha kadhia kubwa katika mji huo, lakini kingewasaidia wao kufanikisha tukio hilo, na jambo kubwa zaidi; kingechelewesha ujio wa polisi. Jambo ambalo wengi hawakulifahamu ni kwamba, kabla ya Biruse kujiunga na chuo hicho, alipata mafunzo maalumu katika masuala ya TEHAMA, kwenye chuo cha Tohoku, nchini Japan.

Katika chuo hicho, Biruse alijifunza mambo mengi mno yanayohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano, na huko, katika chuo hicho, ndiko Biruse alikutana na Zinaeda kwa mara ya kwanza. Wawili hawa walisoma darasa moja, na kutokana na mafunzo ambayo Biruse alikuwa nayo kwenye masuala ya kijasusi, baadaye aliweza kugundua kuwa Zinaeda si mwanafunzi wa kawaida. Ndipo alipoamua kumfuatilia.

Biruse alijenga urafiki wa karibu na msichana huyo na baada ya urafiki kukolea haswa wawili hawa walijikuta wakianzisha uhusiano wa mapenzi. Kama wasemavyo Waswahili, basi penzi nalo hulevya. Tena hulevya haswa kuliko hata kileo chenyewe, tuseme sasa kileo haswa - mfano wake; vile vyakula vya wazee wetu! Naam; Gongo, ewaa tena ile ya kuitwa namba *one.*

Basi Zinaeda alilewa kwa penzi la kijana huyu wa Kitanga; akawa tayari kumruhusu Biruse afike nyumbani kwake kila mara na ndipo huko Biruse aliweza kugundua taarifa nyingi za msichana huyo kuwa; ni miongoni mwa vijana wadogo wa *KBG,* waliokuwa katika mkakati maalumu wa kiintelejensia wa kupata mafunzo ili kuweza kutumiwa baadaye na shirika hilo.

Toka hapo, Biruse alipanga kuishi kwa akili ya Zinaeda; akawa ni mtu mwenye tahadhari kubwa kwenye kila alichokizungumza pamoja na matendo yake. Lakini, pamoja na tahadhari kubwa aliyoichukua, pasipo kutegemea Zinaeda naye aliweza kugundua ya Biruse kutokana na ujuzi wa kiintelejensia aliokuwa nao.

*Shee!*

Wakati Biruse akijiuliza amekosea mahala gani hata mwanadada

huyo akaweza kugundua jambo hilo, Zinaeda yeye ilimshangaza kutambua amekuwa kwenye uhusiano na Biruse kwa kipindi chote hicho cha takribani mwaka mmoja na sehemu na hafahamu kuwa ni kachero. Ilimshangaza mno!

Hata hivyo, pamoja na hayo yote, hawakuwa na namna. Biruse alimwambia Zinaeda kwa Kimombo; *we're stuck with each other!*

Zinaeda naye alimjibu huyo mwamba; *no way, we have to deal with each other!*

Hawakuwa na chaguo lingine zaidi ya kulimwagilia pendo lao maji kutoka kwenye kisima cha moyo hata liweze kumea na kukua zaidi. Ikawa ni sawa na mbegu ya mmea iliyopandwa. Baada ya kumwagiliwa maji ya bwawani, mche ulichomoza kwenye mgongo wa ardhi na hatimaye mmea ukadhihirika. Hivyo ndivyo unavyoweza kulinganisha pendo la watu hawa lilivyokuwa baadaye.

Basi, baada ya kumaliza muda wao katika Chuo cha Tohoku, Japan, walijiunga kwa ajili ya masomo zaidi katika Chuo Kikuu cha Tsingua, jijini Beijing, kwa ajili ya kujiendeleza zaidi kimasomo.

Siku zikapita. Zikaenda na nyingine zikarudi. Zikajirudia katikati ya majira na nyakati. Zikaonekana tofauti na baadaye zikaonekana sawa. Hatimaye zikatimia zile siku za kuikamilisha ile kauli ya Biruse aliyomwambia Zinaeda: *we're stuck with each other!*

Ilikuwa ni katika hilo sekeseke la maandamano na kuzima umeme wa chuo pamoja na jiji hilo la Beijing.

Ukweli ni kwamba, tofauti na Biruse; ambaye toka akiwa kijana mdogo, akiandaliwa siku moja kuwa kachero na idara ya usalama ya Tanzania, alipitishwa kwenye vikundi vingi vya mafunzo, ikiwemo kuwa skauti, kushiriki mafunzo mbalimbali ya mbio za mwenge, kwenda JKT, na fursa mbalimbali alizobahatika kuzipata; Zinaeda, pamoja na mafunzo yote alikuwa ni mwenye hofu kupindukia.

Hata hivyo, hofu ya Zinaeda haikuwa ya bure. Ilitokana na namna ambavyo analifahamu taifa la China, jinsi lilivyopiga hatua kwenye suala la teknolojia na mawasiliana. Zinaeda alifahamu kuwa, achana tu na kudukua, ilikuwa ni hatari hata kwa mtu kufanya kitendo cha

kuwaza kutenda jambo hilo.

"Ninahisi kama tunajiingiza kwenye hatari kubwa," Zinaeda alisema kwa sauti ya chini, akitazama moja kwa moja kwenye macho ya Biruse. Alikuwa ameshika kikombe cha kahawa, lakini vidole vyake vilitetemeka kidogo ingawa kipoza hewa ndani ya chumba hicho cha Biruse, kilichojikita katika mtaa uitwao Dashilan, kilikuwa chini.

Biruse aliyekuwa ameinama kwenye *laptop* yake, akifanya mawasiliano na marafiki zake ambao walikuwa wanasubiri wasaa ufike waliopanga kwa ajili ya kutekeleza tukio hilo. Biruse aliinua uso na kumtazama Zinaeda.

Kisha baada ya sekunde chache, alipata utashi wa kuiweka *laptop* yake juu ya meza, iliyokuwa karibu na kitanda kile alichokuwa amekikalia, akamsogelea mpenzi wake yule na kukaa karibu yake. Akaweka mikono yake juu ya mabega ya Zinaeda. Akanyoosha mikono na kuishika mikono ya Zinaeda kwa pamoja. Akamwambia:

"sikiliza mpenzi, dunia haitabadilika yenyewe. Watu wanapaswa kusimama na kupinga uonevu. Hiki ndicho tunafanya sasa."

Zinaeda alitabasamu kwa huzuni. "Na ikishindikana?"

"Kila mpango una hatari zake," Biruse alisema, akatabasamu kwa kujiamini, "lakini hakuna njia bora ya kupambana na dhuluma bila gharama."

Zinaeda alipandisha kifua na kumwaga pumzi nyingi nje. *Ohuuuuu!* Mawazo yake na utashi wake vinapingana. Anatamani sana kushiriki katika kila mpango ambao mpenzi wake Biruse ameuandaa kwa ajili ya kukileta chuo chao kwenye magoti yake, lakini utu wake wa ndani umenyong'onyea na unamwambia hilo jambo ni hatari mno hasa akiwaza juu ya taifa hilo la China na maendeleo yake ya teknolojia.

Ukimya wa haja ulijengeka na akiwa katikati ya ukimya huo; mara Biruse alimuita: "Zinaeda," aliita kwa sauti ya chini iliyosikika vyema. Zinaeda aliinua uso na kumtazama mpenzi wake yule.

"Usiogope, tunakwenda kuandika historia." Biruse alimwambia.

"Historia ni sawa tunaweza kuandika maana kwa *software* niliyonayo tunaweza kufanikiwa kabisa, lakini kumbuka hili taifa lina sheria kali B. Lazima tutakamatwa tu, ama kama si sisi, basi kuna wenzetu wanaweza kwenda jela hata kwa kipindi chote cha maisha yao kwa jambo hili tu tunalokwenda kufanya."

"Ninafahamu mpenzi, lakini hakuna jambo lisilo na gharama yake. Tunachotazama sasa ni kuwafundisha adabu hawa washenzi, ili wafahamu umuhimu wa kuheshimu ubinadamu. Kitendo walichomfanyia Fanta si sawa kabisa. Si kitendo cha kibinadamu. Nina uhakika tukifanya jambo hili na dunia ikafahamu ni kwa nini tumefanya itasimama pamoja na sisi. Usiwe na hofu na kuna uwezekano mkubwa asiwepo hata mmoja wetu atakayepatwa na jambo baya katika utekelezaji wa mpango huu!"

Zinaeda alijikuta akishusha pumzi ndefu kwa mara nyingine. Katika maisha yake yote, hajawahi kushiriki, achana na jambo la namna hii wanalojiandaa kufanya, bali hata migomo ya shuleni ama vyuoni. Siku zote, katika nyendo zake alijitahidi kuwa makini ili asiwape sababu watu kumfuatilia hata kugundua kuwa ni kachero wa KGB!

Siku hii, ama tuseme nyakati hizi, kinachomponza ni uhusiano wake na Biruse, ambaye matukio kama haya, yeye alikwisha yazowea. Utashi wa Zinaeda ni kutokutenda tukio hili, lakini nguvu ya mapenzi inamvuta na analazimika kusimama pamoja na mpenzi wake.

Kwa upande wa Biruse, matukio ya namna hii yalikuwa ni matukio ya kawaida mno. Toka akiwa sekondari amekuwa akiongoza migomo ya wanafunzi, na migomo yake mara nyingi ilikuwa inasababisha kadhia kubwa. Tabia hiyo, huko nyuma ilikuwa ni ya ujana maji ya moto. Baadaye baada ya kupitishwa kwenye mafunzo mbalimba ya kiintelejensia aliweza kuachana na tabisa hiyo. Lakini leo mzimu uliolala kwa kipindi kirefu ndani yake ulikuwa umeamshwa kutokana na kitendo kile cha kidhalilishaji alichofanyiwa Fanta.

Na kutokana na uzoefu wake katika matukio, Biruse alifahamu

anakwenda kuitikisa China kwa kile kinachokwenda kufanyika, na kiu yake ni jina lake libaki katika taifa hilo milele. Kwamba, hata miaka mingi ikipita, China itambue kwamba kuna mwamba kutoka Tanzania aitwaye Biruse alipita taifani hapo. Na wala kijana huyu hakuwa anajali jambo gani litampata.

Alifahamu wazi, taifa hilo linasheria kali na kama ambavyo Zinaeda alikuwa akiwaza na kuhofu; China ilikuwa imeendelea kwenye teknolojia, na kwa kitendo hicho alichokuwa anakipanga kukifanya pamoja na wenzake, ni tukio ambalo linaweza kumpeleka jela kwa kipindi chote cha maisha yake. Kama si yeye, basi wenzake. Lakini, Biruse hajali juu ya hilo. Biruse anachoamini siku zote kuna njia ya kutokea na amekwisha panga njia kadhaa kichwani kwake kwa namna ambavyo atauepuka mkono wa dola yeye pamoja na washirika wake.

Kwa upande wa Zinaeda, jambo lingine ambalo lilikuwa linampa ugumu kushiriki kwenye mpango huo ni juu ya familia yake. Zinaeda alikuwa na kazi kubwa ya kujilinda katika mienendo yake kutokana na kuwa, baba yake alikuwa ni ofisa wa siri wa Taasisi ya Kijasusi ya Komitet Gosudarstvennoy Bezopasnosti *(KBG)*.

Na Zinaeda alifahamu, ikitokea kwa namna yoyote akadakwa na jeshi la usalama wa China kwa tukio hilo linalotakiwa kwenda kufanyika, utakuwa ni mwanzo wa kuchimbwa kwake na si ajabu taarifa juu ya baba yake zikawekwa wazi. Jambo ambalo hakuhitaji litokee kabisa. Kwahiyo, Zinaeda alikuwa ni mwenye hofu kubwa mno!

*****

Wakati hayo yakiendelea kati ya Biruse na Zinaeda, katika upande mwingine, Fanta, msichana ambaye ndiye hasa amepelekea kuwepo kwa mipango hiyo ya maandamano na yote yaliyokuwa yanapangwa nyuma ya pazia, kutokana na tukio la kibaguzi lililompata, yupo chumbani kwake katika eneo la hosteli za chuo hicho, pamoja na rafiki yake wa kike aitwaye Destiny, msichana mweusi mwenye asili ya Marekani, wakisubiri wakati uwadie waweze kuungana na

wenzao.

Fanta na Destiny, walikuwa kwenye mazungumzo yao, wakijadili namna ambavyo Biruse alilishikia bango tukio hilo pamoja na mipango aliyowaeleza.

"Huyu jamaa ni mwanaume wa shoka!" Fanta alimsifia Biruse.

"Mh! Hana uoga kabisa." Destiny naye alishadadia, "bila yeye sidhani ikiwa haya yote yangewezekana."

"Mtanzania huyo. Hawa watu nchini kwao kumejaa amani tele. Lakini ni majasiri. Mahali popote sijawahi kukutana na Mtanzania legelege."

"Lakini…" mwishowe Destiny alimvuta usikivu Fanta, "tumewaza baada ya hili tukio maisha yetu ya kusoma yatachukua sura gani hapa chuoni ama kuishi hapa China? Tukumbuke tupo China na si Marekani ama mataifa mengine. Sheria za hapa ni nyingine kabisa."

"Ni kweli, lakini hayo maisha yetu mpaka sasa yana sura gani Destiny? Si ni ubaguzi tu unaoendelea katika hili taifa? Umefika wakati tufikirie juu ya miaka kumi mpaka ishirini mbele, wakati wa wadogo zetu ama watoto wetu.

"Unajua kwa kiasi kikubwa tumefika hapa kwa sababu mababu na babu zetu hawakuwa wabinafsi. Kama na wao wangejifikiria wao wenyewe; kwamba wangeishije watakapoanzisha harakati za kukomesha masuala ya utumwa, huenda mpaka leo tungekuwa watumwa. Lakini, waliweka ubinafsi wao pembeni wakaamua kujitoa kwa namna ya liwalo na lile!

"Hilo ni funzo kubwa mno kwetu. Nasi, hatuna budi kwa sasa kusimama na kupigania kile ambacho tunaona ni sawa na kupinga kile ambacho si sawa pasipo kujali gharama gani tutaingia. Na huko ndiyo kujitambua. Ila tukibakia hii ni China na si Marekani, ni ngumu kuondokana na minyororo ya ubaguzi."

Destiny hakuzungumza haraka. Alibaki kimya akitafakari jambo wakati maneno yale yakijichimbia ndani kabisa ya keto za akili yake; na baada ya sekunde kadhaa za ukimya, akasema; *"anyways…"* aliongea taratibu akionyesha kuzidiwa hoja ama kukubali yaishe,

kisha akaongeza, “tuyaache hayo sasa, ila kusema ukweli wa moyo, ninampenda sana Biruse.”

Fanta, ambaye hakutegemea Destiny angehama kwenye mazungumzo yao haraka namna hiyo, alipepesa macho na kuyatuliza usoni mwa Destiny, kisha akajenga tabasamu hafifu usoni mwake na kutania: “Naye Biruse anampenda Zinaeda…”

*Mchii!*

Destiny alibwaga kite cha kupuuzia jambo hilo ambalo Fanta aliliibua. Mara kwa mara, Destiny amekuwa akimweleza rafikiye huyo juu ya mapenzi ya dhati aliyonayo dhidi ya Biruse. Namna ambavyo, amekufa na kuoza; lakini kila amwelezapo, Fanta humsihi ajihusishe na wanaume wengine kwa sababu, Biruse alikuwa kwenye uhusiano wa kimapenzi na Zinaeda, na kwa namna walivyokuwa wanapendana, hakuona Biruse akiwa tayari kumuacha mpenzi wake huyo kwa ajili ya Destiny.

Na jambo lingine, hata dalili kwamba jamaa huyo anaweza kumsaliti hazioni!

Lakini, Destiny naye mapenzi yamekuwa upofu. Haoni wala hasikii. Kila siku anachowaza ni jambo la kufanya ili kuweza kuwatenganisha watu hawa wawili naye achukue nafasi, na si kumuepuka Biruse. Hata hivyo, mpaka wakati huu alikuwa hajapata jambo la kufanya. Ila kupitia tukio hili, ambalo linakwenda kufanyika la maandamano na uharibifu wa miundombinu katika chuo chao hicho cha Tsingua, kuna mawazo Destiny ameyapata ambayo anayaona wazi yatasaidia kumtenganisha Biruse na Zinaeda.

“Kuna siku tu Biruse atakuwa wangu.”

“Unaota Destiny, hebu amka.”

“Sawa. Wewe endelea kuona ninaota lakini ipo siku utasadiki.”

*“Khm!”* Fanta aliguna," “wenzako wale kila unavyowaza wataachana ndivyo wanazidi kupendana, unapoteza muda wako bure.”

“We subiri, utajionea mwenyewe.”

“Haya, yangu macho.”

# 2

*Saa 2 na dakika zake, usiku.*

Hali ya hewa ilikuwa tulivu mno kwenye majira haya katika jiji hili la Beijing. Jiji ambalo, limetawaliwa na alama nyingi za kihistoria zinazoeleza juu ya taifa hili la China na jiji hili ni miongoni mwa majiji yenye utajiri mkubwa na makazi ya watu matajiri zaidi duniani.

Utulivu huo uliokuwa umelimeza jiji hili la Beijing, ndio huo huo ambao ulikuwa umeenea katika Chuo Kikuu cha Tsingua.

Katika majira haya, tayari Biruse na kikundi chake walikuwa wamekwisha weka sawa mipango yao ya kuanza zoezi la uharibifu wa miundombinu chuoni hapo.

Mambo mawili ambayo yalikuwa yamebaki, ilikuwa ni Biruse kwenda kwenye senta iliyokuwa inasambaza umeme chuoni hapo na kuweka *'off' 'switch'* ambayo ingepelekea chuo kizima kukosa umeme.

Na jambo la pili ilikuwa ni kuzima umeme wa jiji zima, malengo yao yakiwa kuwachelewesha askari polisi wakati ambao vikundi vyao vitakuwa vikitenda uharibifu waliokuwa wamekusudia kuufanya, jambo ambalo tayari kwa kiasi kikubwa lilikuwa limekwisha onyesha mafanikio maana Biruse amekwisha iingilia *systeam* ya umeme ya mji huo kupitia kwenye komputa yake akisaidiana kwa ukaribu zaidi na Zinaeda..

Biruse akiwa chumbani kwake alimpa maelekezo yote Zinaeda ya nini afanye kwenye komputa yake kuhakikisha umeme wa jiji hilo unazimika na alimsisitiza kitendo hicho akifanye baada ya dakika

ishirini kupita, baada ya yeye kuondoka hapo, kwani alifahamu mpaka majira hayo atakuwa amekwisha fanikisha zoezi la kuzima umeme chuoni.

Baada ya kutoa maelekezo hayo, Biruse aliagana kwa mabusu motomoto na mpenzi wake Zinaeda, wakatakiana kila lenye kheri, ndipo kijana huyo alitupia sweta la *'poolover'* mwilini mwake, akachukua baiskeli yake na kutoka ndani ya chumba hicho.

Baada ya muda wa dakika saba, Biruse alikuwa tayari amekwisha ingia kwenye chuo cha Tshingua, na alipofika, kwa tahadhari kubwa alianza kuelekea moja kwa moja kwenye chumba maalumu kulipokuwa na *'system'* hiyo aliyopaswa kuizima.

Chumba hiki kilikuwa ni chumba nyeti mno. Ni chumba ambacho hakuna mtu aliyeruhusiwa kufika tofauti na walinzi ambao walilinda zamu kwa zamu; wawili katika zamu moja na wawili wengine walifuata baada ya zamu ya wenzao kuwa imemalizika. Hata hivyo, mbali na walinzi hao, kulikuwa na kamera ambayo ilikuwa inamulika wakati wote ndani ya chumba hicho ili kudumisha ulinzi zaidi na kulikuwa pia na taa maalumu iliyokuwa inaangaza kila kona ya chumba hicho.

Hayo yote Biruse aliyafahamu na wenzake waliyafahamu. Na ili kufanikisha zoezi lao, walikuwa wamekwisha jipanga toka mapema yeye pamoja na wenzake; ambapo kijana mmoja wa Kisomalia aitwaye Mohammadou Alli, alipaswa kufanya juu chini kwenda kuingia kwenye chumba cha kamera na kuwadhibiti watu waliyokuwa kwenye chumba hicho na yeye kushika mamlaka, ili Biruse aweze kupata wepesi wa kuingia kwenye chumba cha data pasipo kuwa na rapsha yoyote ile.

Kwa hiyo, wakati Biruse ameanza kuingia kwa tahadhari kwenye chumba cha data, Mohammadoe naye alikuwa katika harakati za kuelekea kwenye chumba cha kamera.

Kwa upande wa Mohammadoe, hiyo haikuwa kazi rahisi. Hofu ilikuwa kubwa ukizingatia Mohammadou hakuwa na uzoefu kwenye mambo haya ya kijasusi. Lakini pia, sheria za nchi hii ni kali

mno. Wote walifahamu kwa namna yoyote ile ikitokea wakatiwa nguvuni, basi hiyo ilimaanisha kwenda jela kwa kipindi cha miaka mingi ama kipindi cha maisha yao yote.

Hata hivyo, nia ya dhati ya kulifundisha taifa hilo la China juu ya kuacha masuala ya ubaguzi ndiyo iliyowasukuma, na ilimfanya Mohammadoe pamoja na kutokuwa na uzoefu awe na moyo wa ujasiri. Wakiwa kwenye vikao vyao, kabla ya wakati huo walikumbushana juu ya mashujaa wa Kiafrika waliofanya mambo makubwa na kuwa tayari kwa lolote, wengine hata kufa kwa ajili ya mataifa na asili zao.

Ambao baadhi yao ni kina Blaise Diagne, Julius Nyerere, Abdel Nasser. Samuar Toure, Patrice Lumumba na Thomas Sankara. Kwahiyo, kijana huyo aliuvaa moyo wa ujasiri wa hao mashujaa!

Mohammadou alivuta pumzi ndefu, kisha kwa uangalifu mkubwa aliingia kwenye korido ndefu iliyokuwa inaelekea kwenye chumba kile cha kamera. Na mkononi kijana huyo wa Kisomali alikuwa ameshika chupa ndogo ya sumu iitwayo *Ricin*, aliyokuwa amepewa na Biruse.

*Ricin* ni sumu hatari inayoua haraka mno kwa njia ya hewa na Biruse aliipata sumu hiyo kabla kwa lengo la kuwarahisisishia zoezi lao lile, ambapo naye kama ilivyokuwa kwa Mohammadoe alikuwa ameshika ya kwake mkononi akielekea kwenye chumba cha data.

Kwa umakini mkubwa, Mohammadoe alizipanda ngazi ambazo ndizo zilikuwa zinampeleka juu kulikokuwa na chumba kile cha kamera. Wakati anazidi kupanda, akiwa umbali mfupi wa kuzimaliza ngazi zile, mara alisikia watu wakizungumza na wakitembea kuelekea uelekeo alipokuwa. Sauti zile zote zilikuwa ni za kiume.

Mahammadoe alishituka mno. Mapigo ya moyo wake yalianza kumwenda mbio kijana huyu. Hakutegemea kabisa kukutana na watu katika eneo hilo. Kutokana na uzoefu waliokuwa nao pamoja na taarifa za eneo hilo, sehemu pekee ambayo alikuwa anauhakika angekutana na mlinzi ni karibu na chumba cha kamera. Sasa hawa ni kina nani?

Mohammadoe alitazama nyuma, aliona ni mbali akisema afanye maamuzi ya kurudi kwenda kutafuta mahala pa kujificha ili watu hao wapite.

Kupitia kwenye vifaa maalumu vya kusikilizia alivyokuwa amevaa masikioni alivyounganisha na simu yake, alimweleza Biruse kilichokuwa kinaendelea.

*"Shit!"* Biruse alijibu akionyesha kuhamanika.

"Nafanyaje kaka?" Mahammadoe alimuuliza.

"Kabiliana nao."

"Kivipi?"

"Tumia sumu."

"Sawa, wanazidi kusogea, tulia…"

Mohammadoe aliitumikisha akili yake haraka juu ya maamuzi gani achukue, na ndipo alipoamua kujitoa muhanga kwenda kukabiliana na watu hao. Kijana huyo alipandisha kifua juu na kukishusha kwa mkupuo mmoja, akamwaga nje pumzi nyingi, kisha akazipanda ngazi kwa mwendo wa kasi na ile amefika tu juu alikutana na watu wale ana kwa ana.

Watu hao, ambao wote walikuwa na asili ya China walisimama ghafla baada ya kumuona, naye akasimama.

"Wewe ni nani na unatafuta nini huku?" Mmoja wa watu wale alimuuliza.

"Nyie ni kina nani mpaka mniulize swali hilo," Mahammadoe aliwajibu kwa jeuri.

Watu wale walihamanika. Vitendo vya huyo mtu mbele yao viliwashangaza. Na kilichowashangaza zaidi ni namna alivyokuwa amevaa. Ni mtu ambaye moja kwa moja alionekana amejipanga kwa uhalifu na si vinginevyo.

Hata hivyo, wakiwa bado katika hali hiyo, mambo mengi yakizunguka akilini mwao, Mohammadoe alianza kuwasogelea. Mmoja wa watu wale, aliyekuwa mwepesi zaidi, kwa kitendo cha haraka alichomoa bastola yake kiunoni. Lakini, alikuwa amekwisha chelewa. Mohammadoe wakati anasogea aliipuliza sumu ya *Ricin*

aliyokuwa nayo mkononi. Sumu hiyo inauwezo mkubwa mno wa kuleta madhara kuanzia pale tu mtu anapoivuta. Na hicho ndicho kilitokea. Yule jamaa ambaye alichomoa bastola, ambaye ni miongoni mwa walinzi katika eneo hilo. Alipojaribu kuinua mkono wake ili amnyooshee mkono Mohammadoe alishindwa. Aliuhisi mkono ni mzito mno. Ilikuwa ni kana kwamba ulikuwa umefungwa mawe makubwa yenye uzito wa kumshinda nguvu.

Hali iliyomtokea huyo bwana, ndiyo hiyo hiyo ilimtokea mlinzi mwenzake. Naye baada ya kugundua Mohammadoe hakuwa mtu mzuri mbele yao alijaribu kukukuruka ili aweze kuchukua bastola kiunoni mwake. Lakini alishindwa. Mwili ulimsaliti. Viungo vyote vilipoteza ushirikiano na akahisi hana nguvu zozote zile. Na pasipo kutarajia watu wale wawili walidondoka sakafuni utasema mizoga.

Mohammadoe alishusha pumzi ndefu akiwatazama wale watu. Hakika kitendo kilichotokea ni muujiza mkubwa kwake. Kuna nukta alifikia moyo wake ulijawa na mashaka makubwa juu ya kuwakabili watu hao.

*"Two man down, over…"* Mohammadoe alimwambia Biruse, akizungumza kwa mbwembwe, kupitia kwenye vifaa vya kusikilizia alivyovaa masikioni ambavyo aliviunganisha pamoja na simu yake.

"*Copy that…*" Biruse alimjibu.

Mohammadoe macho yake yalikuwa kwa wale watu pale chini. Anawatazama akijiuliza awafanyeje. Ndipo akawaza kwamba atafute mahala pa kuwaweka. Aliangaza huku na huko, lakini katika eneo alipokuwa koridoni pale, haikuwa rahisi kusema awavute wale watu na kwenda kutafuta mahala pa kuwahifadhi ili wasiweze kuonekana.

Akijadili na akili yake mwisho alijiambia; "potelea mbali," aliamua kuiruka miili ya hao watu akaendelea kusonga mbele kwenda kwenye chumba cha kamera.

*****

Kwa upande wa Biruse naye alikuwa hatua chache mno kutoka

kwenye chumba cha data. Dakika zinazidi kuyoyoma. Akitazama saa yake, ni takribani dakika mbili zimebaki uweze kutimu ule muda ambao alimweleza mpenzi wake Zinaeda azime umeme wa mji huo kupitia kwenye komputa yake maana tayari alikuwa amekwisha *'zi-hack' 'systeam'* za usambazaji wa umeme katika jiji hilo la Beijing.

Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa Mohammadoe, Biruse alivyofika karibu na chumba cha data, alisikia kuna watu wawili wakiongea jirani na chumba hicho.

Moja kwa moja akili yake ilimweleza kuwa, inawezekana watu hao ni watu wanaolilinda eneo hilo.

Biruse kwa ujasiri mkubwa alianza kutembea kwa kunyata, akitumia vidole vyake vya miguu, mpaka akafika mwisho wa ukuta, jirani mno na mahali pale ambapo wale watu wawili walikuwa wakizungumzia.

Akili yake ilizunguka mfano wa pia. Alipiga hesabu zake kichwani na akaona hakuna namna ya kuwakabili wale watu pasipo kujitokeza. Ndipo Biruse alipoamua kujitokeza.

Wale watu wawili ambao kama alivyodhani walikuwa ni walinzi, walihamanika sana kumuona. Macho yaliwatoka maana mahala kule hakutegemewa kuonekana mtu yeyote yule, tofauti na walinzi ama mtu aliyefika kwa kibali maalumu.

Sasa huyu mtu ni nani na amefikaje huku? Walijiuliza.

Na wakiwa bado kwenye maswali yao, Biruse alifanya kile kile kilichofanywa na Mohammadoe, kunyunyiza sumu ile ya Ricin aliyokuwa ameishika mkononi, haikuchukua sekunde saba mbele watu wale walipoteza utashi wa kumkabili, wakadondoka chini.

Kutokana na muda kuwa umekwisha muacha, Biruse hakutaka kujihangaisha na watu wale, alichofanya ilikuwa ni kumsachi mmoja kati yao na kutoa kadi maalumu kwa ajili ya kufungulia mlango wa chumba kile cha data, alipofanikiwa hilo, moja kwa moja aliuendea mlango wa kuingia kwenye chumba kile.

Hata hivyo, katika hali ambayo hakuitarajia, Biruse alipofungua

tu chumba kile cha data, wakati ameingia ndani, mara alamu ya usalama katika majengo yale ilianza kupiga kelele.

*“wiiiiiwiiii wiiiiiwiiiiiii wiiiiwiiiiii!”*

*Hee!* Kitendo hicho kilimuogopesha mno Biruse.

“Mohammadoe!” aliita kwa hamaniko akizungumza kupitia vifaa vya masikioni alivyokuwa ameviunganisha naye kwenye simu yake.

“Nambie…”

“Nini kinatokea.”

“Walinzi wengine wamebaini miili ya wale washenzi wawili niliokutana nao njiani.”

*“Doh!”*

“Sema nipo kwenye chumba cha kamera.”

“Hata mimi nipo kwenye chumba cha data.”

“Fanya haraka sasa kuzima. Nzi sasa hivi watajaa.”

“Poa poa.”

Biruse alisonga ndani zaidi ya chumba kile, mpaka kwenye ule mtambo wa data, alitazama kwa umakini ilipokuwa *switch* ya kuzimia. Ambapo, hiyo system ilikuwa imeunganishwa na jenereta. Na laiti kama Biruse asingekwenda kuzima, akasubiri Zinaeda azime umeme wa jiji hilo, bado hapo chuoni kungetawaliwa na mwanga kutokana na mfumo uliokuwa umesukwa wa kuhakikisha umeme haukosekani saa ishirini  na nne mahali hapo.

Basi, Biruse alipoingia, mara aliiona ile *switch.* Pasipo kupoteza muda aliibonyeza na tendo sawa na la kufumba na kufumbua macho, umeme ulizimika katika eneo lote la chuo hicho, jambo ambalo halikuwahi kutokea toka chuo hicho kianzishwe!

“Kazi kwisha!” Biruse alimwambia Mohammadoe.

“Kazi nzuri *comred*.”

“Fanya hima kutoka huko.”

“Poa poa.”

NJE ya majengo hayo, kikundi cha vijana, wenzake na kina Biruse, kilichokuwa kimekwisha jipanga juu ya jambo lile la kufanya uharibifu katika chuo hicho, baada ya kuona umeme umezimika katika chuo hicho na kwenye jiji lote la Beijing, kiliingia ndani ya eneo la chuo kwa fujo, na kuanza kufanya uharibifu wa kila aina.

Kikundi hicho kilivunja vioo vya madarasa na kila kitu kilichokuwa mbele yao ambacho kilikuwa na thamani. Walikwenda kwenye mgahawa wa chuo hicho na kutupa vitu pamoja na vyombo nje, wakaelekea mpaka maktaba wakafanya nako uharibifu mkubwa, na wakaendelea kufanya uharibifu katika maeneo mengine mengi.

Hata hivyo, ndani ya dakika kumi mbele, tayari umeme katika jiji la Beijing ulikuwa umekwisha rejeshwa na wataalamu wa *IT,* na polisi walikuwa wamekwisha mwagika kama mvua katika eneo la chuo hicho.

Hapa ndipo patashika iliianza kati ya wanafunzi wale na polisi. Hata hivyo, ni ngumu kwa jiwe kushindana na nazi; kwa namna ambavyo, polisi walikuwa wamejipanga, lilikuwa ni jambo gumu mno kwa wanafunzi kukabiliana nao. Wanafunzi wengi, wakajikuta wakiishia mikononi mwa polisi, akiwemo kiongozi wa mpango ule, Biruse!

# 3

*Mosccow, Urusi.*

Mzee Dimitir Roshkeov, akiwa ndani, kwenye chumba chake cha mapumziko, anatazama taarifa ya habari kupitia kwenye chombo cha habari maarufu duniani kiitwacho *Al Jazeera,* huku anasukuma muda kwa kunywa kahawa yake taratibu.

Akiwa katika utulivu huo, mara simu yake ilianza kuita. Simu hiyo, ilimtoa katika utulivu aliokuwa nao. Amekaa kwa muda kitambo mahali hapo, kwa hiyo, uchovu pia ulikuwa umekwishauteka mwili wake na Dimitir, hesabu zake zilikuwa, baada ya taarifa ya habari aelekee chumbani kwake kulala.

*Sasa nani anampigia simu majira haya?*

Alijiuliza.

Hata hivyo, pamoja na maswali yote yaliyoibuka kichwani mwake, akijiuliza juu ya simu ile, mzee Dimitir; hakuwa na utashi wa kusema asiipokee simu ile ama kuipuuzia. Kwa hiyo, kwa uchovu alijikakamua na kuusukuma mkono wake, akaichukua simu yake juu ya sofa, lililokuwa pembeni ya mahala pale alipokuwa amekaa.

Kwa sekunde chache alisoma jina la mpigaji.

*PR!*

Ndivyo kioo cha simu yake kilivyosomeka. Akafahamu kuwa, moja kwa moja, anayempigia simu ni mkuu wake wa kazi, Kamishina Putim Rendozovic; aliyemhifadhi kwenye simu kwa kifupi cha jina lake, akichukua herufi ya kwanza na ya mwisho. Aliipokea simu hiyo.

“Bosi!” Mzee Dimitir aliitika.

“Unaendeleaje?” Upande wa pili uliuliza.

“Nipo sawa, nashukuru. Wewe?”

“Si mbaya.”

“Nambie mkuu. Simu zako za usiku huwa zinatisha.”

*Khm!* Kamishina Putim, alisukuma mguno. Kana kwamba alitaka kucheka lakini hakucheka. Ndipo akamwambia: “Ndivyo zilivyo kazi zetu. Hakuna namna.”

“Ni kweli kabisa. Lete khaifa…”

“Upo na nani hapo?”

Swali la Kamishina Putim, lilimshitua kwa kiasi fulani mzee Dimitir. Ikabidi apepese macho kutazama huku na kule ikiwa mke wake alikuwa karibu na mazingira hayo, hakumuona.

Basi akamjibu: “Nipo mwenyewe.”

Ndipo Kamishina Putim, alimpa mzee Dimitir, taarifa za kushitua, zilizomhusu binti yake Zinaeda!

Uzuri wote wa siku hiyo ya afisa huyu wa kikundi nyeti cha usalama cha *KBG,* ulitoweka.

Zinaeda, ni binti yake wa pekee. Anampenda sana binti huyu na ni roho yake na mkewe. Kusikia juu ya taarifa mbaya kumhusu, kama ambavyo, ameelezwa na Kamishina Putim, lilikuwa ni jambo lililomuumiza mno.

Hata hivyo, mzee Dimitir, alijiasa mwenyewe kuwa mtulivu ili asisababishe sintofahamu kwenye familia yake hasa kwa mkewe ambaye alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya moyo na presha.

Pasipo kupoteza muda haraka, mzee Dimitir alisimama; kwa mwendo wa mbiombio alianza kupiga hatua kutoka sebuleni hapo, akalishika korido na hatimaye alianza kukwea ngazi zilizoelekea ghorofani kulikokuwa na chumba chake, baada ya kufika alivaa mavazi kwa ajili ya kutoka, akachukua bastola yake na kuipachika kiunoni kisha akashuka mpaka sebuleni.

Katika wakati huo, mkewe aliyekuwa jikoni kwa kipindi cha muda, ndiyo alikuwa anatoka huko. Alipomuona katika hali hiyo, ilimshitua na kumfanya ajawe na mshangao mdogo usoni. Akamuuliza:

*kulikoni?* Maana muda mchache uliopita, alikuwa amevaa bukta na vesti na alimuacha amekaa sebuleni tena kwa kubweteka. Lakini, ghafla, sasa amekwisha vaa mavazi yaliyomuonyesha wazi kwamba alikuwa mbioni kutoka. Na halikuwa jambo la kawaida, kwa Dimitir, kutoka nyumbani haswa majira ya jioni akisharejea, isipokuwa kila kulipokuwa na suala mahususi, linalohusu kazi zake za kiusalama.

Dimitir, alishusha pumzi fupi akimtazama mkewe.

"Ama kazi zenu hizo tayari zinaniharibia muda na mume wangu!" Mkewe alisema, akijiongeza kutokana na uzoefu aliokuwa nao wa mitoko ya namna hiyo ya mumewe.

Na kuusema tu ule ukweli, hakuna jambo lililokuwa linamkwaza kama hilo. Kitendo cha mumewe kufika nyumbani, kisha kutoka kwa sababu ya kazi huwa kinamkwaza sana, kiasi kwamba, kuna kipindi huwa inafika mwanamke huyu anajuta kuolewa na afisa usalama.

Kuna muda anahitaji ukaribu zaidi na mumewe hasa awapo katika eneo la nyumbani, lakini Dimitir akisha pigiwa simu moja tu, inayohusiana na kazi, hata kama alikuwa anatekeleza majukumu yake ya ndoa, hulazimika kuachana na majukumu hayo na kuelekea kazini.

Dimitir, aliyekuwa anafahamu kinachoendelea, kwamba mtoko wa siku hii, si kama ile ambayo mwanamke huyu anaifahamu, alirusha mikono hewani, akimaanisha hana la kusema. Lakini pia, alikuwa akijitahidi kutengeneza utulivu usoni kwake ili mkewe asibaini kuwa, kuna jambo ambalo haliko sawa kwenye familia yao.

Baada ya kitendo hicho alichokifanya cha kurufsha mikono, Dimitir alimsogelea mkewe, akamzungushia mikono kiunoni kwake na kumvutia karibu naye zaidi, ndipo akamweleza;

"Usijali sana mke wangu, karibu nastaafu kazi, haya yote yatakwisha!" Alisema kwa sauti la utulivu akijilazimisha kuchanua tabasamu hafifu usoni.

*Khm!* Mkewe aliishia kuguna.

Macho ya mkewe, yalivyokuwa yanaonyesha kutoridhishwa na yeye kutoka, lilikuwa ni jambo lililomuumiza pia moyoni Dimitir. Kwa upande wake, kitendo hicho, kilikuwa kinatafsiri juu ya upendo wa dhati ambao mwanamke huyo alikuwa nao kwake na uhitaji alionao juu yake. Ni kitendo kilichofanya hata atamani kumweleza kuwa; binti yao wa pekee Zinaeda, hayupo salama. Yupo matatani na hicho ndicho kinachomlazimisha atoke na kumuacha yeye mwenyewe! Lakini, Dimitir, asingeweza kufanya hivyo, kutokana na mambo makubwa mawili: moja; hali ya maradhi ya mkewe. Lakini jambo la pili, anahitaji kuzifahamu taarifa hizo kwa undani, ndipo aweze kutafuta namna njema ya kumweleza mkewe katika hali ambayo anafahamu kuwa ataweza kukabiliana nayo.

Dimitir alimeza mate ya uchungu, akizidi kujikaza kiume. Kisha akalazimisha kuonyesha hali ya kwamba yupo sawa, ndipo alifanya utani kwa mkewe:

"Na nikistaafu tu kazi, hatuishi tena Urusi…"

Na kabla mkewe hajamjibu, akimtazama kwa macho yaliyoashiria anamsikiliza; aliendelea:

"Tutahamia Havana, Cuba!" Alisema akijenga tabasamu.

Kisha alimbusu mkewe kwenye kipaji cha uso, ndipo akamuachia. Na alipokuwa anapiga hatua za kutoka, alirusha mkono na kumchapa mkewe kibao cha makalioni kwa utani.

"Aii! Wewe!" Mkewe alisema akijishika makalioni pale alipompiga.

Dimitir aliangua kicheko huku akifungua mlango.

*"Bye!"* Alisema wakati mlango ukijibamiza nyuma yake.

Nusu saa baadaye, tayari Dimitir alikuwa amekwisha fika katika eneo lao la siri, kulipokuwa na ofisi za *KGB*. Alipofika tu, moja kwa moja alielekea kwenye chumba cha kamishina wake Putim.

Dimitir alikaa mbale ya meza ya Kamishina Putim, na kamishina huyo alimueleza kile kilichokuwa kimetukia.

"Binti yako ameshirikiana na kikundi cha vijana wahalifu na

wamefanya maafa makubwa mno chuoni kwao. Jambo baya zaidi, vijana hawa wame-hack system ya umeme ya mji mzima wa Beijing na kuuzima."

Dimitir alifinya macho, kitendo kilichosababisha ndita kadhaa zikusanyike usoni mwake. Taarifa anazopewa kwa kweli zinakita mpaka moyoni mwake. Binti yake Zinaeda, ni msichana mkimya na mtulivu sana. Hana makundi wala marafiki wengi. Amemlea katika misingi mizuri ya dini na amekuwa akimweleza mara kwa mara, juu ya namna gani anapaswa kuishi kutokana na kazi ambayo yeye anaifanya. Sasa nini kimempata mwanaye mpaka aweze kushirikiana na kikundi hicho ambacho sasa kimebatizwa jina, kuwa ni kikundi cha kiharamia? Majibu yalikuwa mbali kupatikana.

Dimitir akiwa kimya, kamishina Putim, aliendelea: "Kitendo walichofanya, si cha kawaida na kinachukuliwa kuwa ni ujasusi. Kwa taarifa nilizozipata kutoka kwa watu wetu waliyopo Beijing, zinadai pia, Zinaeda amechukuliwa na gari linalodhaniwa kuwa ni la jeshi la polisi la China, lakini wamejaribu kufuatilia inaonyesha hajapelekwa kituoni."

"Unamaanisha nini?"

"Hajulikani alipo?"

"Hilo gari linadhaniwa, kwa maana yake si gari la polisi?"

Kamishina Putim, alipandisha kichwa na kushusha akimaanisha Dimitir, yupo sawa kwa hoja yake ile. Na pia, akaongeza;

"Kwa mujibu wa mtoa taarifa amesema kuwa, gari hiyo ilikuwa na namba binafsi. Kwahiyo, imefanywa kuwa kama gari ya polisi, lakini si ya polisi."

Kwa mara nyingine Dimitir, alilazimisha mate kupita kooni mwake. Akashusha pumzi fupi na kurudisha mgongo wake kwenye kiti.

"Inabidi niende huko." Mwishowe alisema akijiinua pale kitini.

"Hakika,' Kamishina Putim, alikubaliana naye. Aliendelea kuzungumza: "Kungekuwa na mtu mwingine ninayemuamini ningesema aende. Lakini, sijampata. Sasa pamoja na kwamba, ni

jambo gumu na zito kwako, lakini huna budi kwenda kukabiliana nalo. Nami nitakuwa nyuma yako katika kila jambo."

"Hakuna shida kamishina."

Baada ya mazungumzo hayo, Kamishina Putim, alimweleza kuwa, baada ya nusu saa safari yake itakuwa imekwisha andaliwa, na ataweza kupelekwa na ndege maalumu ya usalama mpaka China.

Walipeana mikono, na Dimitir alitoka ndani ya chumba cha Kamishina Putim, kwa ajili ya kufanya maandalizi machache juu ya safari yake ama kwenda kuusubiri ule muda wa nusu saa, ambao alielezwa kuwa kila kitu kitakuwa kimewekwa sawa kwa ajili ya safari!

*****

Destiny, ni binti mpole kwa muonekano, lakini muongeaji kwa kiasi chake. Binti huyu amezaliwa kwenye familia inayojiweza vyema kifedha; baba yake alikuwa ni mfanyabiashara anayemiliki mgahawa mmoja maarufu katika mji wa Bompton, huko Chicago, nchini Marekani na mama yake alikuwa ni mfanyakazi wa muda mrefu wa mahakamani.

Binti huyu mwenye urefu wa futi tano pointi moja, alipata hata zaidi ya yale aliyoyahitaji kutoka kwa wazazi wake. Hakuna alichoomba akanyimwa na wakati mwingine hakuhitaji kuomba chochote kile. Wazazi wake walipojisikia kumpa chochote ama walipohisi anauhitaji wowote, walimpa pasipo kumpimia. Ilimradi walifanya vile walivyoona ni sawa na itampendeza binti yao.

Pamoja na kupata mahitaji yote ya msingi kutoka kwa wazazi wake, pamoja na maisha ya ghari waliyomzowesha, ila kuna hitaji moja ambalo Destiny alifahamu wazazi hao hawawezi kumpatia. Nalo lilikuwa mapenzi!

Destiny, alihitaji mtu anayeweza kumpa moyo wake, akazimudu hisia zake, akawa pumziko lake na wakapendana kwa dhati.

Alipokuwa nchini Marekani, kabla ya kujiunga na chuo hicho cha Tsingua, Destiny aliwahi kuwa kwenye uhusiano na kijana mmoja wa Kizungu aitwaye Brian.

Yeye na Brian walisoma pamoja toka shule ya msingi. Huko ndiko walikofahamiana. Kutokana na ukaribu waliokuwa nao, walijikuta wakidumbukia kwenye uhusiano wa mapenzi. Destiny alimpenda mno Brian. Alimpa moyo wake wote. Kwa kijana huyo, alijiona amefika na hakuiona dunia nyingine ya mapenzi zaidi ya hiyo aliyokuwa anaishi. Akawa tayari kufanya lolote kwa ajili ya kijana huyo.

Wakati mwingine, alichukua pesa nyingi kutoka kwa wazazi wake na kumpa Brian baada ya hali ya uchumi ya nyumbani kwao na kijana huyo kuwa imeyumba.

Brian akawa ni mwanaume wa kwanza kumjua Destiny. Usiku wa siku hiyo, waliyokutana kimwili, Desiny alijiapiza moyoni mwake kuwa, Brian ndiye atakuwa mwanaume wa kwanza na wa mwisho kumjua.

Lakini, kufumba na kufumbua ndoto yake hiyo iligeuka na kuwa ndoto ya macho wazi. Maana punde yule malaika wake wa kumtumainia aligeuka na kuwa shetani. Brian alijiingiza kwenye uhusiano wa mapenzi na msichana wa asili yake ya Kizungu aitwaye Trace.

Hilo, lilikuwa pigo kubwa mno kwa Destiny. Baada ya kubaini juu ya mahusiano hayo, kati ya Brian na Trace. Msichana huyo aliumia mno kiasi cha kushindwa kufanya jambo lolote, akawa anashinda tu ndani analia. Baadaye baada ya mama yake kuigundua hali hiyo, ilimbidi kuwa naye karibu na mara kwa mara akawa anazungumza naye akimwelekeza juu ya walimwengu na maumivu yao. Akimuasa pia, kujifunza kuwa thabiti katika maisha yake kwa maana maumivu ya namna hiyo ama zaidi ya hayo atakutana nayo kipindi kwa kipindi katika maisha yake.

Ukweli ni kwamba, halikuwa jambo rahisi kwa Destiny kukubaliana na ukweli huo, hali iliyosababisha tukio hilo likae kichwani na moyoni mwake kwa muda mrefu. Mbali na hivyo, kutokana na tukio hilo, Destiny alijikuta akiwachukia mno vijana wa Kizungu, lakini pia kutokana na namna alivyoumizwa hakuwa na hamu ya

kusomea chuo nchini hapo Marekani. Alitamani kwenda mbali na kumbukumbu zote ambazo zilikuwa zinamkumbusha uhusiano wake na Destiny, ndipo akawasihi wazazi wake wamtafutie chuo nchini China.

Alipokipata chuo hicho, mambo ya Marekani na yanayomhusu Brian angalau akawa ameyaacha nyuma ya mgongo wake.

Destiny ni binti mwenye mchanganyiko wa asili. Asili ya baba yake ni kutoka Afrika ya Magharibi, lakini mama yake ni chotara aliyezaliwa kati ya baba mweusi na mama Mzungu.

Destiny, alibarikiwa uzuri wa sura. Uso wake wa umbo la yai, Mwenyezi Mungu aliupamba kwa macho makubwa mazuri, yaliyozunguka mahala pake kana kwamba mishipa za kuyashikilia zilikuwa zimelegea.

Msichana huyu, alibarikiwa nywele na nyusi nyingi na pua yake ilisimama shadidi juu ya midomo yenye lipsi nene. Rangi ya ngozi yake, ililalia zaidi upande wa mama yake; kwa kumuona ungedhani ni chotara na umbo lake halikuwa jembamba la kumuita mtu mwembamba na halikuwa nene la kumuita mtu mnene. Alikuwa na mwili wa haja ulionogeshwa na kimo chake.

Akiwa chuoni hapo Tsingua, vijana wengi walijitokeza kumuwania binti huyu, lakini wote waliojitokeza aliwatolea nje. Destiny, aliwatolea nje kwasababu tofautitofauti. Hasa wale wenye asili ya Kizungu hakuwahitaji kabisa, lakini wengine aliwatolea nje kwa kuwa hawakuwa moyoni mwake, naye alikuwa amezimika kwa kijana wa Kitanzania aitwaye Biruse.

Kwa kijana huyo, Destiny alikuwa amekufa ameoza na hakujitambua kabisa. Destiny, hakufahamu ni kwanini hasa alimpenda Biruse, kwa namna hiyo aliyokuwa anajihisi moyoni mwake. Lakini, alichokifahamu ni kwamba, kila akimpima Biruse kwenye mizani yake, alimuona kuwa ndiye kijana anayefaa kuziba pengo la Brian. Na imani yake inamweleza pengine akimpata Biruse atakuwa tofauti na Brian. Anaamini kijana huyu kwa muonekano

wake wa upole, ucheshi na ukarimu, basi atampenda kwa dhati na kuulinda moyo wake kiasi cha kumsahaulisha machungu yote ya mapenzi aliyopitia huko nyuma.

Pamoja na kwamba, Biruse alikuwa kwenye mahusiano ya mapenzi ambayo Destiny aliyafahamu, lakini hicho hakukiona kuwa ni kikwazo cha kumzuia yeye kuwa na mtu anayempenda. Na juu ya hilo, msichana huyu aliapa kufanya jambo lolote lile ilimradi aweze kumpata Biruse. Hata kusema kuua mtu, Destiny alikuwa tayari.

Sasa kutokana na urafiki ambao, Destiny alikuwa nao na Fanta, aliweza kupata taarifa kuwa, katika siku ya maandamano iliyokuwa imepangwa na baadhi ya wanafunzi wa chuo chao; maandamano ya kupinga ubaguzi wa rangi, Zinaeda, msichana mwenye asili ya Urusi, mpenziwe Biruse, atabaki kwenye nyumba aliyokuwa anaishi Biruse kwa ajili ya zoezi la kuzima umeme wa mji huo wa Beijing, zoezi ambalo Biruse ndiye aliyeliratibu.

Hapo ndipo, Destiny alipoiona nafasi yake ya dhahabu ya kuweza kutekeleza hatua moja ambayo alikuwa anaiwaza ya kumsaidia yeye kuwa na Biruse. Nayo ilikuwa ni kumpoteza Zinaeda.

Kazi hiyo, kwake haikuwa ngumu sana. Kutokana na mazoea ya kutembelea kwenye nyumba za starehe aliyokuwa nayo, kuna vijana kutoka nchini Nigeria alitokea kujenga nao urafiki, vijana ambao nchini hapo China walikuwa wakijihusisha na matukio ya kihalifu kwa malipo.

Destiny aliwafuata vijana wale watatu waliojiita *The Happy Maker,* wakimaanisha kikundi chao hicho kilikuwa kinatoa furaha kwa watu ambao furaha yao ilishikiliwa na watu wengine na waliwahitaji wao ili kuweza kuirejesha tena furaha yao.

Baada ya kuonana nao, aliwaeleza juu ya mpango wake wa kumpoteza Zinaeda na alikuwa tayari kuwapa kiasi cha pesa wanachokitaka. Walipokubaliana, Destiny alilipa asilimia sabini na tano ya pesa waliyoihitaji na ndipo vijana hao wakaingia kazini.

Kwa kufuata malekezo ya Destiny, vijana hao Chineke Udu,

Uche Obwagedo na Ikena Obemba, walizuka kama mzimu kwenye makazi ya Biruse, kule ambako alimuacha Zinaeda, kwa kutumia ufunguo malaya walifungua mlango na kuingia ndani, wakamteka binti huyo Zinaeda na kutoweka naye, ikiwa ni muda punde tu alipomaliza kuzima umeme wa jiji lile la Beijing!

*****

"Simu yake inaonyesha mara ya mwisho alikuwa anawasiliana na mtu aitwaye Biruse Seyunguson!" Boros Lobos, mshirika wa *KGB,* aliyekuwa nchini hapo China, alikuwa akimpa taarifa Dimitir Roshkeov, baba yake na Zinaeda baada ya kukutana naye kwenye chumba cha hoteli, alipofika jijini Beijing, nchini hapo China.

"Naye huyo Biruse ndiye nani?" Dimitir Roshkeov, aliuliza akiwa amegeuza mgongo wake akitazama nje kupitia kwenye dirisha kubwa lenye vioo, lililopangwa vizuri likiachwa na nafasi katikati ya kutazama nje. Akiutazama uzuri wa jiji hilo hata asiuone kutokana na yale yanayoendelea kichwani mwake.

"Mpenzi wake."

"Mpenzi wake?" Dimitir Roshkeov, aliuliza akitoa macho yake yote kana kwamba hakuhitaji yabaki ndani. Akageuka na kumtazama Boros, kwa macho makali yenye udadisi ndani yake.

Lilikuwa ni jambo gumu kuamini ikiwa bintiye alikuwa na mpenzi. Akiwa katika hali hiyo, yule mshirika wake alimwambia: "Samahani mkuu, huo ndiyo ukweli wenyewe."

"Kwamba Zinaeda ana mpenzi?"

"Ndiyo, huyu kijana. Tumefuatilia kwa ukaribu mkubwa juu ya mawasiliano yake na tumegundua wanawasiliana sana. Lakini, hata mara ya mwisho, ambapo Zinaeda ametoweka alikuwa nyumbani kwa huyo kijana."

Dimitir Roshkeov, alijaribu kujenga utulivu katika hayo yote. Ndipo alipopata utashi wa kusogelea sofa na kukaa. Alipokaa tu, alimwambia Lobos: "Kuna mengine ninayopaswa kufahamu?"

"Tulipochimba zaidi, tumegundua huyu kijana Biruse, ndiye

ameratibu maandamano hapo chuoni kwao. Lakini, jambo linalovutia zaidi ni kwamba; baba yake alikuwa ni miongoni mwa wanausalama tishio Afrika. Na alipata mafunzo kutoka kwetu, lakini sasa hayupo tena hai."

Dimitir Roshkeov alizidi kuchanganywa na taarifa hizo.

*Mwanaye anampenzi! Na mpenzi wake ndiye ameratibu maandamano yaliyopelekea maafa makubwa katika chuo cha Tsingua! Na huyo mpenzi wake ni mtoto wa mwanausalama mwenye jina kubwa katika medani hizo, pande za Afrika, Othuman Seyunguson!*

Mawazo tele yalianza kutiririka akilini mwake.

"Jina la Seyunguson siyo geni!" Mwishowe Dimitir alimweleza Lobos, akisema kwa sauti iliyopoa.

Na Lobos akiwa hajajibu neno lolote, Dimitir aliongeza; "ninachojiuliza ni kwamba, huyu kijana mbona anajulikana mahali aliposhikiliwa, lakini hakuna taarifa juu ya binti yangu? Hakuna tukio la kijasusi kweli hapa katikati?"

Lobos alilazimisha kumeza mate. Siyo siri taarifa za Zinaeda, zinachanganya. Kwa kutumia intelejensia yao, wamejaribu kutafura taarifa zake lakini wameshindwa kabisa.

"Inabidi mbinu zitumike huyu kijana atoke mahabusu," Dimitir alisema taratibu, "yeye ndiye atatuongoza kumpata Zinaeda."

Lobs alipandisha kichwa chake na kushusha chini akimaanisha alikuwa akikubaliana na mawazo hayo.

"Lakini…*heee!* Kukiwa kuna jambo lolote baya limempata binti yangu; huyu kijana korodani zake nitazikata na kuzikaanga akiwa anaona!" Dimitir Roshkeov, alisema kwa ghadhabu kali.

# 4

Mambo mawili yalikuwa yanazunguka ndani ya kichwa cha Biruse akiwa ndani ya chumba cha mahabusu. Jambo la kwanza lilikuwa; alijiuliza; nini hatma yake baada ya kukamatwa kutokana na tukio lile aliloratibu?

Biruse baada ya kukamatwa, alinyang'anywa mawasiliano yake yote, akavuliwa nguo zote na kuwekwa kwenye chumba maalumu peke yake akisubiri mahojiano ya kina.

Akiwa ndani ya chumba hicho anawaza juu ya walinzi waliowaua kwa sumu yeye pamoja na Mohammadoe, na hapo ndipo anazidi kukata tamaa na anaona wazi hakuna uwezekano wa kutoka zaidi ya kuozea jela.

Sambamba na hivyo, Biruse anawaza kwamba, kesi hiyo itakapokwenda mahakamani, mbali na kukabiliwa na shitaka la kuhusika kwenye vifo vya walinzi hao, shitaka lingine analoliwaza kichwani ni juu ya kadhia ambazo zimesababishwa na kukatwa kwa umeme kwa dakika hizo takribani kumi.

Taifa hili la China ni miongoni mwa mataifa ambayo yameendelea. Matumizi ya umeme ni makubwa kwa sababu; sehemu kubwa ya uzalishaji wake kupitia nyanja mbalimbali unategemea umeme. Kwahiyo, kitendo cha umeme kukatika kwa dakika moja, husababisha kadhia kubwa sana. Vipi kwa kipindi chote hicho ambacho umeme ulikatika. Dakika kumi nzima. Biruse anawaza mengi na anajionea shida kwa hakika.

Jambo la pili, linalomsumbua akilini Biruse, ni juu ya mpenzi wake Zinaeda. Anajiuliza; msichana huyu baada ya kuuzima umeme wa jiji lile la Beijing kwa kutumia maelekezo aliyompatia,

nini kimempata? Naye aliingia mikononi mwa polisi? Au polisi hawakufanikiwa *kum-trace* na kufahamu mahali alipokuwa?

Na hilo linawezekanaje *wasim-trace* na kufahamu mahala alipokuwa. Interejensia ya taifa hili si ya kuungaunga! Na jambo ambalo Biruse anaona ni wazi alilikosea, ni kutokufikiria kuweka tahadhari kuwa, ikiwa mambo yatakwenda ndivyo sivyo, nje ya mipango waliyojiwekea, Zinaeda afanye nini!

Kwakweli mambo ni mengi kichwani kwa njemba huyu, kiasi mpaka anakihisi kichwa kikizunguka *'ziiiiiiii'* utasema kulikuwa na selemala anakwangua mbao kichwani kwake kwa msasa!

Basi majuto nayo ni mjukuu; na wengine husema; 'ninge…' ama 'nisinge…' huja zimechelewa mno kwenye maisha. Akiwa katika utulivu huo, akitafakari kwa dhati, Biruse anajikuta akijuta kumshirikisha Zinaeda kwenye mpango huo.

Ni mpango ambao, anafahamu wazi kuwa, bila yeye, Zinaeda asingekubali kushiriki. Na anakumbuka awali alipomweleza juu ya jambo hilo alilomhitaji alifanye, mpenzi wake huyo alimkatalia na kumweleza wazi kuwa hawezi, lakini baada ya kumsihi akimwelekeza cha kufanya, hatimaye Zinaeda alikubaliana naye. Hata hivyo, Biruse alitambua kwamba msichana huyo alikubaliana naye kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo dhidi yake na si vinginevyo.

*Kwanini lakini nilimshirikisha?* Alijikuta akizungumza peke yake utasema mwendawazimu!

Lakini ndiyo hivyo tena; 'laiti kama…ninge – lijua… ama nisinge…' zimefika, anazijadili akilini mwake, lakini zimefika zimechelewa mno. Wakati huu hakuna anachoweza kukibadili. Mambo yanakwenda kama ambavyo aliyapanga yaende!

*****

Katika wakati huo, ambao Biruse alikuwa akiwaza ya kwake kichwani, baba yake Zinaeda, Dimitir Roshkeov, alifika katika mahabusu aliyokuwa ameshikiliwa kijana huyo na kuzungumza

na wakuu wa usalama ili aweze kupata nafasi ya kuzungumza na kijana huyo juu ya binti yake Zinaeda.

Kutokana na nafasi yake katika medani za usalama, na uhusiano uliokuwepo wakati huo, kati ya nchi hizi mbili, China na Urusi, Dimitir Roshkeov, aliweza kukubaliwa juu ya jambo hilo, ambapo Biruse aliletwa mbele yake kwenye chumba maalumu ili waweze kuzungumza.

Wakiwa kwenye mazungumzo hayo, ndipo Biruse anafahamu kuwa Zinaeda alikuwa ametoweka na alitoweshwa na gari ambalo linatiliwa mashaka kuwa si la jeshi la polisi wala mawakala wa usalama hilo.

Habari hizo zilikuwa za kushitua mno kwa Biruse. Wasiwasi wake ulikuwa ni kwamba, huenda baada ya tukio hilo, Zinaeda naye alidakwa na polisi. Sasa, hizi habari za kutoweka kwake katika mazingira haya ambayo anaelezwa zilikuwa za kushitua mno.

"Kwakweli mzee, mimi sifahamu lolote juu ya habari hizi!"

"Kijana… mimi siyo babu yako tusileteane utani, nataka kufahamu ni wapi alipo binti yangu. Hilo basi!" Dimitir Roshkeov, alizungumza kwa ukali kiasi cha kuipiga meza kwa nguvu.

Biruse uso wake ukiwa umetaharuki aliendelea kusisitiza kuwa, hafahamu ni wapi binti huyo alikuwa, zaidi akiapa mbele za Muumba wake kuwa, anachokisema kilikuwa ni ukweli mtupu.

Kutokana na uzoefu aliokuwa nao, Dimitir Roshkeov, wa kuzungumza na wahalifu ama kufanya mahojiano na watu mbalimbali, kuna namna alikuwa anauona ukweli ndani ya macho ya kijana huyu. Kuwa yale aliyokuwa anamweleza yalikuwa na ukweli ndani yake. Sasa, swali likabaki pale pale, kama hayo anayoyasema yana ukweli, ni nini kimetokea kwa binti yake?

Akipima ikiwa alikuwa na maadui ambao wangeweza kuisonga familia yake - haoni, na hata kama kulikuwa na maadui, hao maadui waliwezaje kuunganisha nukta hata wamtwae binti yake katika wakati huo ambao maandamano ya wanafunzi yalifanyika! Bado kila akipima mizani yake anaona ni ngumu kuacha kulihusisha

tukio hilo la kutoweka kwa binti yake na tukio la kuandamana kwa wanafunzi.

"Mzee naomba unisikilize vizuri…" Hatimaye Biruse alisema taratibu akimtazama Dimitir Roshkeov, usoni.

Dimitir Roshkeov, alimtupia macho akiongeza umakini wa kumtazama Biruse ili ikiwa kuna jambo anajaribu kuficha aweze kulibaini.

"Ndani ya chumba changu, ukiingia tu, kwenye ukuta unaoutazama mbele, kuna picha ya mama yangu mzazi ambayo imetengenezwa kwa kibao cha mbao. Shusha hiyo picha na ikague, kuna kamera ndogo ya usalama utaibaini. Hiyo kamera inauwezo wa kurekodi matukio na kuyahifadhi kwenye kadi ambayo ipo pembeni yake.

"Kama tukio la kuchukuliwa kwa Zinaeda lilitokea mule ndani. Utaliona kwenye kamera hiyo. Naapa mbele za Mwenyezi Mungu nilimuacha Zinaeda ndani na kama hiyo kamera haijagundulika itakuonyesha ukweli wote."

Hizo zilikuwa ni taarifa za kusaidia. Basi, walipomaliza maongozi, Biruse alirudishwa ndani ya chumba cha mahabusu na Dimitir Roshkeov, akiongozana na mshirikia wake Boros Lobos, walitoka ndani ya mahabusu yale kwa ajili ya kwenda mahala ambapo Biruse alikuwa amepanga nyumba kwa ajili ya kukagua kuona ikiwa wataipata hiyo kamera ambayo anaizungumzia kijana huyo.

*****

Nusu saa baadaye, Dimitir Roshkeov, akiongozana na Boros Lobos, waliweza kufika kwenye nyumba ile ambayo alikuwa amepanga Biruse. Walipoufikia mlango, walikuwa ni wenye tahadhari kubwa.

Hata hivyo, kwa sababu za kiusalama, iliwabidi wachunguze kwa makini ikiwa kuna namna yoyote ambayo mlango ama kitasa kilivunjwa au kufunguliwa kwa nguvu lakini hawakuweza kubaini lolote lile.

Kwa kutumia funguo yao yenye uwezo wa kufungua vitasa mbalimbali walifungua na kuingia ndani.

Baada ya kufika ndani, waliona kila kitu kikiwa sawa. Hakukuwa na dalili ya purukushani yoyote kutendeka humo ndani, kitendo kilichowaeleza ikiwa Zinaeda alichukuliwa humo ndani, basi alichukuliwa katika namna isiyokuwa na purukushani. Alitii amri pasipo shuruti.

Hata hivyo, Dimitir Roshkeov, akiangaza ndani ya chumba hicho, kwenye kochi dogo lililokuwa karibu na friji aliweza kuona kibanio cha nywele alichokifahamu kuwa kilikuwa ni cha binti yake. Alikifahamu kibanio hicho kutokana na mazoea aliyokuwa nayo ya kuwasiliana naye kwa njia ya video na binti yake kila mara, na mara kadhaa alimuona akiwa amekivaa kibanio hicho.

Dimitir Roshkeov, alipiga hatua, akaenda moja kwa moja kulipokuwa na kibanio hicho kisha akakiokota na kukinusa. Baada ya kufanya kitendo hicho, alijikuta akilazimisha mate kupita kooni mwake. Pasipo kutarajia, alihisi uchungu ukimpiga moyoni na alijiapiza moyoni mwake, kuwa wote ambao wanahusika kwa namna yoyote au nyingine na kumshikiria binti yake watakiona cha moto. Na heri yao ampate akiwa hai, lakini vinginevyo, kila atakayehusika kwenye ubaya atakaotendewa binti yake, basi ukoo wake utalipa kwa maumivu makali mno!

"Picha aliyoelekeza siyo hiyo kweli?" Boros Lobos, alimuuliza Dimitir Roshkeov.

Akawa amemzindua kutoka kwanye mawazo yale ambayo yaliiteka akili yake.

"Huenda ndiyo hiyo," Dimitir Roshkeov alijibu, "hebu itoe."

Boros aliisogelea ile picha na kuitungua, kisha akaikagua. Bahati ya mtende ilikuwa kwao. Waliweza kuona kamera ndogo ikiwa imenasa kwenye ubao ule kama ambavyo walielekezwa na Biruse. Waliitoa kamera ile na kuchomoa *memory card* kisha wakakaa kwenye moja ya masofa na kuipachika *memory card* ile kwenye kifaa maalumu kinachosoma taarifa kwenye komputa na kuanza kuikagua.

Wakizidi kuikagua, mwishowe walipata kile walichokuwa

wanakitafuta kwa hamu sana. Walikutana na *video* ambayo ilionyesha vijana watatu waliovalia tracksuit pamoja na kofia za soksi kichwani, zilizoficha nyuso zao, pamoja na viatu vigumu mguuni wakiingia ndani ya chumba hicho huku wakiwa wameshika silaha mkononi.

Wakati watu hao wanaingia, Zinaeda anaonekana akiwa amekaa kwenye moja ya masofa ndani ya chumba hicho huku akiwa *busy* na *laptop* iliyokuwa mbele yake na masikioni alikuwa amevaa *headphones.* Na bintu huyo, alikuja kushituka kuwa yupo kwenye hatari, wale watu wakiwa tayari wamekwishaingia ndani ya chumba hicho.

Baada ya kuingia, ile *video* ilionyesha wale watu walimnyooshea silaha zao na kumtaka atulie. Zinaeda anaonekana akiwa kwenye taharuki isiyosemekana. Hicho ni kitendo ambacho hakukitarajia kabisa. Anaonekana akiwa ametoa macho na kuhema kwake kukiwa kumebadilika. Hofu ilimtanda na akawa ananyoosha mikono akiwasihi watu hao wasimzuru.

Mmoja kati ya watu wale watatu, waliokuwa wanaunda kikundi cha *The Happy Maker,* aitwaye Ikena Obemba, alisogea mpaka pale kwenye sofa alipokuwa Zinaeda, kisha akatoa kichupa kidogo cha plastiki mfukoni mwake na kumpulizia msichana yule. Dakika si nyingi, Zinaeda alipinduka na kugaragara pale sofani pasipo ubishi wowote ule; njemba huyo mwenye mbavu nene, aliyejazia kutokana na mazoea ya kunyanyua vyuma vizito, alimkusanya pale sofani na kumuweka begani.

Mwenzake aitwaye Uche Obwagedo, naye alisogea na kuichukua *laptop,* ambayo Zinaeda alikuwa nayo pale sofani, kisha wakatoka. Video ile iliishia kuonyesha waliporudishia mlango baada ya kutoka ndani ya chumba hicho.

Baada ya kumaliza kutazama video hiyo, Dimitir Roshkeov, alijikuta akishusha pumzi za haja. Kisha aligunjama sofani pale, tafakuli mbili tatu zikipita akilini mwake.

Kwa muonekano wa wale watu, pamoja na kwamba walikuwa

wamezificha nyuso zao, si watu wenye asili ya asia. Mbavu zao zilikuwa nene na walikuwa ni warefu kulinganisha na watu ama askari wengi wa Kichina.

Lakini, mbali na hivyo, kama wangekuwa ni askari polisi, Dimitir Roshkeov anajiuliza, walikuwa na sababu gani za kuficha nyuso zao?

"Hapa lazima kuna kitu hapa ambacho si cha kawaida…" Dimitir Roshkeov alijikuta akizungumza peke yake.

"Mzee unasemaje?" Boros Lobos, alimuuliza. Hakuwa amesikia vyema yale ambayo aliyazungumza.

Dimitir Roshkeov, aliinua mgongo wake kutoka sofani pale alipokuwa amejilaza na kukaa vyema kisha akamtazama Boros.

"Najaribu kutafakari ni jambo gani linaendelea, lakini nashindwa kupata majibu kabisa."

"Ama hawa vijana kuna namna walijiingiza kwenye magenge ya kihalifu?"

"Magenge ya kihalifu?" Dimitir Roshkeov, aliuliza kwa mshangao, tafakuri zaidi zikizidi kupita akilini mwake. Kiasi kwamba, ndita kadhaa zilijikusanya usoni mwake. Akaongeza kuuliza swali; "Uhalifu huo ndiyo upelekee mmoja wao atekwe?"

"Hii video ukiitazama mzee, ni wazi unabaini kuna mtu yupo nyuma ya tukio hili. Ama kwa kulipa kisasi au vinginevyo. Hawa vijana, kitendo cha kumpulizia Zinaeda dawa ya kumpoteza fahamu ni ishara tosha kuwa hakuna walichofuata hapa zaidi ya binti huyo, na pengine wamechukua *laptop* yake kwa kulazimika tu. Kwa sababu wamekuta yupo nayo na kuicha walihisi litakuwa jambo la hatari kwao.

Dimitir Roshkeov, alikubaliana kabisa na mawazo hayo ya Boros Lobos. Lakini kitendawili kikabaki; ni nani yupo nyuma ya tukio hilo? Jibu lilikuwa gumu kupatikana. Hata hivyo, baada ya kuona swali hilo linawaelemea, wanausalama hao, waliamua kurudi kule mahabusu kwa ajili ya kuzungumza na Biruse, kuona ikiwa watapata dondoo zitakazowasaidia kumtoa Zinaeda.

*****

*"Mh!"* Biruse aliguna baada ya kuitazama ile video mwanzo mwisho. Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, walikuwa wakimtazama kwa makini machoni. Kijana huyo alizungusha kichwa ishara ya kukataa jambo kisha akashusha pumzi ndefu na kukaa vyema pale kwenye kiti alipokuwa amekaa.

"Ni kina nani hawa?" Dimitir Roshkeov, alimuuliza kwa sauti ya upole akiwa amemkazia macho.

"Kwakweli sifahamu?"

"Kijana usitake mambo yawe magumu! Nini kinaendelea? Kuna watu gani pengine una ugomvi nao ama kuna visasi kati yenu vinaendelea?"

Biruse alizungusha kichwa kwa ishara ya kukataa. "Hakuna mzee." Kisha alisema kwa uhakika.

"Sasa nini kinaendelea?" Dimitir Roshkeov, alizungumza kwa hali ya ukali. Mhimili wake wa ustahimilivu ulikuwa umekwisha mtoka na pasipo kutegemea alikuwa tayari amekwisha mvaa Biruse kwa kunyoosha mikono yake na kumkunja.

Boros Lobos, ilimbidi afanye jitihada za makusudi za kuitoa mikono ya mwanausalama huyo wa *KGB,* shingoni mwa Biruse. Haikuwa kazi nyepesi, lakini hatimaye Boros alifanikiwa.

Hata baada ya kuachanishwa, Dimitir Roshkeov, alibaki akitetemeka kwa hasira. Uchungu dhidi ya mwanaye ulikuwa ukimpiga moyoni mwake kiasi kilichomfanya apoteze kabisa mhimili wake. Kwa upande wa Biruse, alipoachiwa kwa kuachanishwa, alijiegemeza kwenye kiti kile alichokuwa amekikalia na kushusha pumzi ndefu kwa mara nyingine. Naye akilini mwake anajiuliza: *nini kimetokea? Kwanini Zinaeda atekwe?*

Suala la kutekwa kwa Zinaeda, halimuingii kabisa akilini. Biruse anachofahamu hakukuwa na mtu yeyote ama watu ambao anatofauti nao hata waseme wanalipa kisasi. Lakini, ni hivyo hivyo kwa Zinaeda.

Maisha ya binti huyo aliyafahamu kwa kila nukta. Ni binti mpole aliyejali mambo yake tu. Hana mambo mengi wala hana vikundi vya wasichana wenzake ama wavulana, hata atilie mashaka kuwa kupitia vikundi hivyo ndipo utekaji umetokea. Akiwa jijini hapo Beijing, Zinaeda, ni yeye na masomo, masomo na yeye. Akisema atoke, kama si kutoka pamoja na Biruse basi ni baadhi ya rafiki zake wachache anaowafahamu. Lakini, mara nyingi pia yupo nyumbani kwake.Kwahiyo, kutokana na uhalisia huo maswali ni mengi kichwani mwa Biruse.

Kila mmoja akiwa kimya, mara Biruse alipata wazo. Wazo hilo alipolichekecha akilini mwake, aliliona kuwa ni wazo jema ambalo linaweza likatoa mwanga mwingine katika zoezi hilo la kumsaka Zinaeda.

"Wazee wangu," aliita taratibu.

Wale watu wawili mbele yake walimrushia macho na kumtazama.

"Sema," Boros Lobos, alimshinikiza.

"Tujaribu jambo moja pengine linaweza kusaidia."

"Jambo gani?"

"Pale nyumbani nilipopanga, kwenye *apartment* ya tatu, kuna kamera ambazo zinamulika katika eneo lote la nje, naomba mjaribu kwenda kuzungumza na mwenye *apartment* ile, ili awape video za siku ya tukio, huenda kuna jambo tutabaini ambalo litatusaidia kumpata Zinaeda!"

Dimitir Roshkeov na Boros Lobos walitazamana. Macho yao ni kama yalizungumza jambo ambalo walishindwa kulizungumza kwa mdomo. Kisha waliyapepesa macho hayo na kila mmoja akayarudisha kwa Biruse. Ukweli ni kwamba, pamoja na kubobea kwao kwenye masuala ya kiusalama, wazo lile hawakulifikiria kabisa. Hata hivyo, wazo hilo; walilipokea kwa mikono miwili na waliafikiriana haraka lifanyiwe kazi. Ni kweli, ikiwa video zinazoenyesha eneo la nje zikipatikana; huenda zitasaidia juu ya upatikanaji wa Zinaeda!

# 5

*Dar es Salaam, Tanzania.*

Huku hayo yakiendelea huko China; nchini Tanzania, kwenye makao makuu ya kitengo cha usalama, ndani ya chumba cha ofisi ya mkurugenzi wa idara ya usalama, Kamishina Marwa Warioba; walikutana wakuu wa idara hiyo, kwa ajili ya mazungumzo mazito.

Wakuu hao waliokutana, alikuwa ni mkurugenzi mwenyewe, Kamishina Marwa Warioba, kamishina msaidizi, Slyvester Jenge na mkuu wa idara ya mawasiliano ya idara hiyo, Kepteni Chimbusu Mwambukusi.

Mazungumzo ya wazito hawa wa idara hiyo nyeti inayotazama usalama kwa mapana yake, sasa yamechukua saa moja na zaidi na bado ni ngumu kuupata muafaka wa kile kilichowakutanisha.

Mwishowe, Kepteni Slyvester Jenge alishauri, “inabidi mmoja kati yetu akwee pipa na kwenda huko China.”

“Halafu…?” Kamishina Marwa Warioba alihoji.

“Akazungumze na kitengo cha usalama kuona ikiwa tutamnusuru.”

“Hilo ni wazo zuri,” Kepteni Chimbusu Mwambukusi aliunga mkono mawazo yale ya kamishina msaidizi, Jenge.

Ukweli ni kwamba, suala la Biruse, kijana wa Kitanzania, kuratibu maandamano katika Chuo Kikuu cha Tsingua, nchini China, yaliyosababisha vifo vya takribani watu sita, jambo lililopelekea kijana huyo pamoja na wenzake kadhaa kushirikiliwa na jeshi la polisi la nchi hiyo, lilikuwa ni jambo gumu kulipatia ufumbuzi.

Jambo hilo lilikuwa gumu haswa kutokana na sababu kuu mbili; sababu ya kwanza; Biruse mbali na kuwa mtoto wa mwanausalama mwenye heshima kubwa kwenye medani za usalama za taifa hili, marehemu Othuman Seyunguson, alikuwa ni nyota njema ambayo inatazamwa katika medani hizo.

Kitengo cha usalama, kilikuwa kikimuandaa kijana huyu kufuata nyayo za baba yake na kwa bidii aliyokuwa nayo, walifahamu wazi, Biruse atafanya mambo makubwa kuliko hata yale ambayo alifanya baba yake mzazi.

Toka akiwa kijana mdogo, kwa heshima ya baba yake, kitengo hicho cha Usalama, kiliamua kumchukua na kumuweka kwenye mpango maalumu wa muda mrefu, uliohusisha kuandaa vijana ambao taifa lilikuwa likiwatazamia kwa kipindi kijacho watakaokaa kwenye nafasi nyeti za kitengo cha usalama, wakiwa wanakifahamu vyema kitengo hicho na wakiwa wameshiba mafunzo hasa.

Biruse kila mara, mbali na kusomeshwa katika shule mbalimbali na kubwa duniani, amekuwa akihudhuria kila mara mafunzo yanayohusu masuala ya kiusalama na kutokana na maadili ya mafunzo hayo aliyokuwa anachukua, ulikuwa ni mwiko kutenda kosa lolote la jinai ama kujihusisha kwenye matukio ambayo yangemfanya aanikwe kwenye vyombo vya habari na taarifa zake kuanza kufuatiliwa.

Lakini sasa kijana huyo alikuwa amekiuka maadili hayo!

Jambo la pili, ilikuwa ni namna gani kitengo cha usalama kingeweza kumuondoa mikononi mwa jeshi la China! Biruse kwa hayo aliyoyafanya pamoja na wenzake, anahesabika kuwa mhalifu kama wahalifu wengine.

Pamoja na kwamba, yeye na wenzake hawakupendezwa na kitendo ambacho mwalimu Bolin Chaoxiang, alikifanya cha kumtemea mate Fanta Seydoe, kwa madai kuwa binti huyo alimkanyaga mbwa wake, wakuu hao wa idara ya usalama ya taifa, mtazamo wao ulikuwa, pamoja na kwamba pia, Chaoxiang alimdhalilisha kwa kumtukana matusi na kumuita sokwe mtu Fanta, bado vijana

hawa walikuwa wananafasi ya kuitafuta haki yao kwa njia ya amani hata kama yangekuwa ni hayo maandamano waliyoyahitaji, basi maandamano hayo yalipaswa kufanyika katika namna ya amani!

“Basi tusimamie hapo,” Kamishina Marwa Warioba, alisema na kuongeza, “mwenzetu mmoja afike China.”

“Na sasa, vipi kuhusu hatima ya huyu kijana? Ni kama ameanza kukengeuka sasa?” Kepteni Chimbusu Mwambukusi alihoji.

Kamishina Marwa Warioba alilazimisha mate kupita kooni mwake, kisha akarudisha mgongo na kuuegemeza kwenye kiti kile alichokuwa amekalia.

“Hawa vijana wa miaka ya siku hizi wanashida sana. Ni ngumu kukaa kwenye misingi ya malezi wanayolelewa. Mara zote wakiwa na jambo ndani yao wanalohisi ni muhimu, basi wanapenda kuonekana mbele. Vifua wanapandisha juu na kujiona miamba. Kazi kwelikweli!

“Ni tofauti na nyakati zetu. Unapoaminiwa na kuwekwa kwenye kitengo nyeti kama hiki wakati mwingine hata wale watu wako wa karibu mno wanakuwa hawafahamu. Mimi kuna makamanda ninawafahamu wapo zaidi ya miaka kumi kwenye kitengo hiki lakini unakuta hata wake zao tu hawafahamu kama ni usalama.”

Baada ya kumaliza kuzungumza maneno hayo, Kamishina Marwa Wariaoba, alishauri, “itabidi huyu kijana tukifanikiwa kumtoa huko China, tumpe misheni aende Kongo huko akapambane na vikundi vya waasi vya 3. Pengine akikoswa koswa na risasi huko akili yake itakaa sawa. Ni kana kwamba utoto unamsumbua.”

Viongozi wale wa Usalama walijikuta wakicheka kwa pamoja. Kashese za kwenye uwanja wa kivita hasa zinazohusu kitengo nyeti cha usalama wanazifahamu. Na hilo ndilo lililowafanya wacheke!

Hata hivyo, mwisho wa mazungumzo, walikubaliana kuwa; mkuu wa idara ya mawasiliano ya kitengo hicho, Kepteni Chimbusu Mwambukusi, atasafiri kwenda China, kwa ajili ya kufuatilia suala la kumtoa Biruse, kwa kufanya mazungumzo na kitengo cha usalama la China.

*****

Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, walirudi kwenye mtaa ambao alikuwa amepanga Biruse na kuonana na jirani ambaye alikuwa amefunga kamera katika eneo la nje la eneo lile.

Baada ya salamu na kujuliana hali na jirani huyo, ambaye alikuwa ni mwanamama mwenye asili ya Korea Kusini aitwaye Xao Chung, wawili hao walijitambulisha kuwa ni wanausalama na wakamueleza juu ya kile kilichotukia katika makazi hayo na nia yao iliyowasukuma kufika mahala hapo.

Mwanamama Xao Chung, alishangazwa mno na habari hizo. Pamoja na kwamba alisikia habari juu ya maandamano yaliyofanyika kwenye Chuo Kikuu cha Tsingua, taarifa juu ya kutekwa kwa Zinaeda hakuwa amezinasa kabisa kwenye masikio yake. Lakini pia, mwanamama huyu hakuwa amekagua kamera zake kwa takribani siku tatu sasa, kutokana na kuwa, hakukuwa na kiashilia chochote cha uvunjifu wa amani ama hali ambayo ilimsukuma kwenda kukagua kamera zake.

Zaidi ya hayo yote, taarifa hizo zilimsikitisha mno. Xao alikuwa anamfahamu Zinaeda. Mara kwa mara alikuwa anamuona akiingia ama kutoka na Biruse katika makazi yale ambayo Biruse alikuwa anaishi.

Kusikia kuwa, binti huyo ametekwa na watu wasiofahamika na hali ya usalama wake ni mashaka matupu, alijikuta akiingiwa na ubaridi mkuu moyoni mwake.

“Mbona si kawaida kwa matukio ya namna hii hapa Beijing?” Alisema mwanamama Xao kana kwamba alikuwa anazungumza mwenyewe. “Nimeishi kwa miaka mingi katika jiji hili lakini matukio ya namna hii ni nadra kukutana nayo!”

“Aah! Ndiyo hivyo tena. Tutasemaje na tukio ndiyo limetukia.”

Mwanamama Xao ambaye umri wake ulikuwa unaelekea katikati ya miaka hamsini, alishusha pumzi fupi, akikitwika kiuno chake

uzito wa mikono yake.

"Tunaomba tafadhali uturuhusu tuweze kukagua kamera zako," Dimitir Roshkeov alimsihi.

Kutokana na uzito wa suala lenyewe, mwanamama Xao, aliyekuwa anaishi na wanaye wawili hakuweza kuwa na hiyana hata kuwakatalia. Aliwakaribisha ndani na kuwaruhusu kufanya kile walichokusudia kufanya.

Aliwapa laptop yake ambayo alikuwa ameiunganisha kwenye kamera zile, nao wakaanza kukagua.

Walipozifikia picha zilizorekodiwa, siku na muda ambao tukio la kutekwa nyara la Zinaeda lilipotokea, kuna kitu walibaini ambacho kilivuta umakini wao. Lilikuwa ni gari dogo ambalo liliondoka katika maegesho ya majengo yale punde tu baada ya gari walilokuja nalo wahalifu wale kuondoka.

Wakizivuta karibu zaidi picha zile, walibaini kuwa kwenye gari lile kulikuwa na msichana aliyevalia kofia nyeusi na fulana nyeupe. Lakini, kwa namna alivyokuwa ameivaa kofia ile kiasi cha kumfunika paji la uso na macho, lilikuwa ni jambo gumu kumbaini.

Hata hivyo, kilichowavuta zaidi kwa mwanamke huyo ni kwamba, namna alivyokuwa ameegesha gari lake ilikuwa ni kana kwamba alikuwa anafuatilia kila kilichokuwa kinaendelea mahali pale na baada ya kujihakikishia kuwa kile alichokuwa analenga kitokea kimekwisha tokea, mwanamke huyo aliliondosha gari lake akilifuata nyuma lile gari ambalo Zinaeda, aliingizwa.

Picha hiyo, pamoja na kwamba ilikuwa haielezi zaidi juu ya huyo mwanamke aliyevaa kofia nyeusi alikuwa ni nani au mambo ambayo yangerahisisha zaidi kuwabaini wahalifu, lakini kwa Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, ilikuwa na umuhimu mkubwa.

Baada ya kumaliza kufanya ukaguzi wao, wawili hao walimshukuru mwanamama Xao na waliagana naye, wakatoka katika maeneo hayo.

*****

Biruse aliitazama video hiyo zaidi ya mara tano. Tena aliitazama kwa umakini wake wote akiirudia na kuirudia. Pasipo kuzungumza neno lolote, wala kutoa macho yake kwenye laptop ya Dimitir Roshkeov, kijana huyo alirudia tena kuitazama video hiyo tani yake.

"Vipi?" Dimitir Roshkeov alimuuliza, "kuna kitu unabaini?"

Biruse alishusha pumzi fupi. Wale wanaume wawili mbele yake walimkazia macho. Na kwa namna walivyoyakaza macho yao, ilikuwa ni ishara tosha kuwa, wanawasiwasi Biruse kuna jambo amebaini nao walihitaji kusikia hicho alichokibaini.

"Hii gari hii…" hatimaye alisema. "Kuna mahala nimeiona lakini kila nikijaribu kuvuta taswira ni mahala gani nashindwa kukumbuka vyema."

"Hebu kumbuka," Boros Lobos, alimwambia.

"Nimejaribu sana, lakini inaniwia vigumu kukumbuka."

Ukimya mfupi ulitanda. Biruse aliicheza kwa mara nyingine video ile. Kwa hakika akili yake ilikuwa inamweleza kuwa gari hiyo anaifahamu. Na si mara moja wala mara mbili ameiona tena akili yake inamweleza kuwa gari hiyo inamilikiwa na kati ya watu anaowafahamu. Lakini, taswira juu ya nani anaimiliki gari hiyo inakataa kata kata kumfika kichwani mwake.

"Samahani…" alisema taratibu. Dimitir Roshkeov na Boros Lobos walimrushia macho haraka.

"Haiwezekani kufanyike mpango nitoke mahabusu, tuungane pamoja katika kulifuatilia jambo hili? Ninauhakika nikiwatembelea watu wote ninaowafahamu kuna namna nitapata mwanga. Nina uhakika kuna mtu ninayemfahamu anaimiliki hii gari na tukiipata unaweza kuwa mwanga wa kumpata Zinaeda."

"Wewe kutoka huwezi," Dimitir Roshkeov, alizungumza kwa sauti yenye ukali ndani yake. "Kumbuka wewe ni mhalifu unayekabiliwa na kesi ya mauaji. Jambo la kukusaidia kabla sijakunyonga kwa mikono yangu mwenyewe ni wewe kukumbuka juu ya nani anamiliki hiyo gari!" Dimitir Roshkeov, alizungumza kwa ukali

akiwa amemkazia macho Biruse.

Lakini, bado lilikuwa jambo gumu kwa kijana huyo kukumbuka. Kwahiyo, baada ya kuona kijana huyo, bado anashindwa kukumbuka; waliamua kumpa nafasi kwa mihadi kwamba watarejea muda ujao.

"Tutarudi baadaye, uwe na majibu yote."

Wawili hao Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, waliinuka na kuwataka askari polisi wamrudishe Biruse mahabusu.

*****

Akiwa mahabusu, kwenye kona moja ya ukuta Biruse alizama kwenye tafakari ya dhati, akitafakari juu wapi aliiona gari ile. Kijana huyu kwa namna alivyokuwa anajaribu kuzivuta kumbukumbuku zake, mpaka uso wake ulikunjamana kwa kutengeneza ndita.

"Ni nani mwenye hii gari?" Alijiuliza.

Ni kweli akili yake inamweleza gari hiyo ipo miongoni mwa gari wanazomiliki rafiki zake; lakini mbona inakuwa ngumu kumkumbuka rafiki huyo. Kutokana na kutafakari sana, kuna upande wa akili yake ulimweleza pengine mmiliki wa hiyo gari hakuwa mtu wa karibu sana, maana laiti kama angekuwa mtu wa karibu, basi ingekuwa rahisi kwake kukumbuka. Ama pengine anaichanganya gari hiyo na gari nyingine ambazo anazifahamu za watu wake wa karibu.

Wakati ambao Biruse akiyajadili hayo yote akilini mwake, kuna mawazo mengine yalianza kutiririka: Kama ikiwa gari hiyo inamilikiwa na mtu anayemfahamu; Ni sababu ipi hasa iliyomfanya huyo mtu kumteka Zinaeda. Shida ni Zinaeda au yeye? Na kama shinda ni yeye, amefanya nini hasa kilichomchukiza huyo mtekaji mpaka kufikia maamuzi magumu ya namna hiyo? Na ikiwa shida ni yeye, kama ambavyo mawazo yake yalivyokuwa yanajaribu kudodosa, mbona hakutekwa yeye, atekwe Zinaeda? Na ikiwa basi shida si Zinaeda, mwanadada huyo mpole na mkarimu alikuwa ametenda jambo gani la kumkwaza mtu mpaka afikie hatua hiyo ya kumteka?"

Ukweli ni kwamba, maswali yalikuwa ni mengi mno yaliyokuwa yanamiminika akilini mwa Biruse.

Jambo lenye kusikitisha zaidi, maswali hayo hayakuwa na majibu. Biruse, akiwa kwenye kona ya ukuta ndani ya mahabusu alijikunyata na kufutika kichwa chake ndani ya magoti!

Kutokana na hayo aliyokuwa anayawaza, alijikuta mwili wake ukimsisimka wakati shauku yake ya ndani inawaka, akitamani ikiwa kungekuwa na uwezekano atolewe ndani ya mahabusu hayo ili aingie mwenyewe mtaani kumsaka mpenzi wake Zinaeda.

Kwa kipande hicho cha video alichokiona, Biruse ana uhakika isingemchukua muda kufahamu ni nani alikuwa anamshikilia Zinaeda. Lakini sasa, atatokaje? Kesi inayomkabili ni nzito na yupo kwenye taifa lenye sheria kali na lisilo na mchezo, hasa na wageni waliojihusisha kwenye uhalifu. Biruse alijikuta akinyong'onyea mno mwili wake mahali hapo alipokuwa amejikunyata.

*****

Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, walipofika kwenye *appatment* yao, ambayo ilikuwa ndani ya mjengo ambao ni moja ya maeneo nyeti ya *KGB,* walimokuwa wanaishi makachero wachache wenye asili ya Urusi, katika jiji hilo la Beijing, alimpandia hewani mkuu wake wa kazi Kamishina Putim Rendozovic, na kumsihi afanye mpango kwa kutumia nafasi aliyonayo, ili Biruse aweze kuwa huru washirikiane naye katika shughuli ile ya kumtafuta Zinaeda.

Maneno ambayo Biruse alimweleza wakiwa kule mahabusu, katika eneo la kuzungumzia, yalimkaa kichwani na muda wote akiwa njiani maneno hayo yaliimba kama wimbo. Na kutokana na maneno hayo, kumkaa sana kichwani, Dimitir Roshkeov, alilazimika kumshirikisha mshirika wake Boros Lobos, juu ya mawazo yale aliyokuwa nayo.

Boros naye, alimweleza ni vyema kuwasiliana na mkuu wao wa idara ili kuona kama kutakuwa na uwezekano wa jambo hilo kufanyika. Ndipo, Dimitir Roshkeov, alipoamua kumpigia simu kamishina wake.

Dimitir, anaona muda unazidi kuyoyoma na dalili za kumpata mwanaye Zinaeda bado ni kitendawili.

Hata hivyo, Kamishina Putim Rendozovic, alimweleza Dimitir Roshkeov kuwa, jambo hilo ni gumu mno. Lakini, alimtaka ampe muda aweze kujaribu kulifanyia kazi kuona ikiwa atafanikiwa ama la!

Baada ya kukomesha maongezi, Kamishina Putim Rendozovic, alifanya mawasiliano na idara ya usalama hilo la China, na kuzungumza na mkuu wa idara hiyo ambaye alikuwa ni rafiki yake wa muda mrefu kutokana na kushiriki pamoja naye katika matukio mbalimba ya kiusalama dunia.

Hata hivyo, mkuu huyo wa idara ya usalama wa China, kutokana na ukaribu aliokuwa nao na Kamishina Putim Rendozovic, alikubaliana na ombi lake kwa mashariti ya kwamba, baada ya kufanikisha zoezi hilo, Biruse arejeshwe kwenye mikono ya serikali ya China, aweze kuungana na wanafunzi wenzake waliodakwa kwenye sekeseke lililopelekea vifo vya watu sita ambao hasa walikuwa ni walinzi katika Chuo Kikuu cha Tsingua.

Walikubaliana hivyo. Nusu saa baadaye, Kamishina Putim Rendozovic alimrejea Dimitir Roshkeov na kumpasha juu ya kukubalika kwa ombi lake lakini zaidi alimweleza pia juu ya makubaliana yao.

Dimitir Roshkeov, hakuwa na neno, yeye anachotaka ni kupatikana kwa mwanaye Zinaeda na mambo mengine hayakuwa shida yake.

Alipokomesha tu mawasiliano, Dimitir Roshkeov alimpasha habari hizo Boros Lobos na pasipo kupoteza muda waliinuka na kuongozana kwenda kumchukua Biruse kule mahabusu. Ambapo baada ya kufika huko, taratibu za kiusalama zilifuatwa na kijana huyo akaweza kuachiwa huru!

*****

Kwa upande wa Destiny, katika hali ambayo hakuitarajia; sasa anajikuta anateswa na jaka la moyo.

Pamoja na ujasiri aliokuwa nao wakati anaipanga mipango ya

kumteka Zinaeda na hata alipofikia maamuzi ya kukitafuta kikundi cha *The Happy Maker,* kumfanyia kazi hiyo, hali ya kutekwa kwa msichana huyo inaanza kuutesa moyo wake.

Destiny, sasa anajihukumu moyoni. Anajiuliza: Kwanini alifanya jambo hilo? Ni kweli anampenda kwa dhati Biruse, ila kwa nini upendo wake uyagharimu maisha ya Zinaeda? Na msichana huyo alikuwa na hatia gani? Hatia yake ni kuwa kwenye uhusiano na Biruse? Destiny kiukweli alijikuta anachanganyikiwa.

Hata hivyo, pamoja na kuchanganyikiwa huko, hakuna ambacho Destiny angeweza kukibadili. Alipokwenda kuzungumza na kikundi hicho cha *The Happy Maker,* walimuuliza swali, tukimteka msichana huyo unataka tumfanye nini? Naye aliwaambia; futeni ushahidi, yasibaki hata mabaki yake!

Sasa ni siku ya pili toka Zinaeda atekwe, moja kwa moja Destiny anafahamu tayari msichana huyo alikuwa amekwisha potezwa katika uso wa dunia.

Hata hivyo, kutokana na jaka la moyo ambalo lilikuwa linamkereketa na kumtesa msichana huyo, anajikuta anapata msukumo wa kuwasiliana na kikundi kile ili ikiwezekana kama bado Zinaeda anapumua aweze kumnusuru. Suala la kuwatenganisha na Biruse, anawaza atalitafutia ufumbuzi mwingine lakini si huo wa mpaka kuyagharimu maisha ya mtu. Destiny aliwaza, hata suala hilo tu la kutekwa kwake Zinaeda, akielezwa juu ya sababu hasa zilizosukuma atekwe pengine moyo wa kumpenda Biruse ungekufa. Kwa hakika, Destiny moyo wake unamhukumu na kumwambia kwamba, kwa kumuua Zinaeda, damu yake itamlilia katika kipindi chote cha maisha yake!

Destiny aliichukua simu yake ya mkononi na kumpigia mkuu wa kikundi kile cha *The Happy Maker,* aitwaye Chineke Udu.

"Chineke…" Destiny aliita akizungumza kwa sauti iliyopoa mno baada ya Chineke kupokea simu yake.

*"Ah! Bossy Lady!"* Chineke aliongea kwa bashasha.

Destiny alisukuma mgumo hafifu akijaribu kulazimisha furaha

ambayo hakuwa nayo.

"Upo wapi?" Alimuuliza.

"Kwani unasemaje madam, na mbona leo haupo kwenye furaha zako, yule msichana tushamaliza, unapaswa kuwa na furaha ebo!"

Hapo moyo wa Destiny, ulidunda kwa nguvu na mapigo yakaanza kwenda kwa kasi isiyokuwa ya kawaida.

"Chineke mlimmaliza?" Aliuliza akiwa na shauku ya kusikia vinginevyo.

*"Haa!* Sasa anawezaje kuwa anapumua mpaka dakika hizi, sisi tukipewa kazi hatumcheleweshi mtu. Halafu haya mambo mengine si ya kuzungumza kwenye simu madam. Lakini pia, sisi na wewe mkataba juu ya jambo hili ulikwisha malizika…kazi yako tuliifanya na chetu ulikwisha tulipa…kila mtu afe na hamsini zake…"

Destiny, alimwaga pumzi nyingi nje. Anashindwa hata aseme nini. Kauli imemtoka na nguvu zote za mwili wake anahisi zimemwishia.

Katika namna ambayo hakuitarajia, machozi yalianza kujitengeneza machoni pake na punde si punde machozi hayo yalimbubujika mashavuni. Katika maisha yake yote hakuwahi kujihusisha kwenye vitendo vya namna hiyo. Ni msukumo wa mapenzi ndiyo umemsukuma atende unyama huo. Destiny moyo wake upo hatiani. Anajilaumu kwa nini hakuyawaza hayo yote kabla ya kuchukua hatua ile aliyoichukua ya kuwatafuta kina Chineke Udu. Mwanaume huyo mwenyewe anayempenda anauhakika gani kuwa baada ya kupotea kwa Zinaeda atakuwa naye kwenye mapenzi.

Destiny anajiona ni mjinga kuliko wajinga wote duniani! Lakini zaidi, anajiona ni mkosefu mbele za Mungu, mbele za wazazi wa Zinaeda, marafiki na Zinaeda mwenyewe. Msichana huyu anatamani apate mahala pa kuuficha uso wake mbele za uso wa Mwenyezi Mungu lakini anapakosa. Kutokana na mazungumzo yale, Destiny alijikuta akiikata simu ile aliyompigia Chineke Udu, akadondoka kitandani pale alipokuwa amekaa na kuufutika uso wake kwenye mto, kisha akaanza kugumia kwenye kilio kikali cha kwikwi!

# 6

“Usilete ujanja wa aina yoyote ile?”

“Siwezi.”

“Kumbuka ujanja wa aina yoyote utamaanisha kuyachezea maisha yako!”

“Naomba mniamini, siwezi kufanya jambo lolote lile nje ya makubalino yetu. Ninachohitaji ni Zinaeda apatikane mzee wangu, hakuna kingine!”

“Sawa.”

Dimitir Roshkeov, alimtazama Boros Lobos, kisha akamwelekeza kwa ishara kuwa alegeze vitasa vya mlango wa gari ile waliyokuwemo ili Biruse aweze kutoka.

Hayo yalikuwa ni majira ya saa kumi za jioni baada ya kumtoa Biruse mahabusu. Katika mazungumzo yao baada ya kumtoa, walikubaliana wampe Biruse nafasi ya kufanya uchunguzi wake kwa kipindi cha saa mbili, kisha watakutana kwa ajili ya kupata mrejesho wa nini alikibaini ambacho pengine kingeweza kusaidia katika kumpata Zinaeda.

Biruse hakutaka kuambatana kila mahala na kina Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, kwa sababu aliwaeleza kufanya kwake hivyo, kutawafanya wasizipate taarifa ambazo wanahitaji. Kutokana na hali ilivyokuwa ya kushikiliwa kwa wanafunzi na yote yaliyotukia chuoni kwao, halafu yeye kuonekana yupo huru, kunaweza kukaibua maswali mengi na wenzake wanaweza wasimuamini hata kumpa taarifa anazozihitaji.

Sababu hizo, zilionekana kuwa na mashiko na ndipo kina Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, walipokubaliana naye kwa makubaliano

ya kuwa, baada ya saa mbili mbele wangeweza kuonana na kujadili mawili matatu.

Breki ya kwanza ya Biruse ilikuwa nyumbani kwake kwenye *apartment* alikokuwa amepanga. Alipoingia ndani aliyatazama mazingira ya chumba kile kwa makini, hakika hayakuwa na tofauti kubwa na namna ambavyo aliyaacha kwa mara ya mwisho alipoagana na Zinaeda na yeye kuelekea chuoni kwa ajili ya kile walichokuwa wamekipanga kukifanya pamoja na kikundi cha wanafunzi wengine.

Biruse, ndani ya chumba chake kile kuna mahali alikuwaameficha simu ya mkononi ambayo alikuwa akiitumia katika mawasiliano yake ya siri na watu wachache ambao hakutaka kuwasiliana nao kupitia kwenye simu ya kawaida. Aliichukua simu ile na kuiwasha.

Baada ya kuiwasha alikuta kuna jumbe kadhaa mbapo baada ya kuzisoma aliamua kuachana nazo. Ndipo akayatafuta mawasiliano ya Fanta na kumpigia. Biruse alihitaji kuzungumza na Fanta kwa maana ni miongoni mwa watu wake wa karibu ambao anataarifa kuwa hawakukamatwa. Anafahamu kwa kuzungumza naye kuna mambo atayafahamu juu ya hali halisi ya mambo yalivyokuwa yanaendelea huko nje.

Baada ya kuipigia namba ile, simu upande wa pili ilianza kuita na baada ya sekunde chache hatimaye iliweza kupokelewa:

*"Hallow!"*

"Fanta!"

"Biruse."

"Hali yako?"

"Si salama."

"Nafahamu."

"Umetoka?"

*"Yes…!"*

"Umetokaje?"

"Ni simulizi ndefu Fanta."

“Unaweza kufupisha?”

“Si kwenye simu, upo wapi?”

“Golden Coastline!”

“Beach?”

“Ndio.”

“Unafanya nini saa hizi beach?”

*“Ah!* Nimekuja kusafisha akili B. Haya yanayoendelea si madogo.”

Biruse alishusha pumzi fupi. Namna ambavyo Fanta alizungumza, ilidhihirisha wazi kile kilichomo ndani ya moyo wake. Msichana huyo hakuonekana kuwa sawa kabisa. Na Biruse alimuelewa vyema. Kweli mambo hayakuwa madogo. Ni mazito na wakati wanapanga hayo yote waliyoyafanya hakuna aliyewaza yangetokea yaliyotokea.

“Nahitaji kukuona,” hatimaye Biruse alimweleza Fanta.

“Muda gani?”

“Ikiwezekana mida hii.”

“Vipi kuhusu Zinaeda? Kuna lolote lile umesikia?”

“Achana na haya mambo kwenye simu Fanta, kumbuka tupo China. Tuonane.”

Ikawa sasa ni zamu ya Fanta kushusha pumzi fupi. Mwishowe akamwambia Biruse, “Sawa. Dakika arobaini mbele tuonane. Ingawa sijajua wapi?”

“Nakuja kwenye apartment yenu!”

“Sawa.”

Dakika kumi baadaye, ndipo Biruse alitoka ndani ya chumba chake baada ya kujimwagia maji mwilini ili kujiweka sawa pamoja na kubadilisha mavazi aliyokuwa ameyavaa kwa kitambo kidogo.

Baada ya kutoka, alitembea hatua chache akawa ameifikia barabara ambayo ilikuwa inaungana na barabara kuu iliyoelekea katikati ya mji huo wa Beijing. Ndipo kijana huyo alipoangaza huku na huko, akasimamisha gari ndogo ya abiria, *‘taxi’,* aliyoiona ikija katika uelekeo aliokuwepo. Baada ya gari hiyo kusimama, alimuagiza

dereva kumpeleka kule alikokuwa anahitaji ampeleke.

Dereva wa ile taxi alikuwa ni mzee mmoja mwenye kati ya miaka sitini na sabini. Lakini, kwa muonekano wake alikuwa anaonekana ni mtu mwenye nguvu na kilichomvutia zaidi Biruse, mzee huyo alikuwa ni mweusi.

"Ni nadra sana kuona watu weusi katika taifa hili la China. Hasa wazee kama wewe." Biruse alishindwa kukaa na donge lake moyoni. Hatimaye alimweleza yule mzee.

Yule mzee alichezesha kichwa na kumtazama kijana huyo, kisha akakirudisha kutazama mbele kule walikokuwa wanaelekea.

"Watu weusi wapo kila mahali!"

"Umekuwepo China kwa muda gani?"

"*Ah!* Muda mrefu sana. Toka enzi za Li Xiannian."

"Rais Li Xiannian! *Mh!* Kweli umekaa sana. Umekula mema mengi ya China."

"*Ah!* Kuna mema basi hapa. Kwa wageni hasa watu weusi ni machungu tu. Masuala ya ubaguzi yamekithili sana?"

"Lakini ubaguzi upo katika kila taifa mzee wangu. Bahati mbaya suala la ubaguzi huwa tunalitazama kwenye upande mmoja wa shilingi. Mtu mweupe kumbagua mweusi. Lakini, ukweli ni kwamba mzee, hata sisi Afrika kuna namna tunawabagua hawa watu weupe."

Yule mzee alidakia haraka: "Inawezekana ikawa hivyo, lakini kumbuka chanzo cha ubaguzi na yote yanayopelekea watu duniani tusiishi pamoja yametokana na hawa watu weupe. Unafikiri kama si biashara ya utumwa duniani, leo kungekuwa sehemu salama sana ya kuishi. Haya biashara ya utumwa ilifanywa na nani kama si hawa watu? Unafahamu historia kweli wewe?"

"Lakini, ukizungumzia biashara ya utumwa mzee, chanzo chake ni masilahi. Ukitazama katika historia hiyo unayojaribu kuijengea hoja, hata kabla ya utumwa, jamii na jamii zilikuwa ni ngumu kukaa pamoja kwa kipindi kirefu pasipokuwa na vita vya kimasilahi. Huyu anataka amtawale yule na huyo hataki kutawaliwa. Kwahiyo,

suala la mmoja kuwa mtawala na mwingine kuwa mtumwa kwa mtazamo wangu ni suala la asili ya mwanadamu. Hata wasingekuja Wazungu isingetokea watu wakaishi pamoja."

"Hivi kijana unaelewa unachozungumza kweli. Au umeamua kuharisha kwa kutumia mdomo! Ama huelewi hata maana ya utumwa ni nini? Utumwa tunaouzungumzia hapa, ni ile hali ya mtu kukutawala kwa mabavu na akikudhooficha katika hali yako yote ya kibinadamu.

"Kuanzia nguvu, utashi, akili mpaka kuliongoza kusudi la kuzaliwa kwako. Hii hali kwa historia unayojaribu kuieleza wewe, ilitokea kabla au baada ya kuja kwa biashara ya utumwa?"

Biruse alicheua tabasamu hafifu akilazimisha kusukuma kicheko kifupi. Pasipo kutarajia alijikuta akipandisha kichwa na kushusha taratibu mara kadhaa kuonyesha yule mzee yupo vizuri na anaelewa vyema anachokizungumza. Hata hivyo, kwa upande wake, maneno aliyoyazungumza yalikuwa ni katika hali ya kumchemsha akili yule mzee wala hakuwa anamaanisha sana kile ambacho alikisema. Mwishowe akamwambia yule mzee: "Natania tu mzee wangu. Usinichukulie kwa umakini zaidi…"

"Na bora uwe unatania. Maana vijana wa siku hizi hakuna mnachokijua. Mkipita kwenye shule zenu hizo, mnajiona mmeelimika, lakini kumbe mnazidi kujazwa ujinga wa kutokujitambua. Na hayo ndiyo madhara makubwa zaidi ya utumwa ambayo yatatutafuna mpaka pale watu weusi tutakaporudi kwenye ufahamu wetu."

"Ni kweli kabisa unachokisema. *Anyways*…nasikia Li Xiannian, alikuwa ni rais mzuri wa mfano wake kuwahi kutokea hapa China."

"*Ah*! Kila mtu anasema hivyo. Nami nakiri kwakweli, yule bwana alikuwa ni mwanadamu wa sayari nyingine. Ungesikia historia yake ungefuta machozi. Mtu aliyezaliwa kwenye umasikini uliokithili, akawa fundi selemala, kisha baadaye akajiunga na jeshi na hatimaye baada ya misukosuko mingi na safari ndefu, akawa kiongozi wa taifa.

“Nampenda sana, lakini pia ninamkumkumbuka kwa mengi. Yule alikuwa kiongozi wa China wakati ukomunisti ni ukomunisti. Sio sasa! Kumebaki na rangi tu ya ukomunisti. Lakini pia, ndiye msingi wa kusimama kwa taifa hili la China. Alikuwa mzalendo wa kweli na alizilinda kwelikweli rasilimali za Wachina na si ajabu kwa ule msingi alioujenga, leo wamefikia mahala hapa!”

Mpaka wanafika mwisho wa safari yao, wawili hawa walikuwa wamezungumza mambo mengi kuhusu China, masuala ya ubaguzi na mengineyo. Kwa kipindi kirefu, ukiachana na marehemu babu yake mzaa mama, Biruse hakuwahi kuzungumza na mzee wa makamo ya huyu dereva taxi na kuambulia madini kama aliyoambulia hapa. Akili yake ilikili kwamba; watu weusi wanaojitambua bado wapo duniani. Huo utumwa waliokuwa wanauzungumzia haukumaliza kila kitu.

Na hilo ndilo jambo linalotia matumaini, kwamba, suala la kujitambua kwa watu weusi na kujikwamua kwenye aina zote za utumwa linawezekana. Ilihali kuna watu wachache ambao wanajitambua na pamoja na kuishi kwenye minyororo ya utumwa, lakini si watumwa kiuhalisia.

Kabla ya Biruse kushuka kwenye taxi hiyo, alimlipa yule dereva ujira wake, naye yule dereva baada ya kuipokea pesa yake alichukua kadi yake ndogo ya biashara iliyokuwa na mawasiliano yake, kisha akampatia Biruse.

Biruse aliitazama na kusoma ilivyokuwa imeandikwa.

“Hemed Hamdan!” Biruse alisoma na kuongeza, “utakuwa Mswahili wa kwetu wewe…” alisema akitabasamu.

“Unamaanisha nini?”

“Haya majina ya nyumbani kabisa haya.”

“Wewe ni mtu wa asili ya wapi?”

“Tanzania.”

“*Mh!* Tanzania. Kwa mwalimu?”

“Ndiyo kwa mwalimu. Unapafahamu?”

“Ndiyo. Na nimefurahi kusikia hivyo kwamba unatoka kwa

Mwalimu. Kimepita kitambo cha muda mrefu kukutana na mtu kutoka Tanzania. Niliwahi pia kuwa na rafiki Mtanzania, alikuwa anapaita huko Bongo. Ndiye alipata kunieleza habari za baba wa taifa hilo na falsafa zake. Alikuwa mtu mzuri sana na mkarimu hajapata kutokea mtu kama yeye.

"Alinieleza ndiyo haiba ya watu wake. Namkumbuka sana rafiki yangu. Hajawahi kuondoka akilini mwangu na ni miaka mingi hatupo pamoja."

"Yupo wapi kwa sasa?"

"Alikwisha kwenda mwana kwendazake. Naikumbuka siku aliyofariki kama ni jana vile. Kiukweli ilikuwa ni siku ngumu sana na kifo chake kiliwashitua watu wengi ambao tulikuwa tunamfahamu. Lakini, tulishirikiana kuusafirisha mwili wake huko kwao Tanzania. Toka miaka hiyo sijawahi kuisikia Tanzania, kupitia kwa mtu yeyote mpaka hivi leo ninapokutana na wewe!"

"Aisee," Biruse alizungumza kana kwamba habari zile zilikuwa zimemchosha. "Pole sana na uniwie radhi kwa kukukumbusha juu ya rafiki yako mpendwa."

"Usijali, ndiyo maisha yalivyo. Mambo huja na mambo hupita. Milima hubakia milele. Lakini, huzuni ni kwamba; kadiri tunavyozidi kusonga mbele mazuri tunayaacha nyuma."

Kwa busara za huyu mzee, Biruse alisema moyoni mwake akizidi kumsikiliza anaweza kujikuta wamekaa pamoja siku kadhaa akisherehekea tu madini yake. Kutokana na ratiba aliyokuwa nayo na mambo aliyojipangia kuyafanya kichwani, alilazimika kukatisha mazungumzo yale:

"Mzee wangu, tutawasiliana. Asante kwa ukarimu wako, nimejifunza mengi na nimefurahia sana kutumia usafiri wako! Tukikutana wakati mwingine utanieleza wewe ni mtu wa wapi!"

Mzee Hamdani alitabasamu na kumwambia Biruse: "Usiache kunitafuta ukiwa unauhitaji wa usafiri."

"Wala usijali. Ilimradi kadi yako ninayo basi safari zangu zote zitaambatana na wewe!"

"Biruse alishuka ndani ya gari ile ndogo ya abiria na kuufunga mlango wa gari.

FANTA alipofika ndani ya *apartment* aliyokuwa anakaa pamoja na Destiny, hakufanikiwa kumkuta rafikiye huyo. Jambo hilo lilimshangaza kidogo kwa sababu Destiny hakumweleza kuwa angetoka ilihali waliwasiliana saa moja iliyopita.

Hata hivyo, Fanta hakujali sana. Pamoja na kwamba Destiny hakumuaga, alifahamu ni mtu mzima mwenye maamuzi na utashi wake. Kwahiyo, aliamua kuchukua hamsini zake. Binti huyo alibwaga mkoba wake kwenye sofa dogo la kukalia mtu mmoja naye akajibwaga kwenye sofa jengine.

Simu yake alikuwa ameishika mkononi. Aliibofya bofya mara kadhaa kisha akamtumia Biruse ujumbe mfupi wa maandishi kuwa amekwisha fika. Alipohakikisha ujumbe huo umemfikia Biruse, aliiweka simu yake pembeni jirani na mkoba wake alipoubwaga.

Dakika kumi mbele, ndipo Biruse alisimama mbele ya mlango wa apartment hiyo ya kina Fanta na Destiny na kubisha hodi.

Fanta alikwenda kufungua mlango na Biruse aliingia ndani.

"Fanta."

*"Hey*….karibu."

"Asante."

Biruse alichagua sofa na kukaa. Fanta alikaa kwenye sofa la mbele yake. Wakawa wanatazamana kila mmoja akikaa kwenye mkao ambao ulionyesha alikuwa makini na maongezi ama mkutano wao huo.

"Vipi?" Fanta alimuuliza.

Biruse alishusha pumzi fupi.

"*Ah!* Wewe acha tu…" alisema taratibu.

"Najua…mambo ni magumu."

"Magumu kweli si mchezo."

"Vipi Mohamadoe?"

"Sina taarifa zozote kwakweli."

“Yupo ndani na vijana wengine kama kumi hivi. Na kinachoonekana hii kesi imekaa vibaya sana wote waliokamatwa wataozea jela.”

“Nani kasema?”

“Ndivyo zinavuma hivyo chuoni B.”

*“Duh!”*

“Ndiyo hivyo, tumewaponza watu Biruse.”

“Hapana Fanta. Tena usije ukathubutu kuiingiza nafsi yako lawamani. Mabadiliko ama suala la haki lina gharama yake. Na wakati wote huwezi kuchagua ikugharimu kwa kiasi gani!”

Fanta alipandisha kifua juu na kuvuta pumzi nyingi kisha akazimwaga kwa mkupuo mmoja. Baada ya kukaa sawa, alimuuliza Biruse:

“*Enhee* nieleze; umetokaje?”

Biruse alimsimulia kila kitu pasipo kumficha jambo lolote lile.

Kwa mara nyingine, Fanta alibwaga pumzi nyingi. Pamoja na maneno ambayo Biruse alimweleza hapo awali kwamba asiidumbukize nafsi yake lawamani, bado kwa yote yanayoendelea Fanta anaona hawezi kuepuka kujitupia lawama.

Kama si maandamano hayo, waliyoyaratibu yeye pamoja na Biruse anauhakika watu wote ambao wapo mikononi mwa polisi wakati huo, na Zinaeda ambaye ametoweka, wangekuwa wanaendelea na utaratibu wa maisha yao kama ilivyokuwa kawaida. Lakini, sasa ni hekaheka mtindo mmoja na mbaya zaidi mahala alipo Zinaeda ni kitendawili.

“Kuna hizi video hebu zitazame!” Biruse alitoa simu yake mfukoni na kumuwekea Fanta, vipande vya video, moja iliyorekodiwa kwenye apartment anakoishi na nyingine iliyorekodiwa na kamera zilizofungwa kwa jirani yake, yule mama wa Korea Kusini aitwaye Xao Chung.

Fanta aliichukua simu ya Biruse na kuanza kuzitazama zile video. Alizitazama mara nne, akizirudia kila alipomaliza kuzitazama.

“Mbona kama hili gari ninalifahamu?” Fanta alisema.

Mapigo ya moyo wa Biruse yaliongeza mwendo wa kudunda.

Kitu ambacho Biruse alikigundua kwenye moja ya video hizo, ndicho hicho hicho ambacho Fanta naye amekibaini. Akajikuta anamweleza:

“Hata mimi niligundua hii gari si ngeni machoni pangu, lakini katika kumbukumbu zangu sikumbuki inamilikiwa na nani kati ya rafiki zetu?”

“Hii gari ni kama gari ambayo Destiny huwa anakodi kwa ajili ya matembezi mbalimbali.”

Biruse aliicheza tena ile video kwenye simu yake. Na hapo ndipo akili yake ilipofunguka na kumbukumbu zote zikamrejea.

“Fanta…si kama, ni yenyewe!”

“Hakika ni yenyewe.”

*“Mh!”* Biruse alijikuta akiguna. Maswali sasa yameanza kufumuka akilini mwake. Anajiuliza; Destiny alikuwa anafanya nini majira hayo mahali hapo? Na kama si yeye ni nani ambaye alikwenda kuikodi gari hiyo na kufika eneo la tukio katika majira ambayo Zinaeda alipatwa swahibu hilo.

Wakati Biruse akijiuliza hayo, kwa upande wa Fanta anakumbuka mazungumzo yake ya mara ya mwisho na Destiny juu ya namna alivyokuwa anamueleza kuwa anampenda Biruse kwa dhati na yupo tayari kufanya jambo lolote ili tu kuwatenganisha Biruse na Zinaeda.

Hapo woga unaingia. Anawaza akilini; Destiny asije kuwa amefanya ujinga ambao utamgharimu na utayagharimu maisha ya mwenziye.

“Destiny yupo wapi?” Biruse anamuuliza Zinaeda na anakuwa amemzindua kutoka kwenye tafakari zile alizokuwa anaogelea.

“Sijui kwakweli.”

“Mpigie simu.”

“Hapana, mimi nina wazo Biruse…”

Biruse alimtupia macho ya moja kwa moja Fanta pasipo kuzungumza jambo lolote.

“Wazo gani?” hatimaye alimuuliza.

"Tusimpigie simu Destiny."

"Kwanini," alimuuliza haraka.

"Wewe nenda kwenye kampuni ambalo huwa anakodi hiyo gari ukapate taarifa ilikodiwa na nani katika siku hiyo ya tukio, hapo tutapata mwaga zaidi. Tukimpigia na kuanza kuzungumza naye tunaweza kuharibu kila kitu."

Mawazo hayo ya Fanta kwa hakika yalikuwa ni mazuri na Biruse aliafikiana nayo. Hakupenda kupoteza wakati. Haraka kwa mwendo wa umeme, alichukua kadi mfukoni mwake iliyokuwa na mawasiliano ya mzee Hemed Hamdan. Alinakili namba ya simu ya mkononi ya mzee huyo na kumpigia. Alipompata alimpasha kuwa kuna mahala anahitaji kumpeleka.

Mzee huyo alimwambia ndani ya dakika chache mbele atakuwa amekwisha kisogeza chuma mahala hapo alipomwelekeza!

# 7

Destiny, moja haikai wala mbili haikai. Mawazo ni tele yanayokisonga kichwa chake. Anawaza hili na kabla ya kulipatia ufumbuzi anawaza jengine. Mawazo yamesongamana kichwani na hayataki kumpatia kabisa nafasi.

Ukweli ni kwamba, kitendo alichokifanya badala ya kumpa furaha aliyokuwa anaihitaji sasa kimegeuka mzimu unaomuandama. Tena unamuandama kwa kasi ya ajabu na upo mbioni kumtafuna *'nyamnyam!'*

Katika majira haya, ya jioni hii, jioni ambayo jijini hapa Beijing kulikuwa kumepoa kutokana na hali ya hewa ya siku hiyo kuja kwa upole na utuvu wake, yupo kwenye mgahawa mmoja wa vinywaji moto na baridi, na mbele yake kulikuwa na chupa ya kinywaji chenye kilevi kikali.

Kinywaji hicho, Destiny alikuwa anakibugia kwa pupa. Glasi zilikimbizana mdomoni. Akitua, kabla hajameza, glasi nyingine inapanda. Destiny anatamani aivuruge akili yake kabisa na asipate kujitambua kwa wakati huo ili yote aliyojitwika kichwani asiuhisi uzito wake. Hayo yote ambayo Destiny alikuwa akiyafanya, yalitokana na hatia ambayo ilikuwa inamshitaki moyoni mwake.

Akizidi kubugia ulabu, mara simu yake iliita. Alijikuta anabwabwaja: *mshenzi gani tena huyu anayenipigia simu muda huu nipo kwenye starehe zangu?* Alimalizia kwa kushusha msonyo mkali: *mchiiiiiiiii!*

Kilevi kilikuwa kimeanza kufanya kazi kichwani kwa mwanadada huyu na mhimili wake ulikuwa umekwisha anza kupotea. Hata hivyo, aliitoa simu yake na kuitazama: Fanta! Alisoma kwenye

kioo na sauti yake iliyokuwa imeanza kukolea ulevi!

Akaipokea.

"Destiny!"

*"Hey!"*

"Upo wapi?"

"Baa kipenzi."

"Baa…?" Fanta alisema kwa mshangao, akaongeza, "unafanya nini baa leo?" Fanta hajawahi kumsikia Destiny, akizungumzia habari za starehe tofauti na siku moja moja za wikendi ambazo huenda klabu.

"Ndio nipo baa. Nakunywa pombe, nataka ninywe mpaka nife kabisa!"

Maneno ya Destiny yalimshitua na kuzidi kumchanganya Fanta. Namna ambavyo rafiki yake huyu anazungumza ni namna inayoonyesha wazi hayupo sawa. Akamwambia.

*"Hey D… come down!* Nambie unashida gani na upo wapi nikufuate?"

Katika namna ambayo Fanta hakuitarajia, badala ya Destiny kumjibu alianza kuangua kilio.

*Ama!* Fanta alizidi kustaajabu. Huyu rafiki yake leo amepatwa na nini? Anajiuliza maswali mengi, lakini maswali yake hayo yanakosa majibu.

Hata hivyo, kwa hali hiyo, Fanta alifahamu wazi kuwa katika siku hii rafiki yake huyu hakuwa sawa na anahitaji msaada wa haraka, kwa hiyo, hakupenda kupoteza muda zaidi wakifanya maongezi hayo simuni. Alichokifanya, alikata simu kisha akamtafuta kupitia mtandao mahala alipokuwa.

Baada ya kumnasa, Fanta alitoka ndani ya chumba chake haraka haraka na kuelekea huko alikokuwa Destiny.

SAA moja baadaye Fanta alikuwa amekwisha rejea pamoja na Destiny mpaka kwenye makazi yao pale walipokuwa wanaishi. Na alipofika alimuweka kitako mwanadada huyo na kumuuliza

tatizo lilikuwa ni nini mpaka alikuwa anafanya hayo aliyokuwa anayafanya.

Alimweleza hajamzoea kwenye hali hiyo na hilo ni jambo linalompa wasiwasi. Fanta alimsihi Destiny ikiwa hatojali, amweleze kinagaubaga ni jambo gani hasa lilikuwa linamsibu.

Fanta alizungumza na Destiny kwa upole mno na kwa kusihi. Hali ambayo ilimfanya Destiny ajihisi uchungu mno moyoni mwake. Pamoja na kilevi alichokuwa nacho kichwani, Destiny bado alimudu kukumbuka kuhusu Zinaeda na nafsi yake ikazidi kumhukumu juu ya jambo lile alilolitenda la kumteka msichana huyo kupitia kwa kikundi cha *The Happy Maker.*

Katika hali ambayo Fanta hakuitarajia, Destiny alianza kuangua kilio. Tena kilio kile chenyewe. Kilio kikali cha kwikwi kilichoambatana na kutokwa makamasi.

Kwa upande wa Fanta, kutokana na hali hiyo halisi aliyokuwa anaiona, kwa kweli kichwani mwake maswali mengi yalizidi kumiminika. Na dalili hizo zilimfanya atafakari kwa kina juu ya video ile ambayo wameiona pamoja na Biruse ambayo ilionyesha gari ambayo Destiny hupendelea kuikodisha kwa ajili ya matembezi yake na shughuli zake mbalimbali kuonekana katika eneo la tukio.

"Destiny…" Zinaeda aliita kwa msisitizo baada ya kuona angalau Destiny amepata mhimili wake. "Nini kinaendelea…?"

Destiny hakuwa na namna nyingine ya kufanya zaidi ya kumweleza msichana huyo kila kitu.

"Mungu wangu!" Fanta alipigwa butwaa. "Destiny ndio umefanya nini sasa!" Alizungumza kwa wahka kubwa.

"Nisaidie rafiki yangu." Fanya alizungumza huku analia.

"Mimi nitakusaidiaje! Hapa tunapozungumza Biruse amekwenda kwenye ofisi za kampuni uliyokodi gari kwa ajili ya kufuatilia taarifa zake, unadhani hapa mimi nitakusaidiaje Destiny!"

Desiny hakuwa na lingine la kusema wala kuongeza zaidi ya kuzidi kulia na kumwaga machozi mengi!

*****

“Akili yako inaonekana ipo mbali mno,” Mzee Hamdan alisema taratibu.

Alikuwa anamwambia Biruse baada ya kuona kijana huyo yupo kimya kwa muda mrefu katika safari hiyo. Jambo ambalo aliliona ni la tofauti.

Alipomfuata ili ampeleke huko watokako katika majira haya, safari yao ilijawa na maongezi kuhusu mambo mbalimbali. Ila kwa sasa ni tofauti. Safari imetawaliwa na ukimya mkuu. Muda mwingi Biruse alikuwa anatazama nje kupitia kwenye kioo cha dirishani cha upande wake. Mzee Hamdan alijiuliza; *huyu kijana muda wote huko nje anatazama nini?* Hakupata majibu. Lakini pia, pamoja na kujiuliza swali hilo, hakuweza kumuuliza Biruse juu ya nini alikuwa anatazama nje. Badala yake, mzee huyu akizidi kukanyaga kibati cha mafuta alipata utashi wa kumuuliza Biruse:

“Vipi Bwana!”alisema taratibu akimrushia macho mara moja kisha kuyarudisha mbele yake kule walikokuwa wanakwenda. “Una shida gani, mbona uso wako umetepeta ghafla.”

Biruse alivuta mafua ambayo hakuwa nayo, kisha kana kwamba asiyetaka, aliyatoa macho yake kule nje alikokuwa anatazama, akachezesha kichwa chake na kumtazama mzee Hamdan.

*“Ah!* Mambo ni mengi mzee wangu!” Alisema sauti yake ikiwa kavu na iliyopoa.

“Ndiyo maisha kijana wangu. Maisha ni mtiririko wa mambo mengi. Na kati ya hayo mengi yanayotutafunia furaha mara zote yanazidi yale yatufurahishayo.

“Lakini, hata kwa uchache wa hayo yanayotufurahisha, bado tunaipata maana katika kuishi kwetu na hiyo maana ndiyo inayotusukuma kuwa na matumaini kwa siku inayofuata.”

“Ni kweli kabisa.”

Ukimya mfupi ulitawala kati ya wawili hawa na baada ya kimya hicho cha sekunde kadhaa; Biruse alimwambie yule mzee:

“Lakini wewe hukunieleza ni mwenyeji wa wapi!”

Kijana huyu amejaribu sana kumpima huyu mzee kwenye mizani yake akimjadili akilini mwake, lakini ameshindwa kabisa kufanikiwa kubaini asili yake ni wapi, kupitia uzungumzaji wake ama hulka zake. Sasa imembidi alitoe dukuduku lake moyoni.

Yule mzee alisajili tabasamu hafifu usoni kwake kana kwamba alilitarajia hilo swali. Biruse naye alimkazia macho. Ndipo akamwambia:

"Nilikweleza nipo hapa China kwa miaka mingi, hiyo haikukutosha kukufahamisha kuwa mimi ni mwenyeji wa China."

"Namaanisha taifa la mama yako."

"Nikisema bado ni hili hutasadiki?"

Biruse hakuzungumza haraka. Alibaki akimtazama yule mzee machoni mwake. Ni kama kuna mawazo yanamwambia huyu mzee kuna jambo anajaribu kulificha. Sasa upande wake mwingine wa akili yake unawaza; *anaficha kwa masilahi gani?*

Na mambo hayo yakipita akilini mwake, mara huyo mzee alimweleza:

"Mimi ni mtu wa Liberia."

"Liberia?" Biruse alionyesha kushangazwa na majibu ya mzee huyo. Hayakumuingia akili. *Hamdan awe Mliberia?* "Si kweli." Alikataa. Akaongeza, "Haya majina yako mbona ya kibantu. Mliberia gani anaitwa Hamdan. Hawa kina Hamdan watu wa Tanga hawa *shekhe!"*

"Na Tanga ni wapi vile?"

"Kwetu huko Tanzania."

"Bongo!" Yule mzee alisema na kusajili tabasamu hafifu usoni ambalo kwa namna fulani lilimfanya Biruse badala ya kumshangaa mzee huyo, hali ya udadisi ilimzidi na hatimaye anaendelea kumtilia mashaka kuwa, kuna jambo alikuwa anajaribu kuficha.

Majina yake yalikuwa yanamsaliti. Mtu kutoka Liberia? Haimuingii akilini bado. Kwa uzoefu wake wa kujifunza na kutokana na mafunzo mbalimbali ya kijasusi aliyokwisha pitia, Biruse alifahamu kuna jambo mzee huyu alikuwa anajaribu kuficha.

Na kweli kama alivyowaza Biruse. Baada ya mwendo mfupi akizidi kumchimba huyo mzee amweleze ukweli juu ya asili yake ni wapi, mzee Hemed Hamdan alisimamisha gari kando ya barabara.

Barabara hiyo haikuwa inapitisha watu wengi kwahiyo waliweza kupata wasaha mzuri wa kufanya mazungumzo mawili matatu.

"Unataka kuufahamu ukweli kuhusu mimi?" alimuuliza.

Biruse hakujibu mara moja, zaidi ya kumkazia macho huyo mzee ambaye hali ya utani imeondoka kabisa usoni kwake. Na kitu kingine kinachomshangaza Biruse, haoni sababu ya jambo hilo kuwa jambo la msingi sana hata liwafikishe mahala hapo. Yaani mtu kusema tu asili yake ni mtu wa wapi mpaka adanganye, azungukezunguke, mpaka wachimbanechimbane. Hakuiona sababu hiyo asirani.

Lakini pia, hakuiona sababu ya kufika mpaka wasimamishe safari. *Sasa hata akimweleza itamsaidia nini?* Alijiwazia pamoja na kwamba alikuwa anatamani kuufahamu ukweli juu ya asili ya mzee huyo.

"Majina yangu ni hayo kama nilivyojitambulisha kwako," mzee Hamdan, hatimaye alizungumza akimtazama moja kwa moja Biruse machoni. Kisha alisugua pua yake kwa ubapa wa mkono kana kwamba alikuwa anayarudisha makamasi ndani, ndipo akaendelea:

"Na kweli, mimi si Mliberia kama nilivyokueleza, ila ni Mtanzania. Kwahiyo, sahau kuhusu ile simulizi ya kwanza ya uongo na kweli kumhusu baba wa taifa Mwalimu Nyerere, na rafiki yangu aliyekufa miaka mingi iliyopita."

Biruse uso wake ulizidi kutahayari. Hata hivyo, mzee Hamdan hakumpa muda wa kutafakari hayo aliyokuwa anayaeleza wala kuuliza maswali yaliyoanza kuporomoka akilini mwake. Aliendelea:

"Nipo hapa kwa ajili ya kazi maalumu kutoka kwa mkuu wangu wa kazi Kamishina Marwa Warioba!"

Mzee huyo, alipolitaja jina hilo la Marwa Warioba, Biruse moyo wake ulilipuka isivyo kawaida. Kamishina Marwa Warioba ndiye mkurugenzi wa idara ya usalama. Kwahiyo akili yake moja kwa moja ilimweleza kuwa, huyu mzee mbele yake ni kachero wa

usalama. Na mpaka amefikia uamzi wa kumweleza hayo, kuna sababu. Pengine anahitaji watambuane au zaidi ya hivyo. Biruse aliamini kama si hivyo, mzee huyo hata kwa kuwekewa kisu shingoni asingethubutu kumweleza jambo lolote lile.

Hata hivyo, Biruse kubaini hayo, ilikuwa ni kana kwamba; alikuwa sasa ameyaruhusu maswali yamiminike kichwani mwake: Hiyo kazi maalumu ni kuhusu jambo gani? Ni kumhusu yeye, usalama wameamua kumfuatilia ama jambo gani hasa?

Biruse alijiuliza maswali mengi mno pasipo kupata majibu ya swali hata moja wapo.

Akizidi kujiuliza na kuwaza ya kwake kichwani, mzee yule alimuuliza:

"Imekuwaje umetoka mahabusu?" Biruse alizidi kutoa macho. Moyoni mwake alikiri, kweli kitengo cha usalama kina mkono mrefu. Na kiukweli Biruse alijiona mjinga kuingia kwenye mikono ya mzee huyo kirahisi namna hiyo. Hata kama hakuwa mwalifu, lakini anaingiaje kwenye mikono ya kachero namna hiyo? Aliwaza. Je, angekuwa adui? Maswali mengi yalizidi kutiririka akilini mwake.

Na akiwa bado anawaza hayo, hajamjibu mzee Hamdan swali alilomuuliza, mzee Hamdan aliongeza: "Kilichonileta hapa na kinachomleta kiongozi mwingine mkubwa wa idara yetu ambaye anafika usiku huu hapa Beijing ni kukutoa wewe mahabusu.

"Lakini, jambo ambalo limetushangaza ni kuona umetoka mahabusu na unaambatana na makachero wa *KGB,* Dimitir Roshkeov na Boros Lobos. Unaweza kunifungua macho nini kinaendelea ambacho hatukifahamu."

Biruse alishusha pumzi ndefu na kupepesea macho dirishani akatazama nje. Huko aliangaza kutazama mambo ambayo hata hakuyazingatia na baada ya sekunde chache alirudisha kichwa na kumtazama yule mzee pembeni yake kwenye kiti cha dereva.

"Kuna tatizo," Biruse alisema taratibu.

"Tatizo gani?"

“Zinaeda!”

“Mpenzi wako?”

“Unamfahamu?” Biruse aliuliza kwa wahka. Kila kitu kinachoendelea leo kinamuacha kinywa wazi. Mpaka Zinaeda anamfahamu! Biruse alizidi kuchoka.

“Hakuna jambo linalokuhusu wewe na silifahamu. *Anyways,* unamaanisha nini unaposema kuna tatizo?”

“Huyu msichana ametoweka na huyo Dimitir Roshkeov ni baba yake mzazi. Wamenitoa kwa lengo moja tu, la kuhakikisha binti yao anapatikana na baada ya hapo napaswa kurudishwa mahabusu.”

Mzee Hemed Hamdan alibaki akimtazama Biruse bila kuweka ishara yoyote usoni mwake. Baada ya sekunde chache ndipo akamuuliza:

“Na unafahamu nini kuhusu kupotea kwake?”

“Sifahamu lolote mzee wangu. Isipokuwa kuna kamera niliweka ndani ya usalama inaonyesha alichukuliwa na watu watatu ambao wamevaa soksi usoni. Ni watu weusi. Lakini pia, kuna gari ilibainika kuwepo eneo la tukio kutoka kwenye kamera za jirani. Gari hiyo ni kutoka kwenye kampuni ya *Avis Car Service.”*

“Ndiyo hapo nilipotoka kukupeleka?”

“Ndiyo. Lakini jambo ambalo linaniumiza kichwa… hiyo gari hupendelea kutumiwa na msichana ambaye ninamfahamu. Ni miongoni mwa rafiki zetu. Ila nilipokwenda kufuatilia taarifa juu ya mtu aliyekodi hiyo gari siku hiyo, ni jina la kiume.”

*“Mh!”* Mzee Hemed Hamdan alijikuta akiguna.

“Huyo rafiki yako siku ya tukio alikuwa wapi?”

“Siku ya tukio ndiyo ilikuwa siku ya maandamano pale chuoni kwetu. Sasa, sina uhakika kwamba naye alikuwa miongoni mwa waandamanaji ama la!”

“Na unahisi anaweza kuhusika na jambo hili?”

“Nimekwisha jiuliza sana lakini sipati muunganiko. Huyu msichana ni binti mpole sana na ni mtu ambaye hana vikundi. Sasa nikijiuliza kwamba anaweza kuhusika nakosa majibu na nashindwa

kupata hata chembe ya sababu ya kumuhusisha!”

“Umezungumza naye jambo lolote lile?”

“Hapana.”

“Basi fuatilia taratibu. Hakikisha unaonana naye. Katika mazungumzo yenu, ukimtazama machoni kuna jambo unaweza kubaini.”

“Sawa!”

“Lakini pia, hakikisha unakuwa makini. Hawa Warusi wakifahamu taarifa zako zaidi wanaweza kuhitaji wakutumie. Usije ukaingia kwenye huo mkenge. *KBG* ni watu ambao tunashirikiana nao, lakini kuna mambo ambayo hatukubaliani nayo.

“Wasije kuhitaji kukutumia kinyemela. Kuna mission unapaswa kwenda kuzifanya nyumbani huko Rwanda na Kongo. Ni *mission* muhimu sana ambazo zitakupa heshima sana kwenye medani za usalama. Pengine heshima kuliko hata baba yako maana unaenda kushughulika na watu wazito, wenye mnyororo mrefu na nguvu. *Goma Cartel.* Kwahiyo kuwa makini sana na kila hatua unayopiga.”

“Sawa mzee nimekuelewa.”

Baada ya mazungumzo hayo, Biruse alimtaka Mzee Hamdan ampeleke katika mtaa wa Dashilan, ambako alipanga kwenda kuonana na kina Dimitir Roshkeov pamoja na Boros Lobos.

Mzee yule, mzoefu kwenye masuala ya kikachero, aliyewekwa hapo katika taifa hilo la China kwa miaka mingi na kitengo cha usalama cha Tanzania, kwa ajili ya kufuatilia mambo mbalimbali ya kiusalama yanayoligusa taifa hilo la Afrika Mashariki, yanayojitokeza huko, aliweka wimbo wa miondoko ya Pop, uliovuma zaidi miaka ya 1980, uitwao *Call Me* wa mwanamuziki Blondie, kisha akakanyaga kibati cha mafuta!

*****

Dakika ishirini na tano baadaye, taxi ya Mzee Hamdan iliegesha katika hoteli ya Beijing Hydre Courtyard, ambapo ndipo Biruse alipanga kwenda kukutana na kina Dimitir Roshkeov, pamoja na Boros Lobos.

Baada ya kuingia ndani ya hoteli hiyo, Biruse akifuata maelekezo alielekea mpaka kwenye ukumbi wa ndani kabisa katika mgahawa mkubwa uliojikita ndani ya hoteli hiyo.

Kijana huyo, aliwakuta wazee wale wa kazi wakipata bia, huku wakizisukuma dakika kusonga mbele kwa maongezi ya hapa na pale.

Aliwasabahi na kuketi pamoja nao. Na ndipo alipowasimulia kila kitu alichobaini katika uchunguzi alioufanya kuhusiano na kutoweka kwa Zinaeda.

"Huyu binti yupo wapi kwa sasa?" Dimitir Roshkeov, aliuliza. Uso wake kwa namna fulani ulionyesha kuwa na ghadhabu.

"Sifahamu ila anapoishi ninapafahamu."

"Inabidi tumchukue. Halafu apelekwe kwenye eneo letu kule kitengoni, akipata mateso sawasawa atasema tu ukweli. Huyu ni lazima anahusika. Hilo ninauhakika nalo."

Boros Lobos, aliyashadadia mawazo hayo aliyotoa Dimitir Roshkeov. Lakini kwa upande wa Biruse ni kama hakukubaliana nayo. Anamfahamu Destiny vyema. Bado haimuingii akilini kwamba msichana huyo anaweza kuhusika kwenye jambo kama hilo la kumteka mtu. Anahisi pengine kuna mtu ambaye ni 'master mind' nyuma ya mpango huo. Na pengine kwa Destiny imetokea tu coincidence kwamba, lile gari huwa naye analikodi ama zaidi ya hivyo, huyo mtu ambaye yupo nyuma ya huo mpango ameamua kumtoa sadaka binti huyo ili iwe ngumu kumfikia yeye.

Kwahiyo, kwenda kumtesa Destiny na bado haimuingii akilini kuwa alihusika na jambo hilo, haoni kama ni sawa.

Biruse pamoja na kukubaliana na kina Dimitir Roshkeov na Boros Lobos juu ya hilo, akilini mwake alikuwa anachakata mawazo kuona ni namna gani atamsaidia binti huyo, Destiny mpaka pale ukweli utakapobainika! Pasipo kufahamu kuwa, Destiny, anayemuwaza amsaidie kumbe ni kweli, yeye ndiye aliyekuwa nahusika haswa na utekwaji wa Zinaeda!

# 8

Kepteni Chimbusu Mwambukusi, alitua Beijing, machweo hivi; na alipokelewa na mzee Hamdan, aliyempeleka moja kwa moja nyumbani kwake katika mtaa wa Yao Mao Sush.

Katika makazi hayo; mzee Hamdan, alikuwa anaishi mwenyewe; familia yake ilikuwa nchini Tanzania. Mara kwa mara alikuwa anaizuru huko na yenyewe ilipata nafasi ya kumzuru pia jijini hapo Beijing.

Baada ya kufika katika makazi hayo, kepteni Mwambukusi, alipata mapumziko ya kipindi kifupi cha muda, yaliyohusisha kujimwagia maji na kupata chakula cha jioni. Na baadaye majira ya saa tatu hivi, wawili hao walipata wasaa mzuri wa kufanya mazungumzo.

Ambapo walikaa sebuleni katika *apartment* hiyo, na waliyasukuma mazungumzo yao kwa vinywaji, huku kwenye televisheni kukizungumzwa taarifa mbalimbali ambazo hawakuzisikiliza kutokana na kupunguza sauti mpaka namba ya chini kabisa.

"Hili suala la hawa Warusi litatupotezea muda!" Kepteni Mwambukusi alimweleza mzee Hamdan. Mzee huyo, akiwa bado hajaichangia hoja hiyo, kepteni Mwambukusi aliongeza: "Huyu kijana anapaswa kwenda Kongo *asap!*"

"Kwani huko mambo yakoje?" Mzee Hamdan alihoji.

"Mambo ni magumu sana!"

"Kwanini?"

"Goma Cartel…" kepteni Mwambukusi baada ya kulitaja jina hilo, alizungusha kichwa mfano wa mtu anayesikitika, "hao watu ni washenzi mno! Hawajali ubinadamu kabisa."

"Kepteni, nini kinaendelea?"

*"Just imagine!"* Kepteni Mwambukusi alizungumza taratibu; "wamesaini mkataba wa mauaji ya wanajeshi mia hamsini wa AU, raia wasiopungua elfu tatu na waziri wa madini na nishati, nchini Kongo, Cante Mukolozi, yupo kwenye hatari ya kuondolewa!"

"Unamaana gani? Kuuawa?

"Hilo siyo swali."

"Usiniambie bwana…!"

"Ndiyo hivyo…."

"Wamesaini mkataba na nani hawa washenzi? 3?"

*"Yes!* Pamoja na Marekani."

"Kwa maslahi yapi?"

"Kwani unafikiri madini yanayochotwa Kongo yanakwenda wapi?"

"Si Rwanda?"

"Rwanda ni wakala tu; lakini *real deal* ni hao ambao wamejichimbia kwenye kivuli."

"Marekani?"

"Ndio; hao ndiyo *master mind* wa kila maafa yanayotokea Afrika kwa sasa. Na unaambiwa madini ambayo yanakwenda kuchotwa huko Goma, katika huu mkakati walionao sasa ni ya kiwango ambacho hakijawahi kutokea. Ni madini ambayo, mbali na kuzidi kuwatajirisha watu wote kwenye hiyo cartel, kwa kuwapa mamilioni ya pesa, itainufaisha sana Marekani. Na M3 watapata misaada ya silaha nzito za kivita na wakati huu wataimarika mno. Hakutakuwa na kikundi cha waasi chenye nguvu kama kikundi hiki.

"Lakini si hivyo tu; hawa Goma Cartel, chini ya kivuli cha Marekani, wanamkono mrefu; ndio hao wanaofadhiri vikundi vya kigaidi Afrika ya Kati, Sierra Leone, na sasa wanashirikiana na kampuni ya Barick International kuchota dhahabu nyumbani Tanzania, kwenye migodi huko Geita wakisingizia wanachukua tu mchanga; makinikia, lakini kumbe wanachota dhahabu tani yao. Na Barick, wamepeleka pia watu wao kwenye machimbo mapya

ya Nyamongo, na wanaiomba serikali kuingia nao ubia walete vifaa vya kisasa kwa ajili ya kusaidia uchimbaji."

"Aisee!"

"Ndiyo hivyo; sasa huyu kijana ndiye *future* ya Afrika yetu. Huyu ana nyota kama ya baba yake. Na sisi kama usalama imani yetu ipo kwake, tunaamini haya yote anatakiwa kuyadhibiti. Na sehemu ya kuanzia ni kuharibu chanzo cha nguvu yao, ambayo ni hawa Goma Cartel. Yaani hii *Cartel* ni sawa na mnara wa babeli, ikisambaratishwa inakuwa ni kama Mungu alivyochafua lugha wakati wa ujenzi wa mnara wa babeli na watu wakashindwa kuelewana. Hawa nao wakisambaratishwa hapo; huu uduwanzi unaoendelea Afrika utakuwa umepata mwarobaini. Maana hawa maharamia watapoteza ile *connection* ambayo walikuwa nayo hapo awali."

"Lakini hii yote ni matokeo ya vita baridi kaka inayoendelea Afrika kote."

"Ni kweli. Lakini, ukitazama mwarobaini wa hiyo vita ni sisi wenyewe. Kwa sababu viongozi wetu wengi wamefanywa kuwa vibaraka. Wanatumiwa halafu wakichuja wanatemwa kama bigijii iliyoishiwa utamu. Nafkiri umefika wakati wa sisi wanausalama kuingilia kati haya yanayotekea na si kukaa nje kana kwamba hatuoni ama hatuyajui."

"Ni kweli kabisa!"

"Ndiyo hivyo."

"Lakini ni mazito kepteni."

"Mazito kweli kweli, na kwa upande wetu ni mbaya zaidi maana damu yote itakayomwagika kwa sasa itakuwa kwenye mikono ya rais wetu."

"Nafahamu, si kwasababu ndiye mwenyekiti wa *AU*, kwa sasa."

*"Yes!"*

Kimya kifupi kilitawala kati ya watu hawa wawili. Mzee Hamdan, alipiga kimya kuyatafakari yale aliyoelezwa na rafikiye kepteni Mwambukusi. Na kepteni Mwambukusi, kimya chake kilikuwa ni

cha kumsubiri mzee Hamdan, atajenga hoja gani baada ya hayo yote aliyomweleza.

Baada ya kimya hicho kudumu kwa sekunde kadhaa, mwishowe mzee Hamdan, aliuliza: “Unawaza nini kepteni?”

Naye kepteni Mwambukusi hakujibu mara moja. Alibaki akimtazama yule mzee mbele yake kana kwamba hakumuona. Baada ya sekunde chache kupita akilitafakari swali lile, ndipo akamwambia:

“Kama nilivyosema, Biruse inabidi arejee nyumbani haraka.”

“Hili jambo lake je, na hawa Warusi?”

Hapo kepteni Mwambukusi, alijenga ukimya mwingine, akitafakari harakaharaka. Akajikuta anacheua kite cha mfadhaiko; *tse!* Aliusugua ulimi pamoja na meno. Ndipo akamwambia: “tunalazimika kumsaidia katika hili jambo, ili alifanikishe haraka nasi tuondoke naye.”

“Lakini nasikia anapaswa kurudishwa mahabusu…”

“Juu ya hilo, kamishina atamalizana na watu wake wa usalama wa huku; sisi tufanye yale yaliyopo ndani ya uwezo wetu.”

“Sawa.”

Basi, baada ya mazungumzo hayo, kepteni Mwambukusi pamoja na mzee Hamdani waliendelea na mazungumzo mengine mbalimbali, huku wakisukuma muda kwa vinywaji. Walipotosheka, kwenye majira ya saa tano na nusu hivi, waliagana kwa ajili ya kupumzika na mihadi yao ilikuwa ni kuamka katikati ya usiku na kuingia kwenye misheni ya kumsaka Zinaeda!

*****

*Duuuuu! Duuuuu! Duuuuuu! Kimya!*
*Duuuuu! Duuuuu! Duuuuuu! Kimya!*

“Anashida gani huyu?” Biruse alijiuliza kwa ghazabu. Akajikuta anasonya na kuinuka kitandani pale alipokuwa amekaa, taratibu akapiga hatua kuelekea dirishani, kisha akafunua pazia na kutazama nje. Macho yake yalitalii kwenye taa zilizokuwa zimeangaza kila

mahali zikikabiliana na giza la usiku huo.

Kijana huyo, alidumu kwa muda wa dakika kadhaa, macho yake yakitalii huko nje na mfano wa mtu aliyekosa kile alichokuwa anatarajia kukiona huko nje, hatimaye, aliliachia pazia, na akaibofya tena simu yake ndogo ya mkononi. Akaipigia namba ile aliyokuwa anaipigia toka hapo awali.

Hata hivyo, simu hiyo iliita tu, lakini, haikupokelewa kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Hali ya wasiwasi ilizidi kumjaa kijana huyu. Anajiuliza maswali mengi yasiyokuwa na majibu. *Nini kimempata Fanta?*

Haijawahi kutokea binti huyo awe mbali na simu kwa kipindi kirefu namna hiyo. Na kinachomshangaza zaidi, ni Fanta kutopatikana kwenye makazi yake aliyokuwa anaishi na Destiny. *Alikwenda wapi?*Amekwisha jiuliza hilo swali mpaka amechoka, na wala hakupata majibu ya aina yoyote ile.

Jioni ya siku hiyo, Biruse alikwenda na kina Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, mpaka kwenye makazi aliyokuwa anaishi Fanta, kwa malengo ya kuonana na binti huyo, ili waweze kuzungumza naye juu ya Destiny, wakiamini; kutokana na urafiki uliyokuwepo baina ya wawili hao, Fanta atasaidia kupatikana kwa Destiny, hatimaye Zinaeda!

Lakini, si Destiny wala Fanta, wote hawakuwapata katika makazi yao. Wamejaribu kuwatafuta kila ambako Biruse, alidhani wangeweza kuwapata wote kwa pamoja ama kumpata mmoja kati yao, lakini hawakuambulia chochote.

Hata hivyo, baada ya kuwatafuta kwa kipindi kirefu cha muda pasipo mafanikio, walikubaliana kuwa; waende kupumzika na ilfajiri ya siku iliyofuata watalianza upya zoezi hilo la kuwatafuta wawili hao!

Hata hivyo, kwa upande wa Biruse, hakupata huo wasaa wa kupumzika. Anayojiuliza kichwani ni mengi na amekwishakuwa na wasiwasi juu ya usalama wa Fanta. Akiwa chumbani kwake, baada ya kuachana na kina Dimitir Roshkeov na Boros Lobos, baadaye

Biruse alipitisha uamuzi wa kutoka kwenda kumtafuta Fanta.

Baada ya kuupitisha uamuzi huo, Biruse alitupia mwilini suruali yake ya dangilizi na fulana nyeupe, kisha juu akaweka kofia nyeusi ya soksi, aliyoivuta kiasi cha kukifunika kipaji cha uso wake na chini mguuni alitupia raba.

Baada ya kumaliza kuvaa, Biruse alikwenda tena dirishani pale aliposimama mwanzo, akalifunua pazia kwa sehemu ndogo, kisha akatazama nje kupitia kwenye ule upenyu wa uwazi uliopatikana baada ya kufunua pazia.

Aliangaza macho nje, pande zote za mtaa ule aliokuwa anaishi, alipojilidhisha kwenye kile ambacho alikuwa anakiangaza, aliamua kutoka ndani ya chumba chake.

Alishika njia na kuelekea barabara kuu, lengo lake adake taxi, impeleke kule alikokuwa anaishi Fanta, kujaribu kuona ikiwa wakati huo atafanikiwa kumpata.

Alipoingia tu mtaani, akitembea kando ya barabara mara kuna *taxi*, ilipiga honi na kusimama mbele yake. Biruse pasipo kupoteza wakati aliingia ndani ya *taxi* ile. Alipokaa tu, hata akiwa hajamtazama yule dereva *taxi* vyema, ambaye alikuwa ni mtu mwenye asili ya Afrika, aliyevaa kofia kichwani, alimweleza kule ambako anataka kwenda.

Naye yule dereva, akiondoa gari kwa mwendo wa taratibu, alimuuliza:

"Unakwenda kwa Fanta?"

Swali hilo lilimshitua Birusi. Akajikuta anageuza uso haraka, kutoka upande mwingine alikokuwa anaangalia, wakati akiuweka sawa mkanda wa siti yake.

Aliporusha macho akashangazwa na alichokiona.

*"Hee!* Mzee Hamdani?" alisema kwa mshangao.

Yule mzee pembeni yake alitabasamu.

*Kha!* Biruse alizidi kuhamanika akishangazwa na hicho kilichotokea. "Afanalek!" akajikuta anasema kwa hamaniko kubwa. "Kwahiyo mzee unanifuatilia kila ninakokwenda? Huna hata muda wa kulala? We ni kula sahani moja tu na mimi? Sindiyo?" Aliuliza

maswali mfululizo.

Yule mzee naye, akiwa katika hali ya utulivu, alimuuliza akizungumza taratibu: “umeuliza maswali mengi mno, sijui nianze hata na swali lipi kujibu?”

“We anza na lolote lile bhana.” Biruse alizungumza kwa jazba akifungua mkanda wa siti ile aliyokuwa amekalia, safari yake anaiona imekwisha ingiwa na doa!

Mzee Hamdan, kutokana na uzoefu wake, aliisoma hali ile ya taharuki aliyokuwa nayo Biruse, ikambidi azungushe usukani na kuegesha gari pembeni.

“Tulia kijana,” alimwambia Biruse. “Huko unakotaka kwenda Fanta hayupo.” Alizidi kumweleza maneno ambayo yalizidi kumfanya Biruse apigwe butwaa. Akaendelea: “Ila jambo la kumuomba Mungu ni kwamba, mpenzi wako Zinaeda awe hai!”

Biruse alitoa macho.

Anajiuliza haya mambo yote huyu mzee ameyafahamu vipi? Ni saa chache nyuma, toka waachane, haya yote ameelezwa na nani hata yeye asiyafahamu? Alijiuliza.

“Hizi taarifa mimi ninaziaminije?” Mwishowe alimuuliza.

Ndipo mzee Hamdan alimsimulia Biruse namna ambavyo; yeye na kepteni Mwambukusi walivyoingia kazini hata wakafanikisha kumpata Fanta na Destiny. Ambapo baada ya kumhoji Destiny, alifanikiwa kuwaeleza kila kitu juu ya kikundi cha *The Happy Maker,* cha kina Chineke Udu.

Mambo yanazidi kuwa mengi. Jina la *Kepteni Mwambukusi* linazunguka akilini mwake! Huo nao ni msamiati mpya kuusikia. Biruse anajiuliza, huyo kepteni naye ni nani na ametoka wapi? Majibu hapati. Ndipo akaamua asiumize kichwa wakati mtu aliyekuwa na majibu yake alikuwa amekaa pembeni yake. Akamuuliza:

“Huyo kepteni Mwakukisi naye ni nani?”

Biruse akiwa anamtazama mzee Hamdan kwa macho yaliyoashilia shahuku aliyonayo ya kusikia kutoka kwake, mara sauti ilivuma kutoka kwenye siti za nyuma za gari lile!

"Ni mimi hapa!"

Sauti ile ilivuma mfano wa radi wakati wa mvua za masika. Ikapenya kwenye ngoma za masikio ya Biruse mfano wa umeme, ikamkausha kwa mvumo wake na kumfanya kijana huyo akauke kaukau!

Biruse hakutegemea ikiwa ndani ya gari hilo kulikuwa na mtu mwingine. Alipoingia umakini wake ulikuwa kwa dereva na kule alikokuwa anaelekea, na wala si kwenye siti za nyuma ya gari hilo. Huko wala hakuhangaika kurusha macho yake kabisa.

"Usiogope," yule mtu aliyekaa kwenye siti za nyuma alisema taratibu. Akaongeza: "Sisi ni watu wema na nia yetu ni kukusaidia wewe. Ili umpate mpenzi wako Zinaeda: Sawa kijana."

Biruse alijikuta akimeza mate ya baridi yaliyojaa mdomoni. Sasa atasema nini maana watu hawa ni kana kwamba walikuwa wamekwisha mteka!

Akiwa katika hali hiyo, mara alishangaa mzee Hamdan akifungua droo ndogo iliyokuwa kwenye chemba moja, iliyojikita pembeni ya usukani, kisha akatoa bastola ndogo na kumpatia.

"Tunakwenda kwenye kazi." Alimweleza kwa msisitizo ulio wa wazi kabisa. Kule lilipo kundi la *The Happy Maker!"*

"Vipi kuhusu Fanta na Destiny?"

"Wapo salama!"

Baada ya mazungumzo hayo yaliyochukua kipindi kifupi cha muda, mzee Hamduni, mwishowe, alipata utashi wa kutekenya funguo, gari lilipoitika alikanyaga kibati cha mafuta na kuliondoa mahali hapo.

*****

Chineke Udu, kiongozi wa kundi la *The Happy Maker;* ni kijana mrefu kwa umbo na mwonekano wake ulimfanya aonekane jitu la miraba minne. Tofauti na wenzake, kina Uche na Ikena Obemba, pamoja na kwamba wote walipenda starehe, ila Chineke Udu alikuwa zaidi. Ambapo, mbali na masuala ya kustarehe na wanawake pamoja na kunywa pombe kupita kiasi, njemba hili

lilipenda kucheza kamari kwenye kasino mbalimbali.

*Deja Vu Casino,* ni kiwanja ambacho Chineke Udu, alipenda kwenda kwa ajili ya kustarehe na kufanya michezo yake hiyo ya kamari na ndiko Destiny alikowaeleza kina mzee Hamdan pamoja na kepteni Mwambukusi kwamba huko ndiko wanaweza kumpata jamaa huyo. Lakini pia, aliweza kuwapatia picha yake kutoka katika simu.

Majira ya saa saba na dakika hamsini, ndipo mzee Hamdan alikuwa anaegesha gari yake katika gereji ya kasino hiyo na baada ya kuegesha walishuka na kuelekea ndani ya kasino.

Huko, walianza kuzunguka wakimtazama, katika kila mahali ambapo michezo ya kamari ilikuwa inafanyika. Na baada ya zunguka zunguka ya kitambo cha muda, hatimaye waliweza kumuona jamaa huyo kazungukwa na wanawake si chini ya watano ambao walivaa sawa na utupu; wakiwa wanamtomasa sehemu mbalimbali za mwili wake, kijana huyo, aliyekuwa kifua wazi, akianika mbavu zake nje, cheni ya dhahabu ikining'inia shingoni na kwenye pembe ya mdomo wake amechomeka sigara, na mezani kukiwa na bia zisizohesabika kwa urahisi.

Baada ya kina mzee Hamdan na wenzake kumuona, iliwabidi watulie na kuwa wapole. Kama wateja wengine, waliagiza vinywaji na kazi ikawa ni kumsubiri amalize starehe zake kisha waanze kuifanyia kazi azma iliyowapeleka katika eneo hilo.

Kama ni uvumilivu tu, basi iliwabidi wawe wavumilivu maana njemba huyo alibobea kwenye starehe. Suala la kukesha kasino kwake lilikuwa ni jambo la kawaida sana. Ilikuwa ni sawa na mtu ambaye aliutumia usiku wake kulala ndani, basi naye raha yake ilikuwa ni kuutumia usiku wake kulala kasino na mchana kulala ndani. Tena si kulala usingizi basi huo usiku, bali kulala akistarehe kwa kamari, kuvuta sigara ama bangi na kufanya kila aina ya starehe na wanawake.

Majira ya saa kumi na moja alfajiri, baada ya kupunwa pesa zake zote alizokwenda nazo, ndipo Chineke Udu, alijizoazoa pale

kwenye kiti alichokuwa amekaa na wenzake, akapepesuka kutokana na ulevi uliokuwa umemzidia, akaanza kutoka nje ya ukumbi huo.

Kwa namna jamaa huyo alivyokuwa amelewa, ilimbidi baada ya kuingia koridoni atumie mhimili wa ukuta kuambaambaa nao mpaka nje na alipofika nje alijitupa ndani ya gari yake. Akaiwasha na kuweka gia na mfano wa mwendawazimu aliiondoa katika eneo hilo, almanusura hata agonge magari mengine yaliyokuwa katika eneo la maegesho!

*****

Vijana waliokuwa wanaunda kundi hili la *The Happy Maker*, pamoja na kwamba, walikuwa na mambo yao ya kishenzi, haswa ya kupenda starehe na matumizi mabaya ya fedha, lakini shughuli zao za kijambazi, walikuwa wakizifanya kwa umakini usio wa kawaida. Umakini ambao, ulitokana na uzowefu waliokuwa nao katika shughuli hizo, maana wamezifanya kwa kipindi cha muda mrefu!

Na kutokana na umakini wao, ndiyo maana wameweza kudumu kwenye kazi yao hiyo kwa muda huo mrefu pasipo kukamatwa ama kuingia matatani.

Jambo lingine, lililowafanya vijana hawa watatu wawe na tahadhari katika mambo yao, ilitokana na namna walivyowashuhudia wenzao wengi waliokuwa wanafanya shughuli sawa na zao kuingia matatani, wengine kupotelea au kuozea jela, na wengine kupoteza kabisa maisha.

Hata hivyo, pamoja na hayo yote, linapokuja suala la masilahi wakati mwingine vijana hawa walichachawa. Tamaa ya pesa ilikuwa kubwa ndani yao. Walikuwa tayari kazi nyingine walizopewa kuzifanya mara mbili, ilimradi tu wapate zaidi pale kulipokuwa na nafasi ya kufanya hivyo, ingawa kila nukta ya hatua zao walikuwa makini mno!

Na ndiyo maana, walipomteka Zinaeda, kwa kufuata maelekezo ya Destiny, hawakumuua kama ambavyo walikuwa wamekubaliana.

Vijana hawa, walitambua kuwa, Zinaeda ni mtaji kwao. Na hiyo ilitokana na chuo alichokuwa anasoma msichana huyo, chuo cha *Tshingai,* kiliyaelezea maisha anayotoka ama tuseme hali ya uchumi wa wazazi wake ilivyokuwa, kwahiyo walifahamu ikiwa wataitumia nafasi hiyo vyema, basi wanaweza kuchuma pesa zaidi kutoka kwa wazazi wa binti huyo.

Kwahiyo, walichofanya ilikuwa ni kumhifadhi Zinaeda kwenye chimbo lao walikofanyia uhalifu wao, wakimhudumia kwa chakula na vinywaji, wakisubiri siku kadhaa zipite, wazazi wake na watu wanaompenda wahangaike kumtafuta na wao ndipo waweze kuibuka na matakwa yao.

*****

"Angalia asitupotee," kepteni Mwambukusi, alimwambia mzee Hamdan.

"Hawezi." Mzee huyo naye alijibu, akitazama kwa makini kupitia kwenye kioo chake cha mbele ya gari.

"Nafkiri hapo atakuwa amefika."

"Nadhani pia."

"Tushukeni."

"Sawa, tuwe na tahadhari."

"Sawa."

Aliyekuwa mtu wa kwanza kushuka ni kepteni Mwambukusi, aliyekuwa siti za nyuma ya gari. Kepteni Mwambukusi, alishuka kwa tahadhari kubwa, akiwa ameshika bastola yake ndogo iliyoishi kiunoni mwake muda mwingi.

Mtu wa pili kushuka, alikuwa ni Biruse. Naye alishuka akiwa ni mwenye tahadhari na mkononi mwake pia, kama alivyokuwa kepteni Mwambukusi, naye alishika bastola mkononi, aliyopewa na mzee Hamdan.

Mtu wa tatu na wa mwisho kushuka ni mzee Hamdan. Baada ya kuhakikisha amefunga vioo vyote vya gari na kuvikaza; akiwa naye ameshika bastola yake mkononi, mzee Hamdam alishuka ndani ya

gari hiyo na kuufunga mlango wa upande aliokuwepo.

Watu hao watatu, walianza kutembea kwa tahadhari kuelekea upande wa pili, kulipokuwa na jumba ambalo Chineke Udu, aliegesha gari nje yake.

Kwa tahadhari waliyokuwa nayo, iliwalazimu wakati mwingine kujikinga nyuma ya magari yaliyokuwa yameegesha jirani na walikoegesha wao.

Punde wakipiga hatua zao za tahadhari, walimuona Chineke Udu, akishuka ndani ya gari lile, na kwa mwendo wa kupepesuka, walimuona akitembea mpaka alipoufikia mlango. Aliuparamia mlango huo, wala haukufunguka. Ndipo akajipapasa mfukoni na kutoa funguo kisha akafungua na kuingia mpaka ndani. Mlango ukajifunga nyuma yake.

Kina kepteni Mwambukusi na wale wenzake walishuhudia kitendo hicho. Nao pasipo kuchelewa waliendelea kutembea kwa tahadhari mpaka wakaufikia mlango.

Wakiwa mlangoni na bastola zao mkononi, kepteni Mwambukusi alisimama upande mmoja wa mlango na mzee Hamdan, alisimama upande mwingine kisha Biruse alisimama katikati.

Wakiwa hapo mlangoni, walitega masikio yao kwa umakini kusikiliza kilichokuwa kinaendelea ndani ya jengo hilo; lakini, hawakusikia chochote kile kikiendelea. Hakukuwa na mchakato, nyendo za watu, wala chochote kile walichosikia.

Kulikuwa kimya!

Watu wale watatu walitazamana pasipokuwa na yeyote kati yao aliyefungua mdomo na kuzungumza neno lolote lile. Hata hivyo, baada ya ukimya wa sekunde kadhaa, kepteni Mwambukusi, alimfanyia ishara Biruse aingie na ule mlango nao watafuata.

Biruse alivuta pumzi zake ndani akihesabu moyoni; moja, mbili, tatu, kisha alirudi nyuma na kusogea mbele kwa kasi akanyoosha mguu wake na kuupiga ule mlango kwa nguvu zake zote;

*PUUUU!*

Kishindo kikubwa kilisikika wakati mlango ukifunguka na

kwenda kujibamiza kwa nguvu ukingoni mwake.

Kina Biruse, pasipokupoteza muda, waliingia ndani ya chumba hicho kwa sambasoti. Na hiyo ndiyo ilikuwa ponapona yao. Maana walipoingia tu, mara risasi zilianza kunyesha kama mvua kuelekea mlangoni walikoingilia. Kama isingekuwa aina hiyo ya uingiaji wao. Mvua hiyo ya risasi ingewanyeshea na mafuriko yake yangewasomba mpaka kwenye milango ya kuzimu.

Wakiwa sakafuni, kila mmoja wao alitumia umahili wake , kugaragara kuikwepa mvua ile ya risasi iliyokuwa inawanyeshea na kwakuwa bahati ilikuwa upande wao, walifanikiwa kila mmoja kupata hifadhi. Ambapo; Biruse na mzee Hamdan walijificha pamoja nyuma ya ukuta na kepteni Mwambukusi alijificha nyuma ya sofa kubwa.

Ndani ya chumba hicho kulikuwa na giza. Kwahiyo, haikuwa rahisi kumuona adui yao alikuwa upande gani na adui yao hakujua walikuwa wamejificha katika chimbo gani. Lakini, pamoja na hivyo, adui yao huyo, yeye aliendelea kurusha risasi ovyo.

Biruse akiwa nyuma ya ukuta ule, alipiga hesabu zake, kisha zikakaa sawa kichwani. Ndipo alimnong'oneza mzee Hamdan kwamba, atawasha mwanga wa siku yake na kwa kitendo cha haraka mno, atabimbilika sakafuni kuelekea upande wa pili. Akamsihi mzee huyo awe shapu kushambulia kwa sababu aliamini akiwasha tu mwanga wa simu adui ataiona na kuanza kushambulia nao watamuona yupo upande gani.

Basi baada ya kukubaliana, Biruse alifanya kama alivyosema. Alitoa simu mfukoni mwake na kuwasha mwanga wa simu na kuirusha kuelekea pande mwingine wa ukuta; kwa upande wa Chineke Udu, akiwa kwenye chimbo alipojificha aliweza kuuona ule mwanga. Akaanza kushambulia. Hata hivyo, kitendo hicho cha yeye kushambulia, kilimfunua alikuwa amejificha mahala gani, na kepteni Mwambukusi, aliyekuwa nyuma ya sofa lile aliweza kumuona na kutokea upande alikokuwa ilikuwa ni rahisi kumshambulia kuliko alipokuwa amejibanza mzee Hamdan.

Kepteni Mwambukusi bila kufanya ajizi, alianza kumshambulia Chineke Udu na risasi mbili zilifanikiwa kumpata kwenye bega lake la mkono wa kulia. Kitendo hicho kilimfanya Chineke Udu apaze sauti ya kilio cha maumivu. Yalaa! Na kwa mwendo wa haraka sana pasipokupoteza muda walimvagaa mahala pale alipokuwa, wakaisukuma silaha yake kwa mguu wakamuweka chini ya ulinzi.

Biruse alitafuta sehemu ya kuwashia taa, akafanikiwa kuiona. Aliwasha taa ambayo iliangaza ndani ya chumba kile na wakagundua ile ilikuwa ni apartment ya njemba huyo. Haikuonekana katika chumba hicho kuishi mtu zaidi ya mmoja.

Chineke Udu, akiwa anagaragara chini kwa maumivu, Biruse alimsogelea na kumuinua kisha akamuegemeza ukutani. Akamuuliza swali kwa ghadhabu:

"Zinaeda yupo wapi?"

Kimya.

"Nakuuliza Zinaeda yupo wapi?" Biruse mara hii alipandisha sauti yake na ilionekana kujawa hasira na mkazo.

Chineke Udu, badala ya kumjibu alimtemea mate usoni yaliyochanganyikana na damu. Kitendo kile kilimfanya Biruse agande kwa sekunde kadhaa shingo akiivunjia pembeni ya bega lake la upande wa kulia. Ubaridi wa mate yale yakichuruzika usoni kwake ulimfanya apate kinyaa na kifua chake kikajawa na hasira zisizo kifani. Kijana huyo alipoinua uso, aliinuka na mkono wake wa kulia akaurusha kwa nguvu zake zote na kumtwanga Chineke Udu konde la nguvu usoni mwake. Njemba hilo lilibweka kama jibwa koko kwa maumivu makali yaliyosambaa kichwa kizima. Likiwa bado halijakaa sawa, linaugulia kwenye maumivu hayo, Biruse alianza kulishambulia ngumi za kila mahali huku akiongea maneno ya kulitukana na kulilaani.

"Basi bwana basi," mzee Hamdan alisema akimshika Biruse.

Kepteni Mwambukusi pia, alifanya jitihada za kumuachanisha kijana huyo na Chineke Udu. Walifanikiwa wakimuacha yule njemba akiugulia na maumivu yake pale sakafuni alipokuwa

anagaragara.

Hata hivyo, hawakutaka kumpa muda wa kuyasikilizia maumivu yake. Kina mzee Hamdan na kepteni Mwambukusi, walimuinua tena kwa nguvu yule njemba na kumkalisha. Kisha kepteni Mwambukusi alichuchumaa na kumsogelea usoni kabisa. Akamwambia: "Ni heri utoe ushirikiano la, utaendelea kula kichapo, kitakachofuata tutang'oa jino moja baada ya jingine na mwisho utasema tu, lakini wakati huo utakuwa umekwisha umia vibaya mno!"

Basi, baada ya kulibana njemba hilo kwa mateso makali, hatimaye lilisema wapi lilipokuwa chimbo lao walikomficha Zinaeda.

Baada ya kuzipata taarifa hizo, walilifunga pingu na kuliburuza mpaka nje. Wakalipakia kwenye buti la gari, kisha waliliondoa gari kuelekea kule lilikotoa maelekezo.

Waliendesha gari kwa mwendo wa dakika arobani, ndipo wakafika.

Ilikuwa ni nje kidogo ya mji ule wa Beijing, kwenye makazi yaliyotelekezwa muda mrefu na wenyewe. Ambapo njemba hao, wahalifu waliokubuhu, walijimilikisha makazi hayo; wakachimba andaki ambako ndiko walikokuwa wakijichimbia pale ambapo walikuwa wanamaliza kufanya vitendo vya vya kihalifu lakini pia walitumia andaki hilo kuficha silaha zao na mali nyingine za wizi.

Walipofika katika eneo hilo. Kukiwa kunaanza kuelekea kupambazuka; Mzee Hamdan na kepteni Mwambukusi walimtoa Chineke Udu kwenye buti, wakamtanguliza mbele kama ngao yao. Biruse alibaki nyuma kuwapa *back-up,* kwa lolote lile ambalo lingetokea.

Walipofika mlangoni; Chineke Udu alibonyeza kengele; ambayo iliwajulisha watu wa ndani kuwa yupo nje. Kule ndani kulikuwa na kamera za kutazama mazingira yote ya nje. Na Uche Obwagedo ndiye alikuwa karibu na kamera wakati huo, kwa hiyo aliposikia kengele alitazama kwenye kamera; hee! Mapigo yake ya moyo yalianza kumwenda hobelahobela baada ya kuona kile kilichokuwa kinajiri kule nje. Ndipo akamuita mwenzake Ikena Obemba, aje naye ajionee yaliyokuwa yanaendelea huko nje.

Baada ya wawili hao kujiridhisha kuwa hali si shwari, kila mmoja wao alichukua silaha yake na wakaamua kujitokeza ili kukabiliana na hao watu ambao walikuwa wamewateka wenzao.

Hata hivyo, hilo ndilo kosa ambalo walililifanya. Ukweli waliouona kwenye kamera wakahadaika ulikuwa ni ukweli nusu. Kwenye kamera waliona watu wawili ambao walikuwa wamemnyooshea mitutu ya bunduki kamanda wao Chineke Udu, na wala hawakumuona Biruse aliyekuwa amejibanza tayari kwa mapambano.

Kwahiyo, hawa njemba walipoona kupitia kamera ni watu wawili ndiyo walikuwa nje, walijipa kiburi kuwa wanaweza kupambana. Lakini, katika namna mbayo hawakuitegemea, walipotoka nje wakiwa wamenyoosha nitutu yao ya bunduki walishangaa wakianza kushambuliwa kwa risasi ambao hawakufahamu zilitoka wapi.

Hakika, hilo lilikuwa ni pigo la kushitukiza kwao maana hawakulitegemea kabisa na walipojaribu tu kufurukuta, risasi zilikuwa tayari zimekwisha wanyeshea wakalowana chapachapa kwa maumivu na kudondoka chini mfano wa mzigo wa kuni.

Baada ya kuwamaliza watu wale wawili, ndipo Biruse alijitokeza. Wakiwa bado wamemnyooshea Chineke Udu, mtutu wa bunduki walimshinikiza kusonga ndani; ambapo aliwapeleka moja kwa moja mpaka kule alikokuwa amefungwa Zinaenda.

Biruse kumuona Zinaeda katika hali ile aliyokuwa amefungwa alijikuta akiumia mno moyo wake. Mpenzi wake huyo, alikuwa amefungwa kamba mikononi na miguuni, mfano wa mbuzi aliyekuwa anasubiri kuchinjwa. Na kamba nyingine alikuwa amefungwa mdomoni.

Kijana yule alimkimbilia na kumfungua kamba zote kisha walikumbatiana kwa mapanzi ya dhati. Wakiwa wamekumbatiana Zinaeda aliangua kilio cha haja. Uchungu mkali ulimkaba moyoni mwake akiyafikiria yote aliyoyapitia asiyofahamu hata sababu yake ni nini.

Ukweli ni kwamba, ilikuwa ni kazi ngumu kwa Biruse kumtuliza

mwanadada huyo, lakini hatimaye alifanikiwa. Na baada ya kuwa sawa, waliinuka kwa ajili ya kwenda.

Wakiwa wanataka kutoka, Chineke Udu, aliwasihi wale watu wamsamehe na kuiacha roho yake salama. Lakini, kepteni Mwambukusi, hakuwa tayari kwa jambo hilo. Alimnyooshea njemba huyu bunduki kwenye paji la uso; Chineke naye akiwa amekata tamaa alifumba macho yake na sekunde chache mbele kilisikika kishindo cha risasi: *PAAA!*

# 9

*Wiki mbili baadaye…*

**Dar es Salaam, Tanzania.**
**Makao Makuu, Kitengo cha Usalama**

Vigogo wa idara za juu za ulinzi na usalama walikutana kwenye makao makuu ya kitengo hicho, kwa ajili ya kikao nyeti kilichohusiana na misheni mahususi ambayo Biruse alipaswa kwenda kuifanya Kongo.

Unyeti wa kikao hicho, ulianzia kwenye maandalizi yake. Ukiwatoa vigogo wa kitengo cha usalama ambao walifahamu kiini hasa cha kikao kilikuwa ni nini; vigogo wengine mpaka wanafika katika kikao hicho, hawakufahamu nini kinakwenda kuzungumziwa na kujadiliwa. Hata taarifa za kikao walipewa saa moja kabla ya kufanyika kwa kikao chenyewe, na kila kigogo alifuatwa na maafisa wa kitengo mahali alipokuwa.

Katika kikao hicho, alikuwepo mkurugenzi wa idara ya usalama ambaye aliambatana na wasaidizi wake. Alikuwepo pia mkuu wa majeshi, mkuu wa idara ya usalama jeshini *(MI)*, mkuu wa idara ya interejensia ya nchi, waziri wa ulinzi, waziri wa mambo ya ndani pamoja na waziri wa mambo ya nje.

Asilimia kubwa na vigogo hao wote, waliingia katika kikao hicho, wakiwa wamevalia sare zilizotambulisha idara wanazotokea pamoja na vyeo vyao. Watu wachache ambao walikuwa hawajavalia sare, alikuwa ni waziri wa ulinzi na usalama; yeye alivaa suti ya Kaunda ambapo juu ya mfuko wa suti hiyo kifuani, alibandika beji ndogo

iliyochongwa mfano wa bendera ya taifa.

Waziri wa mambo ya ndani na nje, naye alivaa suti, lakini pia, kijana Biruse, ambaye kwenye kikao hicho ndiye alikuwa mtu mwenye umri mdogo kuliko wote na aliyeingia kikaoni kwa nafasi ya *penetrating Officer (PE),* alikuwa amevaa kawaida sana; juu alivaa shati lake jeupe la mikono mirefu alilochomekea kwenye suruali ya kijivu na chini alikanyagia kwenye viatu vyeusi.

Kipoza hewa kikitema baridi la haja lililosambaza hewa safi katika chumba hicho maalumu ambamo kikao kilikuwa kikiendelea; vigogo wale wa ngazi za juu za usalama nao walizidi kuzama kwenye mazungumzo yao;

"Basi hayo yote yaliyotukia China kama nilivyoyaeleza sasa tuyaache nyuma yetu!" Mkurugenzi wa idara ya usalama, Kamishina Marwa Warioba, alizungumza kwa msisitizo na sauti ya mamlaka.

Wakati akizungumza hayo, macho yake yalikuwa yakimtazama kepteni Mwambukusi, lakini baada ya kuzungumza aliangaza macho kuzitazama nyuso za vigogo wengine. Akaendelea kumwaga sera zake:

"Jukumu lililopo mbele yetu ndilo la msingi zaidi," aliongeza kamishina Marwa na alipomaliza kusema hayo, alirusha macho yake na kuyatua usoni mwa Biruse, kijana ambaye kitengo cha usalama kilimtumainia na kilimuhesabu kuwa ndiye *future* ya kitengo hicho, katika upande wa intelejensia na mambo ya kijasusi.

"Seyunguson…" Kamishina Marwa, aliita kwa sauti yake yenye ujazo na msisitizo mkali, akimuita Biruse kwa jina la baba yake.

Biruse alimtazama pasipo kupepesa macho. Ndipo akaitika:

"Naam kamishina!"

"Taifa limekuamini…" Alimwambia.

Biruse alifanya jitihada za kuyalazimisha mate ya baridi yaliyomjaa mdomoni yashuke kooni.

*Taifa limekuamini!*

Maneno hayo yalijirudia akilini mwake na uzito wake, Biruse aliuhisi na ilikuwa ni kana kwamba, maneno hayo yalimfanya ahisi

amelibeba taifa lote mabegani mwake.

Akiwa katika hali hiyo ya kutafakari, alimsikia Kamishina Marwa akiendelea:

"Ni kweli, tunatambua kwamba; tunakutuma kwenye hii misheni ukiwa ndiye *subject* pasipokuwa na misheni za kutosha ambazo umefanya. Lakini, tunaamini mtoto wa nyoka ni nyoka. Anapoaminika na kuwekwa mavumbini nina uhakika hatashindwa kutembea kwa tumbo!"

Biruse alipandisha kichwa na kukishusha akimaanisha alikuwa anakubaliana na mtazamo ule alioujenga kamishina Marwa!

Naye, kamishina huyo, aliendelea kumweleza: "Hii kazi unayokwenda kuifanya ni kwa ajili ya taifa letu, bara letu, lakini zaidi ni kwa ajili ya ustaarabu wetu na kesho ya vizazi vyetu.

"Ustaarabu wetu sisi ni amani na mshikamano. Kwa gharama yoyote ile, tunalazimika kuhakikisha huu ustaarabu hauondoki miongoni mwetu na hata pale ambapo kutaibuka viashiria kwamba unataka kutuponyoka ni lazima kupambana kwa gharama yoyote ile, kuhakikisha ustaarabu huu wa amani unatulia mikononi mwetu.

"Hii kazi ambayo tumekuamini na tunakutuma, ndizo kazi ambazo baba yako; komredi Othuman Seyunguson, alikuwa akizifanya kwa uaminifu na weledi mkubwa na hakika zilimpa heshima mno hata leo ni kielelezo kwenye kitengo hiki cha usalama. Ama nazungumza uongo wakuu?"

Kamishina aliuliza swali hilo na kupepesa macho kuwatazama wale vigogo wengine, nao walitikisa vichwa kumaanisha yale aliyoyazungumza yalikuwa ni ukweli mtupu.

"Sasa imefika zamu yako; ni muda wako wa kwenda kutengeneza jina na heshima yako pia!" Aliongeza kamishina Marwa.

Biruse alijikuta akishusha pumzi fupi.

Baada ya maelezo hayo, kamishina Marwa, alimpa Biruse maelekezo ya kina juu ya operesheni nzima aliyokuwa anapaswa kwenda kuifanya nchini Kongo, iliyopewa jina la kiusalama; ama kwa lugha nyingine, tuseme *code* ya kiusalama iliyojulikana kama

*GM.* Yaani *Goma Magotini.* Ikimaanishwa kuwa; ulikuwa umefika wakati ambao; mtandao wa uhalifu unaojulikana kwa jina la Goma Cartel, ambao unajumuisha viongozi wakubwa wa serikali katika nchi mbalimbali za ndani na nje ya bara la Afrika; wafanyabiashara maarufu, wanamichezo na wanataaluma wenye majina na heshima kubwa, ufikie hatua ya kufutwa.

Huo mtandao, ndio ulikuwa chanzo cha vita zisizoisha huko Kongo, Sudan ya Kusini, Afrika ya Kati na kwenye mataifa mbalimbali. Lakini pia, ulikuwa ni sababu ya ufisadi wa kutisha kwenye mataifa mengi ya Afrika, ukipandikiza ama kushirikiana na makampuni pamoja na taasisi tofauti tofauti. Ni mtandao uliokuwa unaratibiwa na rais wa Rwanda, Emmanuel Matoe; aliyejulikana zaidi kwa jila la *Master Mind!* Akiaminika kwa mipango shadidi na mbinu za kuchochea yote yaliyokuwa yanaendelea kwenye mataifa yenye madini na rasilimali.

Kwa kumalizia, kamishina Marwa alieleza kuwa, mtandao huo wa Goma Cartel, siku za hivi karibuni ulikuwa umesaini mkataba wa mauaji ya wanajeshi mia hamsini wa *AU*, raia wasiopungua elfu tatu na waziri wa madini na nishati, nchini Kongo, Cante Mukolozi, yupo kwenye hatari ya kuuawa!

"Kwa sasa kazi ni moja, ni kuhakikisha tunaokoa maisha ya Mulokozi, lakini pia, kuuvuruga huo mtandao!"

Walikubaliana.

Maelekezo yaliyotolewa yalieleweka na vigogo wengine wa usalama walichangia mawazo yao juu ya misheni hiyo, ambapo pia, waziri wa mambo ya nje, alitakiwa kufanya ziara ya makusudi nchini Kongo, ziara ambayo ingesaidia kupenyeza maofisa wa usalama ambao watasaidiana na Biruse katika misheni hiyo, hasa kwa kukusanya taarifa na *kum-cover.*

Basi, baada ya mipango yote kupangwa na kuwekwa sawa, Biruse alichukuliwa na maofisa wa kitengo hicho cha usalama, wakamrudisha hotelini alikokuwa amefikia kwa ajili ya maandalizi maana usiku wa siku hiyo, majira ya saa nne, ndiyo anapaswa

kuondoka.

Na safari yake ilipagwa kwamba, akitoka Dar es Salaam, atasafiri kwa ndege mpaka jijini Kigali, nchini Rwanda; huko atalazimika kusafiri tena na kwenda kwenye kijiji cha Gasaza; ambako yupo mtu muhimu aliyepaswa kwenda kukutana naye, aitwaye Bihagarason, ambaye alikuwa na maelekezo muhimu ya kumsaidia kwenye misheni hiyo. Kisha baada ya kuonana na huyo mtu, ndipo angeelekea nchini Kongo kwa ajili ya kuianza misheni ile ambako huko atapokelewa na mtu mmoja aitwaye Rosogotason!

*****

Biruse akiwa hotelini, maeneo ya Ubungo Riverside, katika hoteli ya Landmark, alikuwa amejipanga kwa mambo kadhaa ya kufanya kabla ya kuondoka usiku wa siku hiyo kuelekea Rwanda.

Jambo la kwanza; ilikuwa ni kwenda kumuona dada yake aitwaye Halima, ambaye alikuwa ni mgonjwa.

Halima, alikuwa anasumbuliwa na maradhi ya mifupa kwa kipindi cha muda sasa. Ambapo, kuanzia maeneo yake ya kiunoni kushuka chini miguuni mwake, alikuwa akihisi mifupa inatafuna. Toka Biruse arejee kutoka China, hakuwa amefanikiwa kuonana naye kwa sababu za kiusalama. Sasa, hakuhitaji kuondoka kwenda kwenye misheni ile pasipo kuonana naye.

Mwanadada huyo ni dada yake wanayefuatana. Toka udogoni mwao wapo karibu na kiuhalisia Biruse alikuwa sako kwa bako na Halima, kuliko ndugu zake wengine.

Mpaka wakati huo ambapo alikuwa hajakwenda kumtembelea, kila mara walipokuwa wakiwasiliana kwa njia ya simu, Halima alikuwa analalamika; *kwa nini huji kuniona?* Alimuuliza kaka yake. Pamoja na Biruse kumtia moyo na kumweleza hali halisi kuwa sababu zinazofanya asiende kumuona zipo nje ya uwezo wake, lakini pia jambo hilo lilikuwa linamuumiza moyo!

Kwa hiyo, kijana huyo alipanga kwenda kumtembelea maeneo ya Mabibo Jeshini, alikokuwa anaishi.

Lakini, jambo la pili, ambalo Biruse alijipanga kufanya kabla ya kuondoka, ilikuwa ni kununua mahitaji yake muhimu.

Haha hivyo, Biruse alianza na jambo la pili.

Baada ya kupata chakula cha mchana, hotelini hapo Landmark, majira ya saa nane hivi, alitoka na kunyoosha miguu mpaka maeneo ya Ubungo stendi, ambapo kulijawa na wachuuzi wadogowadogo waliokuwa wanafanya shughuli zao mbalimbali.

Hapo, Biruse alinunua fulana kadhaa, vitabu vitatu vya riwaya vya mwandishi Alvin Musiba na kitabu cha mwandishi Jenerali Ulimwengu kiitwacho *Rai ya Jenerali, Juzu ya Kwanza.* Mbali na hivyo, alinunua mahitaji mengine aliyokuwa na haja nayo.

Wakati akiendelea na shughuli zake hizo zote, kuna mtu ambaye Biruse alitokea kuwa na mashaka naye. Mashaka hayo yalitokana na kwamba, alimuona mtu huyo zaidi ya mara mbili katika maeneo tofauti.

Anakumbuka; asubuhi ya siku hiyo, wakati anatoka ili aelekee kwenye kikao chake kilichomuhusisha yeye pamoja na viongozi wa juu wa kitengo cha usalama, alimuona huyo mtu amekaa jirani na kijiwe cha *taxi.* Na kilichomfanya amzingatie huyo mtu, kiasi cha kumkumbuka baadaye, ni namna alivyokuwa anamtazama. Ilikuwa ni kana kwamba kuna jambo alikuwa analifuatilia kwake. Maana, Biruse toka anatoka ndani ya hoteli ile ya Landmark, mpaka anaingia kwenye gari lililomfuata hotelini hapo, alibaini yule mtu alikuwa akimtazama katika namna ya kutohitaji kumpoteza machoni.

Wakati huo, Biruse hakujali sana pamoja na kumtilia mashaka. Majira aliyorudi hotelini akitoka kwenye kikao kile, hakumuona huyo mtu, lakini wakati anatoka kwenda kufanya mahemezi yake hayo Ubungo, ndipo alipomuona kwa mara nyingine yule mtu! Na sasa haikuwa katika mazingira yale aliyomuona pale awali, lakini upande wa pili wa barabara akiwa amekaa kwenye kijiwe kimoja cha kahawa. Na alivyokuwa amekaa, ilionyesha hakuwa pamoja na wale watu kwenye kijiwe kile lakini alikuwa amekaa kimkakati. Jambo ambalo Biruse alilithibitisha kuwa huyo mtu anamfuatilia,

wakati anafanya mahemezi maeneo ya Ubungo Stend, aliweza kumuona maeneo hayo!

Biruse alijikuta anajisehemea: *Huyu mtu ni wazi ananifuatilia huyu!*

Lakini pia akajiuliza swali: *Na kwanini anifuatilie?*

Biruse alishindwa kuhitimisha huo mjadala akilini mwake. Pamoja na mashaka aliyokuwanayo, akili yake nyingine ilimwambia, pengine huyo mtu, yupo na hamsini zake na imetokea tu, amemuona mara kadhaa na pengine imetokea wamekuwa na jambo la kufanya katika muda unao endana hapo Ubungo.

Hata hivyo, pamoja na hoja ambazo akili yake ilikuwa inazijenga; Biruse alijiasa kuwa na tahadhari.

Baada ya kumaliza mahemezi yake, alianza safari ya kurudi hotelini. Na kwakuwa alikuwa anatembea kwa miguu kila mara alikuwa akijihimu kutazama nyuma yake na katika maeneo yanayomzunguka kuona kama atamuona yule mtu, lakini hakuweza kumuona!

Alipofika hotelini, alioga na kupumzika. Majira ya saa kumi na mbili kasoro hivi za jioni, ndipo alitoka tena kwa ajili ya kwenda kumtembelea dada yake Halima, akipanga atumie muda wa saa moja hapo, kisha arejee na kuchukua vitu vyake, aelekee uwanja wa ndege maana muda wake wa kuripoti ulikuwa ni saa mbili na nusu!

Alipotoka nje ya hoteli, alikodi taxi, ya jamaa mmoja aitwaye Rashid, jamaa bongebonge, aliyekuwa anaegesha *taxi* yake katika kijiwe kilichokuwa jirani na hoteli ya Landmark.

Wakati ambao Rashid alikuwa anaiondoa *taxi* yake, Biruse alimuona yule mtu kwa mara nyingine, wakati huu alikuwa amesimama katika kikundi cha madereva *taxi,* waliokuwa kwenye maongezi yaliyoonekana ni ya ushabiki ama mabishano!

*Mh!* Biruse alijikuta akiguna nafsini mwake. Akanong'ona ndani yake: *Huyu lazima yupo kwenye misheni. Haiwezekani iwe hivi hivi, toka asubuhi mpaka sasa anachezea katika eneo hili? Huyu*

*ananifuatilia huyu!*

Mawazo yalikuwa ni mengi kichwani mwake. Na ndipo akapata utashi wa kumuuliza Rashid.

"Kaka samahani…" Biruse alisema wakati Rashid akiondoa gari kituoni, akiendesha kwa mwendo wa taratibu ili aingie barabarani.

"Bila samahani…" Rashid aliitika bila kupoteza umakini wake barabarani.

"Yule jamaa unamjua?" Biruse aliuliza na kumuonyesha Rashid mtu aliyekuwa anamzungumzia.

"*Mh!* Hapana. Ndiyo kwanza nimemuona leo maeneo haya."

Biruse alivuta mafua ambayo hakuwa nayo akipitisha tafakuri mbili tatu kichwani mwake.

"Kwani vipi?" Rashid alimuuliza.

"Usijali, nimemfananisha."

Rashid aliingiza gari barabarani, kwenye barabara ya Mandela. Aliendesha mpaka Ubongo Terminal, kisha akashika barabara ya kushoto kuelekea Mabibo.

Wakiwa njiani wanaelekea huko; Rashid aliweka kwenye gari yake nyimbo za wanamuzi wa zamani wa muziki wa dansi, kina Ndala Kasheba, Remmy Ongara, Tex Moshi William na wengineo na akawa anawazungumzia kwa kuwasifia wanamuziki hao namna walivyokuwa wanaimba nyimbo zenye ujumbe mzito zilizokuwa zinamkosha vilivyo.

Hata hivyo, hakupata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa Biruse, kwasababu, kijana huyo hakuwa mfuatiliaji mzuri wa nyimbo hizo, lakini pia, Biruse alikuwa anawaza ya kwake kichwani; nguvu za kusema ashereheshe mazungumzo hayo hakuwa nazo maana hakuhitaji kabisa usumbufu wa aina yoyote ile. Tayari akili yake imekwisha mwambia awe makini huenda anafuatiliwa. Sasa, kuanza kuzungumzia mambo ambayo hakuyapa umuhimu, lilikuwa ni jambo ambalo hakutaka kulipa nafasi kabisa.

Kwahiyo, kuna muda safari ilitawaliwa na ukimya kati yao.

Walipofika Mabibo Mwisho, walisimamishwa na askari wa usalama

barabarani. Rashid aliegesha gari pembeni ili kuweza kumsikiliza yule askari. Na katika jambo la ajabu, wakiwa wamesimama hapo; kupitia kwenye kioo cha pembeni cha gari katika upande ambao Biruse alikuwa amekaa, alipotazama kwenye kioo hicho, aliona kuna pikipiki kubwa aina ya *Honda XR 250,* ikiegesha pembeni ya barabara umbali mfupi kutoka mahali pale walipokuwa.

Na huyo aliyekuwa akiendesha pikipiki ile, alikuwa ni yuleyule njemba ambaye Biruse alimuona na kumtilia mashaka. Na mara hii, njemba huyo alikuwa ameyaziba macho yake kwa miwani kubwa ambayo almanusura ijae kwenye uso wake wote. Na kilichomfanya Biruse amfahamu njemba huyo ni mavazi aliyokuwa amevaa!

Hapo Biruse alipata uhakika mambo hayakuwa sawa. Hakuwa na mashaka tena kwamba kuna jambo ambalo siyo zuri linamkabili, sasa ukweli ulikuwa ni dhahiri mbele yake kwamba, unaungiwa mkia na huyo anayemuungia mkoa au hao wanaomuungia mkia ni watu wanaofahamu haswa wanachokifanya ama kukitaka.

Swali likawa; *ni kina nani hao wanaomuungia mkia?Na amewafanya nini?*

Na akiwa hajapata majibu ya maswali hayo, swali lingine lilipanda kichwani mwake: *Nifanye nini?*

Mawazo mengine yakamwambia: *Anzisha kasheshe?*

Na hapo akili yake ilimkumbusha moja ya kanuni muhimu wakati akijifunza somo la kukabiliana na adui huko kwenye mafunzo ya usalama. Umahiri na umuhimu wa kuwahi, lilikuwa ni jambo lolilopewa umuhimu katika mafunzo hayo. Tena akakumbuka msemo waliopenda kuusema kwamba; muwahi adui, kabla adui hajakuwahi wewe, maana ukichelewa kumuwahi adui, adui atakuwahi wewe!

Biruse alijipapasa kiunoni mwake na kuchomoa bastola. Kisha alichungulia tena kupitia kwenye kile kioo cha pembeni ya gari katika upande wake. Akaona yule jamaa kwenye pikipiki yake bado amesimama vilevile. Ndipo Biruse aligeuza uso kumtazama Rashid ili amuamuru aondoe gari mahali hapo haraka iwezekanavyo.

Biruse aligeuza shingo, lakini kijana huyo alipogeuza tu uso wake, katika hali ambayo hakuitarajia, alikuta amenyooshewa mdomo wa bastola na yule trafiki na Rashid alikuwa akitetemeka kuliko kawaida, kiasi kwamba amekwisha jiharibia haja ndogo pale pale alipokuwa amekaa kwenye siti ya dereva.

Biruse alihitajia kuwa mtulivu mno. Maana alifahamu kosa moja lingemgharimu uhai wake.

Baada ya yule njemba aliyejifanya trafiki kumnyooshea bastola Biruse, alimuamrisha aweke bastola yake mbele kabisa kwenye kioo cha gari. Biruse alifanya hivyo. Na alinyoosha mikono yake kuonyesha kwamba alikuwa *ame-sarender!*

Na punde tu baada ya kufanya tendo hilo, mara alishitukia pikipiki ikiegesha upande aliokuwepo, na mlango ukafunguliwa. Ndipo hapohapo yule trafiki aliyekuwa bado amesimama ule upande wa Rashid, kwa ishara ya kuchezesha bunduki, alimuamrisha Biruse atoke garini. Biruse alifanya hivyo bila ajizi.

*Hee!*

Kila kitu kilikuwa kinakwenda kasi mno. Biruse na kila shuhuda wa tukio hilo walibaki wametoa macho na vinywa wazi kilichotokea ghafla baada ya Biruse kushusha tu mguu garini ili atoke.

*Tii!*

Yalaa.

*Tii!*

*Aaa!*

Mara ghafla ilisimama Noah nyeusi na mlango ulifunguka. Biruse alimuona Kepteni Mwambukusi na mwanadada mmoja asiyemfahamu.

Biruse akili hapo ndipo zikazinduka. Akazungusha kichwa haraka kutazama kule ambako alikuwa yule trafiki aliyemnyooshea bastola. Hakumuona. Yule jamaa aliyekuwa anamfuatilia yeye alimuona akiwa chini kimya huku pikipiki lake likiwa limemlalia. Hapo ndipo akafahamu jamaa hao walitunguliwa kwa risasi.

"Njoo bwana…" sauti yenye kufoka ilimhimiza.

Biruse alishituka kutoka kwenye ile hali iliyokuwa imeichukua akili yake, na pasipo kupoteza tena muda mahala pale, akakimbilia kwenye gari ile, kisha mlango ulifungwa kwa kubamizwa na gari ile ikaondolewa kwa kasi ikiacha taharuki katika eneo hilo la tukio.

"Kepteni nini kinaendelea?" Biruse alimuuliza kepteni Mwambukusi, wakati gari ile ya usalama ikizidi kutafuna lami.

"Unafuatiliwa."

"Na nani?"

"Goma Cartel."

"Goma Cartel?" Biruse aliuliza kwa kishindo cha mshangao kiasi kwamba uso wake ulitengeneza ndita kadhaa; habari hiyo kiukweli ilikuwa ni ya kushitua mno kwake.

Na kilichomshangaza zaidi Biruse na kumfanya apatwe maswali ni kwamba; hao Goma Cartel, wamezitoa wapi habari zake mapema namna hiyo kuwa, yeye ndiye atakwenda kwenye misheni hiyo? Jambo analofahamu ni kwamba, mkakati huo wa yeye kwenda kwenye misheni hiyo ni wa siri na hakuna anayeufahamu zaidi ya maafisa wa ngazi za juu wa kitengo hicho.

*Sasa nini kimetokea?*

Hao Goma Cartel wamefahamu vipi kuhusu yeye na mahala alipokuwa hata wamfuatilie! Au kuna wasaliti kwenye kitengo chao cha usalama? Maswali yalikuwa ni mengi lakini majibu ni machache.

"Kuna namna taarifa zimevuja," kepteni Mwambukusi alimweleza Biruse.

"Zimevujaje?"

"Bado hatujafahamu haswa, ila jambo la kuelewa hawa watu wanamkono mrefu mno. Hata hapa kwetu wapo. Wapo kila mahali."

Biruse alijikuta akishusha pumzi ndefu. Jambo hilo lilimchosha kwa hakika. Anajiuliza kwa namna hiyo ilivyo, kazi hiyo itafanyikaje ikiwa taarifa nyeti kama hizo zinaweza kuvuja kwa urahisi namna hiyo; na huo mtandao ambao wanatakiwa kuufuta unaelezeka kuwa ni mtandao wa watu wazito, wenye majina, fedha na nguvu ya

maamuzi. Hakika kichwa kilimgonga!

Gari ile aina ya Noah, iliendeshwa, kukiwa kimya garini, na baada ya mwendo wa muda wa dakika zisizopungua ishirini na tano, ilipiga honi katika majengo ambayo Biruse hakuwa anayafahamu. Wala mtaa yalipo majengo hayo hakuwa na kumbukumbu ikiwa aliwahi kufika. Ulikuwa ni mtaa uliotulia na kupangika vyema. Na majengo ya mahali hapo yalikuwa ni ya kifahari kwelikweli.

Wakati Biruse akipitisha macho yake huku na kule, geti lilifunguliwa kisha gari liliingizwa ndani.

Wakashuka watu wanne. Biruse, kepteni Mwambukusi, mwandada ambaye Biruse hakuwa anamfahamu, pamoja na dereva aliyewaendesha. Kisha kepteni Mwambukusi, aliwaonyesha kwa ishara Biruse na yule dada wamfuate.

Walitii. Wakamfuata nyuma ambapo alikwenda kuingia mpaka ndani kabisa ya majengo hayo yaliyotawaliwa na ukimya.

Walipita kwenye korido kadhaa, wakivipita vyumba vilivyoonekana kuwa ni vyumba vya ofisi, lakini hawakukutana wala kumsikia mtu yeyote hadi walipotokea kwenye ukumbi uliopangika utasema sebuleni nyumbani kwa mtu, lakini kina Biruse walifahamu hakukuwa sebuleni kwasababu kwa namna mazingira yalivyokuwa yanaonyesha, mahala hapo hapakuwa sehemu ambayo watu wanaishi.

Ila pengine waliwaza kuwa eneo hilo ni ukumbi wa kupumzikia!

"Karibuni," kepteni Mwambukisi aliwakaribisha kina Biruse na yule dada.

Wakakaa.

Akawauliza: "Vinywaji?"

**Biruse:** Maji.

**Yule dada:** *Coke* baridi?

Kepteni Mwambukisi aliwaletea kama walivyohitaji. Naye mkononi alishika bia aina ya *Henken!*

"Biruse…" kepteni Mwambukusi aliita.

Biruse alirusha macho ya moja kwa moja kumtazama.

Kisha kepteni huyo alimwambia huku akimnyooshea mkono yule dada waliyekaa pamoja naye: “Sasha!” Halafu akahamisha tena mkono na kumnyooshea Biruse, akamtambulisha pia yule dada: “Sasha, huyu ndiye Biruse.”

Yule dada alipandisha kichwa na kukishusha huku usoni akijenga tabasamu hafifu.

Biruse alibaki akimtazama msichana huyo pasipo kusema neno lolote. Amewahi kusikia kutoka nyumbani kwao miaka mingi iliyopita kuwa, baba yake alikuwa na mshirika aitwaye Farida, raia kutoka nchini Kenya. Na huyo mshirika wake alikuwa na binti aitwaye Sasha!

Na baadaye alipoingia kwenye medani hizo za usalama aliwahi kusikia kuwa huyo binti, Sasha, naye ni mwanausalama.

*Ndiye huyu?* Alijiuliza.

Na jibu akalipata hapohapo baada ya kepteni Mwambukusi kufungua mdomo wake!

“Wazazi wenu walikuwa na historia ndefu pamoja katika medani za usalama, na walifanya kazi kwa kushirikiana mno,” kepteni Mwambukusi aliwaeleza.

Biruse na Sasha waligeuza shingo na kutazamana.

Akaendelea: “Kwenye Oparesheni Cartoum O1, walishiriki pamoja kikamilifu huko nchini Sudani ya Kusini, lakini ni oparesheni ya mwisho kushiriki pamoja, kwa maana Farida, mama yako alifia kwenye uwanja wa mapambano.

“Hata hivyo, ndiyo maisha yetu wanausalama. Ni heshima ya pekee pia kufia kwenye uwanja wa mapambano.”

Kepteni Mwambukisi baada ya kuzungumza hayo, aliinua chupa yake ya bia na kupiga mafunda kadhaa, kisha akaishusha. Ndipo akasema: “Sasa,’ kisha alijikohoza na kuvuta mafua, ndipo akaendelea: “hatuna muda wa kupoteza kwenye hizi simulizi zinazowahusu wazazi wenu, ninafahamu mtafahamiana vyema kwa muda wenu mbele kwa mbele, ila naombeni mnisikilize kwa umakini niwaeleze yale ya msingi!”

Baada ya kuzungumza hayo, kepteni Mwambukisi aliyakazia macho yake usoni kwa Biruse.

Akamwambia: “Mipango yote tuliyoipanga na kamishina na viongozi wa usalama wa taifa hili na wale tunaoshirikiana nao Kenya, ambao ndiyo waliotupatia Sasha, itaendelea kuwa kama ilivyopangwa isipokuwa kuna mambo machache yamebadilika. Jambo la kwanza: kwakuwa hatuelewi, hizi taarifa zinavuja kutokea wapi, Biruse hutasafiri tena mwenyewe. Sasha ni mshirika wako kuanzia sasa na wala hamtatumia pia usafiri wa ndege. Mtasafiri kwa njia ya barabara.

“Na makamanda…” kepteni Mwambukusi aliendelea: “hakuna *backup* kwenu zaidi ya nyie kwa nyie. Hamtaruhusiwa kuwa na mawasiliano ya aina yoyote ile mpaka mtakapofika Gasiza. Huko ndiko mtakakofanya mawasiliano ya kwanza na mtawasiliana na mimi.

“Baada ya hapo, hakutakuwa tena na mawasiliano mpaka mtakapofika Kongo. Mkifika Kongo kuna mtu atawapokea. Nitawapa ramani na *code* ya kumpata huyo mtu. Naye ndiye atawakutanisha na Cante Mukolozi. Hapo mtapata maelekezo mengine.”

Kepteni Mwambukusi alinyanyua bia yake na kupiga funda kadhaa kwa mara nyingine, kisha alikunja uso wakati akilazimisha kumeza.

Akapepesa macho kuwatazama wote wawili kwa pamoja. Akafinya uso wake na kuukusanya pamoja. Kisha akawaeleza kwa msisitizo: “Hii ni misheni ngumu, inayowahitaji umakini wa hali ya juu mno; inahitaji kasi, weledi, pamoja na kujituma kwenu.

“Kosa moja litaharibu misheni yote na pengine hata kuwagharimu pakubwa sana. Namaanisha hata uhai wenu. Na mkumbuke hakuna mawasiliano. Kitakachowaongoza ni muda, kufuata maelekezo yote na mengine niliyoyataja hapo juu.

“Kwa vyovyote vile hakikisheni, kufa na kupona mnautumia muda kama ambavyo umepangwa. Mnanielewa!”

Badala ya kujibu vijana wale wawili, Biruse na Sasha walijikuta wakishusha pumzi kwa pamoja. Hakika, misheni hiyo ilikuwa ni ngumu na hatari mno!

Hata hivyo, hawakuwa na namna ya kukiepuka kikombe hicho. Ndiyo maisha waliyoyachagua. Kuwa wanausalama. Watafanyaje sasa? Kikubwa walichofanya ilikuwa ni kuulizia maelekezo zaidi, ambapo walipewa maelekezo yote yaliyohitajika.

“Lakini nawapa tahadhari vijana; kila mara kumbukeni katika maisha yenu ya ujasusi; imani kidogo tu inamfanya jasusi auawe.

“Jasusi pia, halali mahala asipopaamini, ni heri alale porini, na jambo jengine; jasusi halali wakati adui yake yupo macho. Mnanipata?”

Vijana wale mbele yake, walipandisha vichwa na kuvishusha wakimaanisha walikubaliana naye ama walimuelewa katika yale aliyowaeleza.

Basi, baada ya maongezi yale kufika kitembo, na kila kitu kuwekwa sawa; Biruse alimtaka kepteni Mwambukisi kufanya mpango vitu vyake vichukuliwe kwenye hoteli ya Landmark na aliwasilisha ombi lake juu ya dada yake Halima, atafutiwe hospitali kwa niaba yake na aweze kutibiawa chini ya uangalizi maalumu wa madaktari.

Matakwa yake yote yalikubaliwa na kila alichoomba kilifanyika. Usiku wa siku hiyo, ndipo safari ya wawili hawa, Biruse na Sasha ilitegemewa kuanza. Ambapo walipaswa kusafiri mpaka Kenya kisha ndiyo waelekee Kigali, na safari ya kuelekea kwenye kijiji cha Gasiza ianze!

# 10

*Kigali – Rwanda*

Hali ya hewa ya Mji wa Kigali, ilikuwa tulivu asubuhi hiyo. Mawingu yalitanda angani, upepo ulipuliza vilimani na jua lilikuwa bado halijaamka kutoka usingizini. Hewa safi ya oksijeni ilienea kila mahali ya mji wa Kigali. Watu walioga upepo mwanana na uzuri wa mji huu, ni mazingira yake. Bado shughuri za kibinadamu hazijaharibu mazingira hata yalete madhara kwenye tabia ya nchi.

Katika majira hayo, ndipo shughuri za kawaida za uzalishaji mali ndiyo zilikuwa zimeanza kufanyika, wakati Biruse na Sasha wakitua Kigali baada ya safari ndefu ya takribani kilometa elfu mbili na themanini na tano (2,085), wakitumia zaidi ya masaa thelathini (30) njiani.

Biruse na Sasha walitoka usiku wa kuamkia siku iliyopita jijini Dar es Salaam, wakasafiri mpaka Namanga, kisha wakaingia Nairobi asubuhi iliyopita. Wakiwa katika mji huo wa Kenya, walichukuliwa na gari maalumu la usalama lililowafikisha mpaka Kigali, baada ya masaa 19, toka waanze safari yao.

Walipofika Kigali; Biruse na Sasha, walichukua usafiri wa taxi, iliyowapeleka mpaka kwenye hoteli iitwayo Nsengiyumva; walipohitaji kupumzika kwa masaa manne, kabla ya kuianza safari ya kuelekea Gasiza, walikopaswa kwenda kukutana na Bihagarason.

Walichukua vyumba vinavyofuatana katika hoteli hiyo ya Nsengiyumva, ambapo kila mmoja wao alifikia bafuni baada ya kuingia chumbani mwake.

Baada ya kutoka bafuni Biruse aliamua kutulia kidogo kitandani, avute upepo kabla ya kufanya uamuzi wa kwenda kutafuta kifuangu kinywa.

Akiwa ametulia kitandani hapo, alijikuta akiwaza mawili matatu. Aliwaza hili, likatoka, akawaza lingine. Hatimaye mawazo yake yakatulia kwenye misheni hiyo waliyokuwa wanaiendea. Biruse akawaza juu ya unyeti wake, hatari zake na uzoefu wao. Kuna muda akitafakari hayo, alijihisi hofu moyoni mwake. Hofu ikatanda na kutamalaki. Ikamtikisa na kumfanya aweweseke. Ikamshusha na kumfanya asinyae. Akahisi unyonge na kunyong'onyea. Lakini, hofu hiyo kabla haijamzidi na kuzikomba nguvu zake zote, nafsi yake nyingine ilimuibua shujaa ndani yake aliyemtia moyo kuwa; kila kitu kitakuwa sawa. Ikamkumbusha juu ya wimbo wa mwanamuziki wa rege, hayati Nesta Marley, maarufu kwa jila la Bob Marley uitwao *Everything Is Gonna Be Arlight.* Ikasisitiza kwamba; uzoefu ni sawa unahitajika, lakini hata uwezo alionao utamsaidia kufanya maajabu katika uwanja huo wa vita.

Akiyawaza hayo, Biruse alijikuta akiiwaza dunia hiyo ya kijasusi anayoishi. Namna inavyokwenda na hayo yote yanayotendeka na yaliyomfanya yeye kufika mahala hapo siku hiyo. Akajiuliza; kwanini yupo hapo? Akajiuliza tena, namna anavyo-*risk* maisha yake kwa ajili ya usalama wa watu, taifa, bara na ustaarabu wa dunia. Akamuwaza dada yake anayeumwa Halima, akamuwaza mpenzi wake Zinaeda ambaye waliachana China, baada ya kumuokoa kutoka kwenye kikundi cha *The Happy Maker.* Biruse aliiwaza familia yake na marafiki, nchi yake na watu wote wanaopotea kwenye matukio ya vita huko Kongo, Somalia, Sudani Kusini, Afrika ya Kati, na mengine yanayowalazimu watu kama yeye, watu wa usalama kuingilia kati ili kuleta amani, ama kuokoa maisha ya watu wengine wasiokuwa na hatia.

*Ubinafsi!* Upande wake mwingine ukamwambia; ndiyo huo wanaupaka rangi na kuuita masilahi!

*Masilahi!*

Akili yake ikakwama hapo. *Yaani masilahi ndiyo yanafanya watu wakosane, wagawanyike na wauane?* Biruse alijikuta anabwaga kite cha mfadhaiko: *Tsee!* Kijana huyu anajaribu kuitafuta maana ya maisha katika hayo yote na wala haioni.

Watu huzaliwa, huishi na kufa! Hakuna atakayedumu milele. Mwandishi Shaban Robert alisema; *dunia tunapita, kila kitu kitabakia, binadamu ni mchanga, kitabaki milele ni milima!* Sasa kwanini haya masilahi yanaleta maafa ya namna hii katika huu ulimwengu ambao kila mmoja wetu atauacha nyuma yake? Mbona tabia za wanadamu ni kana kwamba wanafikiri wataishi hapa siku zote kutumia hayo wanayoyapata kwa kuwaumiza wenzao ama kuwaua!

Biruse aliwaza na kutafakari mambo mengi mno akizama kwenye kina haswa cha moyo na utashi wake.

Basi, baada ya hayo yote, baadaye, akili yake ilirudi kutoka huko ilikokuwa imepotelea na akajikuta anakumbuka muda wanaopaswa kuutumia mahala hapo ni mchache, na anapaswa kupata kifungua kinywa kabla ya kuelekea Gasiza.

Biruse alishusha pumzi ndefu; *ohuuuuu!* Kisha akajiinua kitandani pale na kukaa. Akatazama saa yake na kugundua tayari imekwisha timu saa nne kasoro robo!

*Oh!* Bwana …Alibwabwaja; *huu muda unakimbia uatasema una miguu!* Akabwaga kite cha mfandaiko; *mchiii!*

Alifanya hayo na kushika mkonga wa simu iliyokuwa juu ya droo ya kitanda kilichokuwa pembeni yake, kisha akabonyeza namba za chumba alichokuwa Sasha. Alizipiga namba zile na kuweka mkonga sikioni. Simu iliita upande wa pili bila kupokelewa. Akapiga tena; hali ilikuwa ni ile ile; simu yaita tu.

*"Ah! Huyu naye mbona hapokei simu? Wanawake bwana! Utakuta hata anajipamba. Ama amekwenda kupata kifungua kinywa? Anakwendaje peke yake?"*Biruse alikuwa anajenga na kupangua hoja zake kana kwamba kuna fyuzi imepata changamoto kichwani mwake!

Aliurudisha ule mkonga wa simu mahala pake akaamua kujiinua. Aliposimama alichukua bastora yake kitandani akaipachika kiunoni, akapiga hatua na kuuendea mlango wake.

Aliufungua kisha akaufunga nyuma yake. Akaanza kutembea koridoni. Hatua chache mbele alikifikia chumba cha Sasha. Jambo la ajabu na lililomshitua, alikuta mlango wa chumba hicho upo wazi!

Hali hiyo ilimshitua. Ndita za uso wake zilijikusanya usoni mwake wakati akitazama kwa makini kwenye ule mlango na mapigo ya moyo wake yalianza kumwenda hobelahobela kuliko hali yake ya kawaida. Kijana huyo, alipata utashi wa kutazama kulia na kushoto katika ile korido, lakini hakuna mtu yeyote aliyemuona.

Ndipo kwa kasi ya mashine, aliichoropoa bastola yake kiunoni na kuishika mkononi. Akaanza kunyata akipiga hatua kuuelekea mlango wa chumba kile cha Sasha.

Wakati akipiga hatua hizo za tahadhari, kichwa chake hakikutulia, alikuwa akitazama kulia na kushoto na baada ya kusogea karibu zaidi na mlango, Biruse alihisi purukushani ndani ya chumba kile cha Sasha.

Hapo damu ilimchemka na kengele ya hatari ilizidi kugonga akilini mwake; akaanza kutoa pumzi kwa haraka kidogo. Biruse alipiga hesabu zake, kisha akaingia kwa kasi ndani ya chumba kile. Na ile ametokeza tu, alishitukia teke likimkumba utasema upepo wa kisulisuli. Akadondokea kitandani na bastola ikaruka upande mwingine.

Biruse baada ya kutua tu kitandani, teke lingine lilimfuata. Kama si ushapu wake teke hilo lingemsiginia hapo hapo kitandani na kwa njemba hilo lililorusha teke lilivyo refu na lilivyoshiba, kwa hakika teke hilo lingempeleka karibu na kuzimu.

Biruse alivyopinduka, alisimama haraka na kujipanga tena. Akakabiliana uso kwa uso na njemba refu mbele yake na jeusi. Lakini, pia upande mwingine alimuona Sasha akikabiliana njemba mwingine.

*Vuup!*

Akiwa anajipanga, lile njemba lilizunguka na kurusha teke, kwa bahati Biruse aliliona teke lile. Alirudisha mgongo nyuma likapita karibu mno na kidevu. Mguu ulipotua chini, jamaa yule bila kupoteza wasaa alirusha ngumi. Biruse aliinua kwa kasi mkono wake wa kushoto akaukunja kwa alama ya *'v'* na kuuziba upande wa sikio lake la kushoto. Ile ngumi iligonga katikati ya mkuno huo. Ingawa ilimtikisa Biruse lakini alipata mhimili na kusimama vizuri.

Ndipo naye alijua kurusha ngumi; jamaa alipangua kama mchezo; Biruse akarusha teke, jamaa hilo nalo likarusha teke na kukutana juu kwa juu na teke la Biruse, likawa limelipangua teke lile. Na lilivyotua tu mguu chini likarusha teke lingine. Biruse alikuwa hajajipanga vyema. Hakuliona teke hilo, jambo lililofanya teke limpate moja kwa moja na kumkumba mpaka ukutani. Akajipiga ukutani kwa nguvu na akiwa bado anajitafuta kuweza kusimama vyema, jamaa lile lililokuwa linaonekana kuwa dhahiri lina asili ya Kinyarwanda lilimsogelea kwa kasi, likarusha ngumi, Birusi alikwepa, likarusha nyingine akapangua, ya tatu ikampata shavuni.

Damu na mate vikachanganyikana na akatoa mguno wa maumivu. *Aya!* Hajakaa sawa, jamaa lile lililokuwa jepesi kwenye miguu lilifyatua teke lingine, teke hilo lilimpata Biruse usoni likamkumba na kumrusha sakafuni, akagaragara utasema kitenesi.

Biruse aligumia kwenye maumivu makali. Akajikunja na kushika mbavu zake alizopiga chini. Akiwa na maumivu mengi mwilini mwake kutokana na kichapo hicho alichopewa na jamaa lile, akigaragara hapo sakafuni, kama bahati, akaiona bastora yake iliyodondoka chini ikiwa jirani naye.

Hapo kijana huyo hakufanya ajizi, pamoja na maumivu aliyokuwa nayo, alijikakamua na kunyoosha mkono kwa kasi, kisha akaidaka ile bastora, wakati ameiweka mkononi anaiinua, jamaa lile nalo lilichomoa bastora yake kwa kasi lakini Biruse alikuwa mwepesi zaidi. Alililenga na kufyatua risasi. Risasi zile zilikwenda na kulichapa kifuani likatupwa kwa kishindo sakafuni na kudondoka

utasema gunia la viazi huku likipiga mayowe ya maumivu.

*Yalaaaaa!*

Biruse pasipo kupoteza wakati, alijigeuza na kutazama kule kwenye patashika kati ya Sasha na jamaa lingine lenye mwili na kimo cha kuendana na hili alilolisafirisha kuzimu, akaachia risasi nyingine. Risasi zile zikalitungua lile jamaa, akakisambaza kichwa chake; damu na ubongo vikachanganyikana wakati jamaa hilo likienda chini!

*Shit!*

Biruse alisema akisikilizia maumivu ya mbavu zake. Sasha ambaye alikuwa amevaa chupi pekee, kutokana na watu hao kumkuta akiwa amejipumzisha baada ya kutoka bafuni kuoga, alimsogelea Biruse na kumsaidia kuinuka pale chini alipokuwa bado amebweteka akisikilizia maumivu makali aliyokuwa anayahisi kwenye mbavu zake.

Baada ya kuinuka na kukaa kitandani; Biruse alijikuta akimuuliza Sasha ambaye alikuwa anafanya hima kuvaa nguo zake.

"Ni kina nani hawa?"

"Sifahamu!" Sasha alimjibu.

Biruse alipiga kimya kifupi na kupitisha tafakuri akilini mwake.

"Au bado ni Goma Cartel wanatufuatilia?"

"Inawezekana," Sasha alimwambia Biruse, "lakini…" akauliza akionyesha mashaka mengi usoni mwake, "ikiwa ni hao Goma Cartel, ni kina nani wanawapa taarifa juu yetu hata wanatufuatilia?"

Swali hilo lilikuwa gumu kwa Biruse. Mwanzoni walipokuwa Dar es Salaam, baada ya kufuatiliwa na almanusura kuuawa, kepteni Mwambukusi aliwaambia wasitumie mawasiliano yoyote ili kupunguza *risk* ya kufuatiliwa maana hao Goma Cartel wanamkono mrefu.

Sasa wakati huu hawatumii mawasiliano yoyote; je, hao watu wamepata wapi taarifa juu yao?

Maswali waliyojiuliza yalikuwa ni mengi mno. Hata hivyo, baada ya kuwaza, Biruse alipata mawazo:

"Nafikiri tuingie gizani moja kwa moja…" alimwambia Sasha.

Sasha alituliza mawazo na macho yake usoni mwa Biruse. Hakuwa amemuelewa mara moja alimaanisha nini kwa kauli hiyo aliyosema. Akamuuliza:

"Unamaanisha nini?"

"Tusifuate maelekezo yoyote kutoka makao makuu. Tutumie njia zetu kufanikisha misheni hii."

"Tunawezaje? Misheni yenyewe ina *code* kila hatua? Hapa tunatakiwa tukamuone Bihagarason. Tukitoka hapo twende Kongo, tukamuone Rusogotason, unafikiri hapo tunawezaje kuingia gizani?"

"Nahisi, taarifa zinavuja katikati hapa, kwa hawa watu wanaotufungulia password kuzifikia *code!* Nina wasiwasi na hawa waliotufikisha hapa, inawezekana kuna mmoja ambaye anavujisha hizi taarifa!"

Sasha hakuzungumza mara moja. Alibaki akimtazama Biruse usoni wakati mawili matatu yakipita akilini mwake. Mwishowe akamwambia: "Ni kama nimekuelewa hivi na naona ukweli kwenye hilo. Lakini, sasa tutazifikiaje *code?"*

"Tutapata njia. Lakini sasa tunajambo moja, tunachofahamu tunapaswa kwenda Gasiza. Wewe twende tukamtafute huko Bihagarason."

"Gasiza ni mji una watu laki sita na sehemu hivi… tutaanzia wapi kumtafuta."

"Tutampa wewe twende."

Sasha alilazimisha mate kupita kooni kisha akamalizia kuvaa mavazi yake. Biruse naye mwili ulikuwa umemkaa sawa, pamoja na kwamba alikuwa anasikia maumivu kwa mbali, lakini alikuwa anamudu kusimama na kusonga mbele kwenye misheni hiyo.

Alisimama na kujiweka sawa, kisha wakatoka ndani ya chumba kile cha hoteli kwa tahadhari kubwa. Walipofika nje waliishika korido, wakaambaa ambaa nayo wakaelekea mpaka nje ya hoteli ile ya Nsengiyumva!

*****

Biruse na Sasha walitembea katika mitaa ile ya Kigali, wakiitafuta stendi ambayo wangeweza kupata gari za kuelekea Gasiza.

Walikuwa wameelekezwa na mtu mmoja ambaye walimuulizia juu ya wapi wangeweza kupata gari za kuelekea huko, naye aliwaelekeza mtaa wa pili kutoka jirani na hoteli ile waliyokuwa ya Nsengiyumva.

Walipita mtaa wa kwanza, wakashika barabara ya vumbi, iliyowapeleka mpaka hapo walipokuwa wameelekezwa.

Kweli, kama walivyokuwa wameelekezwa na yule bwana ambaye kwa asili alionekana ni Mhutu, walikuta basi ndogo zilizokuwa zinaelekea huko Gasiza. Hata hivyo, kilichoonekana mtihani kwao, basi hizo zilikuwa zinauhaba wa abiria na ilikuwa ni mpaka zijae ndipo wangeweza kuianza safari ya kuelekea huko.

Wakati huo, tayari ilikuwa imekwishafika saa nne na dakika zake. Wakiongeza muda wa kukaa hapo kusubiri gari lijae, kama ni mapema sana watatoka hapo saa sita hivi. Na kutoka Kigali mpaka Gasiza ni takribani kilometa thelathini na tano (35). Mwendo wa lisaa na robo hivi kwa mwendo wa kawaida wa gari. Jambo ambalo kwa hesabu za haraka, litawafanya wafike katika mji huo majira ya mchana kuelekea alasiri.

Na hapo bado wanakazi ya kumtafuta Bihagarason na mpango wa awali ulikuwa siku iliyofuata wawe wamekwishafika Kongo, kuiwahi misheni ya siri ya mtandao wa Goma Cartel ya kuua askari wa *AU* na kumuua pia Waziri wa Madini na Nishati, Cante Mukolozi!

Hakika mazingira ya kuifanikisha misheni hiyo, pamoja na kwamba yalikuwa na ugumu wake, lakini sasa yamegeuka kuwa magumu zaidi. Na kwa hali ilivyo, kuna hatari ya Biruse na Sasha kutofanikisha jambo lolote lile katika mipango yote iliyokuwa mbele yenu!

*Nifanyenini?*

Biruse alijiuliza kwa kina.

Kila akichekecha akili yake haimpi majibu. Haoni njia nyingine ya kutafuta msaada ambao utawafanya wawe salama katika misheni hiyo.

Hata hivyo, baada ya kujiuliza kwa muda na kuwaza, kuna mawazo Biruse aliyapata.

"Napaswa nikatafute *internet café!*" alimwambia Sasha.

"Umewaza nini?"

"Nitakweleza."

"Huniachi hapa."

"Sasha inabidi ubaki ili ushike nafasi kwenye gari. Tunaweza tukatoka wotewakaja abiria wengine na tukaanza kusubiri gari upya. Sitachukua muda mrefu nitarejea."

Sasha alilazimisha mate kupita kooni kwake, kisha akaangaza kushoto na kulia kutawaza watu waliokuwa katika eneo lile, ndipo akaurudisha uso wake kwa Biruse. Akayatuliza macho usoni kwa kijana huyo ndipo akamwambia, "Poa. Uwe fasta."

"Usiwaze."

Walikubaliana. Biruse alikwenda kutafuta *internet café!*

*****

Biruse alihitaji kuwasiliana na watu wawili, kutafuta msaada. Mtu wa kwanza alikuwa ni kepteni Mwambukusi, ambaye alihitaji kumweleza yote yaliyotokea baada ya wao kufika Rwanda na mpango waliokuwa nao wa kuingia gizani.

Biruse kwa moyo wake wote, mtu pekee anayemuamini ni huyo kepteni Mwambukusi. Anauhakika ni mtu mwaminifu na pengine kwa kumweleza juu ya maamuzi aliyoamua kuyachukua; atakuwa na mawazo ya kuongezea hata kuwasaidia kusonga mbele pasipo kupoteza muda katika kutekeleza misheni hiyo. Maana kuchelewa kwao kwa namna yoyote ile kufika Kongo, kulimaanisha kifo cha waziri Cante Mukolozi na askari wengi wa jeshi la kulinda amani la Umoja wa Nchi za Afrika *(AU)*.

Mtu wa pili aliyehitaji kuwasiliana naye, ni mpenzi wake Zinaeda. Biruse anaamini huu ulikuwa ni wakati wa kuzichanga karata zake vyema. Pamoja na kwamba, alikuwa anamuamini kepteni Mwambukusi, lakini alipaswa kuwa na mbadala ikiwa mambo hayatakwenda kama vile ambavyo anataka yawe. Kwahiyo, aliwaza, kuzungumza na Zinaeda na kumweleza kinagaubaga juu ya misheni hiyo ya siri na kuona namna gani ambavyo, binti huyo, mtoto wa afisa wa *KGB,* anaweza kumsaidia ikiwa ni hata kumuunganisha na baba yake, maana Biruse anafahamu kuwa, *KGB,* wanamkono mrefu unaofika kila mahala duniani.

Na njia pekee ambayo Biruse, alikuwa anaimani nayo kwamba ni njia salama kwa ajili ya kuwasiliana habari nyeti kama hizo, ilikuwa ni kupitia *e-mail.*

Baada ya kutoka pale stendi, aliswampa mtaani na kuulizia wapi atapata huduma ya intaneti. Baada ya kuzunguka akiuliza hapa na pale, hatimaye aliweza kuonyeshwa sehemu ambayo angepata huduma ile aliyokuwa anaihitaji.

Biruse alikaa na kulipia muda wa nusu saa kisha akafungua *waptrick,* akaenda moja kwa moja kwenye ukurasa wake wa *yahoo,* akamuandikia *e-mail,* kepteni Mwambukusi pamoja na Zinaeda.

Dakika kumi baadaye kepteni Mwambukusi alimjibu *e-mail* yake. Kepteni huyo, alionyesha kushangazwa mno na taarifa hizo ambazo Biruse alimpelekea.

Akamwandikia kuwa:

‘Ni mawazo mazuri mliyopata ya kuingia gizani. Nawaunga mkono. Lakini, nimeanza kuona shida inatokea wapi! Wala si kwa hao wanausalama wa chini kama unavyodhani. Goma Cartel ni watu wenye status ya juu, hawawezi ku-deal moja kwa moja na dagaa. Wao wana-deal na samaki, ila ninachohisi hao samaki ndio wana-deal na dagaa!

*“Kwahiyo, kutakuwa kwa vyovyote vile, kuna kigogo mmoja kati yetu ambaye anahusika na uvujishaji wa hizi taarifa! Huyo akibainika kila kitu kitakuwa sawa.*

*"Sasa, chukua hii code; ukifika Gasize kuna msikiti mkubwa pale unaitwa Msikiti wa Sekhe Suyed Bin Soyee. Ulizia mtu anaitwa Alhadj Jumbe Ndaizeye. Huyo atakufikisha kwa Bihagarason. Na hapo utapata kodi inayofuata. Huku mimi ninafanyia kazi kumfahamu mvujishaji.'*

Kusikia kutoka kwa kepteni Mwambukusi, kulimfariji mno Biruse. Uhai juu ya kukamilisha misheni ile ulimrejea. Kijana akavuta hewa nyingi ndani zikajaa kifuani na akazishusha kwa mkupuo mmoja. *Uhuuuuu!* Matumaini tele yalifurika moyoni.

Hata hivyo, kwa upande wa Zinaeda, mpaka muda wa nusu saa aliolipia kupata huduma ile ya mtandano unamalizika, hakuwa amesikia kutoka kwake. Kulingana na muda na yote aliyokuwa nayo mbele yake, Biruse hakuhitaji kuongeza tena malipo kwa ajili ya kusubiri kusikia kutoka kwa Zinaeda, aliamua kupiga moyo konde na kuiachia siti ile.

Biruse aliamua kutoka ndani na chumba kile kulipokuwa kunapatikana huduma ile ya mtandao wa intaneti, akajitosa mtaani na kupiga hatua moja-moja kuelekea kule stendi alikomuacha Sasha.

Akitembea, alikuwa anawaza namna mabavyo atakwenda kumkabili huyo mtu ambaye ameelekezwa na kepteni Mwambukusi, aitwaye Alhadj Jumbe Ndaizeye, ambaye ndiye angewafikisha kwa Bihagarason.

Biruse alizidi kutembea. Alipofika maeneo ya stendi, alishangazwa na kundi la watu waliojikusanya katika eneo ambalo kwa kumbukumbu zake ndipo lilipokuwa lile gari lililokuwa linasubiri wasafiri wa Gasiza.

*Hee!*

Biruse alishituka na kutoa macho. Moyo ukaanza kumwenda mbiombio. Akajiuliza kuna nini tena kinatokea hapo! Akili yake ilichekecha na kuchakata, na kuna upande ulimweleza kuwa tayari kumekucha. Huenda ni watu wa Goma Cartel wamekwisha inuka

kufanya yao!

Mawazo hayo, yalimfanya azidi kuwa na hofu zaidi na zaidi. Hawa washenzi! Lakini, akiwaza hayo, alijiuliza; ikiwa ni watu wa Goma Cartel, wamepataje taarifa kuhusu wao? Mbona ni kana kwamba wanaendeshwa na nguvu za giza! Tuseme mapepo ya utambuzi! Biruse alijiuliza maswali huku akianza kuhisi hisia za hasira zikimvagaa kichwani mwake. Hata hivyo, hakupata majibu ya maswali yale aliyokuwa anajiuliza.

Akipiga hesabu zake za kawaida, kwa waliyoyafanya kwenye hoteli ile ya Nsengiyumva, hatimaye wakatokomea na kuishia hapo walipo, akijiuliza ni nani ambaye anaweza kunusa mahala walipo na kwa namna gani amenusa, haimuingii akilini asilani!

Kwamba, ama mtu aliwafuatilia toka pale hotelini au amepewa taarifa na nani? *Kepteni Mwambukusi?* Lakini akiwaza, anagundua hakumweleza kepteni huyo wapi alikuwa zaidi ya kumweleza kuwa wapo wanatafuta gari ya kuelekea Gasiza!

Lakini hata muda aliowasiliana nao, hata ikiwa ni kusema alimweleza wapi walikuwa, ni mchache sana kwa yeye kuwasiliana na watu hata wamvae Sasha mahali hapo stendi.

Sasa, swali likabaki palepale; nini kinaendelea kwenye ulimwengu huu wa kijasusi? Kweli Biruse alikuwa anajionea mauzauza!

Bila kupoteza wakati akiwa mwenye tahadhari kubwa, mkono mmoja ukiwa jirani na eneo alipokuwa ameichimbia bastola yake, alipiga hatua kuelekea kwenye lile kundi. Akaanza kuwapangua watu kuelekea katikati kuona nini kilikuwa kinajiri maeneo yale na kuona ikiwa atamuona mshirika mwenza Sasha.

*Kha!*

Alishangazwa na alichokikuta. Dereva wa gari lile, ambalo lilitarajia kuwapeleka Gasiza, alikuwa ameshikiana mtutu wa bunduki na mtu mwingine na kilichoonekana yule dereva alikuwa na asili ya Kitusi na yule jamaa mwingine alikuwa na asili ya Kihutu; walikuwa wametibuana na wanataka kumwagana matumbo chini!

Biruse, baada ya kugundua kasheshe lile lilikuwa halihusiani na

yeye pamoja na Sasha na wala si watu wa Goma Cartel, alijikuta akishusha pumzi ndefu. Akapata ahueni kutokana na ile hofu ambayo ilikuwa imemshika moyoni. Na alichofanya ni kuangaza katikati ya wale watu na kumtafuta Sasha. Hatimaye alimuona.

"Sasha!"

"Biruse."

"Nini kinatokea hapa?"

*"Ah!* Siunajua hawa watu!"

"Mambo yao ya kikabila siyo?"

*"Yes!* Huyo Mhutu naye ni dereva wa gari, kamweleza huyo mwenzake amekwishajaza abiria aondoke, huyu naye anasema bado abilia wawili ambao watakaa kwenye eneo la nyuma ya gari kwenye buti."

"Kipi kikawagombanisha sasa hapo?"

*"Ah!* Naona kuna mmoja anatamani kujaza zaidi na mwingine anaona anachelewa kujaza."

*"Duh!"*

"Ndiyo hivyo, halafu *loh*, kila mtu ana mtutu wa bunduki mazee."

"Hii ni Rwanda *girl,* hapa si Bongo!" Biruse alisema akitabasamu!

*"Ha! Haa!* Wala si Kenya."

"Tuwe makini kwakweli."

"Makini haswa."

"Unajua nilivyofika na kukuta hii hali, ilinipa hofu, nikawafikiria wale washenzi."

"Washenzi gani? Goma Cartel?

*"Naam!"*

*"Ha! Ha! Haaa!* Uoga huo."

"Siyo uoga ni tahadhari."

Hahahaa! Walicheka.

*"Enhee*… nambie, ulikwenda kuwasiliana na nani huko?" Sasha alimuuliza Biruse.

Biruse naye alimsimulia kila kitu juu ya mawasiliano yake aliyoyafanya na mtu aliyeelekezwa kwake; *Alhadj Jumbe Ndaizeye.*

Vurumai lile hatimaye liliweza kupoa baada ya watu wanaowafahamu wale jamaa walioshikiana mitutu ya bunduki kuingilia kati. Na baada ya vurumai kupoa, abiria waliingia kwenye gari lile na walipotoshea safari ya kuelekea Gasiza ilianza mara moja.

# 11

## *Gasiza*

“Nyie ni kina nani?” Mtu mmoja wa umri wa makamo, mrefu na mwembamba; mweusi kwa ngozi ya mwili wake na pua yake ililalia mbele utasema mgogo wa panzi, aliwauliza kina Biruse.

Huyo mtu jina lake aliitwa Kessy Butare. Alikuwa ni miongoni mwa viongozi wa msikiti wa Sekhe Suyed Bin Soyee. Msikiti ambao Biruse alielekezwa na kepteni Mwambukusi, afike hapo na kumuulizia mtu aitwaye Alhadj Jumbe Ndaizeye.

Kessy muda mwingi yupo msikitini hapo kwa ajili ya masuala ya ibada na kuhudumia watu kutokana na mahitaji mbalimbali waliyokuwa wanahitaji kutoka msikitini hapo.

“Sisi ni wageni wake, ukimweleza hivyo inatosha.” Biruse alimjibu Kessy.

Kessy alimtazama Biruse kwa sekunde kadhaa kana kwamba alikuwa anasaili jambo fulani kutoka kwake. Baada ya ukimya wa muda mfupi, alijenga tabasamu hafifu ambalo wawili wale hawakufahamu maana yake, lakini mwishowe alimwambia: “Nisubirini.”

Kisha aliinuka mahala pale alipokuwa amekaa nao, katika eneo la mapumziko msikitini hapo. Akapiga hatua na kuelekea ndani kabisa ya msikiti. Baada ya muda walimuona akirejea huku katika mkono wake mmoja akiwa ameshika birika, mwingine vikombe vitatu vidogo vya udongo!

“Karibuni bakshishi kidogo,” Kessy alisema akiwapa vikombe Biruse na Sasha, kila mmoja cha kwake, naye akabaki na kimoja mkononi.

Wawili wale walitazamana kwa macho ya pembeni, lakini hawakuweza kuzungumza lolote lile. Hata hivyo, ni kana kwamba macho yao yalizungumza maana kwa namna walivyotazamana kuna ujumbe walifikishiana; *kuwa makini!*

Kessy aliwamiminia chai. Kisha akamimina naye kwenye kikombe chake na ndipo akaketi akiunganisha miguu hata kutengeneza namba iliyosomeka nne.

"Mtamsubiri Alhadj, nimekwisha wasiliana naye kwa njia ya simu," bwana yule aliwaambia, "baada ya lisaa hivi atakuwa amefika," aliongeza.

Biruse na Sasha, walitikisa kichwa kuonyesha kwamba walikubaliana naye. Ingawa katika uhalisia muda wa lisaa ulikuwa mkubwa mno kwao ukilinganisha na muda waliokuwa wamesaliwa nao katika kukamilisha misheni ile. Lakini hawakuwa na budi kusubiria maana hakukuwa na namna ya kulazimisha juu ya jambo hilo.

Basi, dakika ziliyoyoma wakifanya mazungumzo ya hapa na pale. Wakiulizia hali ya hewa ya Gasiza, uti wa mgongo wa uchumi wake, kuhusiana na kilimo pamoja na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe bila kusahau vikundi vya waasi.

Mambo waliyozungumzia yalikuwa ni mengi. Na wakiendelea na mazungumzo hayo, ukiwa umepita muda kitambo tangu wawe mahali hapo, ikiwa ni kabla ya kufika muda ule ambao Kessy aliwaeleza kina Biruse kwamba watamsubiri Alhadj Jumbe Ndaizeye, kuna gari *Landrover 110,* iliingia msikitini hapo.

"Alhadj Jumbe Ndaizeye," Kessy alijikuta akisema na kina Biruse walirusha macho yao kulitazama lile gari pasipo kuzungumza neno lolote lile.

"Zaidi ya miaka ishirini sasa anamiliki hiyo gari, anavyoitunza utasema ameinunua jana." Kessy alisema akisimama.

Wakati huo naye Alhadj Jumbe Ndaizeye, alikuwa ameteremka kwenye gari yake na akaanza kupiga hatua kuelekea kule walipokuwa kina Biruse na mwenyeji wao.

Alipowakabili, aliwasabahi na kuwakaribisha kisha akawachukua faragha kina Biruse kwa ajili ya kufanya mazungumzo nao.

Walijitambulisha na kumtambulisha mtu aliyewaelekeza kwake, naye akajitambulisha kwao kama mtu wa usalama ambaye amejikita katika eneo hilo kwa miaka mingi. Na kepteni Mwambukusi ni mkuu wake wa kazi ambaye wanaheshimiana na wamefanya kazi pamoja za kiusalama kwa miaka mingi.

"Biruse," hatimaye Alhadj Jumbe Ndaizeye, aliita, hapo akachezesha kichwa kwa nukta kadhaa akamtazama pia yule mwanadada ambaye alikuwa amekaa pamoja na yule kijana, naye akamuita jina lake, "Sasha," Alhadj Jumbe Ndaizeye, alikuwa akizungumza kwa utulivu sana..

"Ninavyowatazama mbele yangu inanijia picha ya wazazi wenu, comred Othuman Seyunguson na yule mwanamama simba jike, Farida. *Tse!* Maisha haya," Alhadj Jumbe Ndaizeye, alizungumza kwa mfadhaiko na kurudisha mgongo nyuma akaegemea kwenye kiti kile alichokuwa amekikalia.

"Ardhi imemeza watu wema wengi na mashujaa. Hawa nao wamekwenda wana wa kwenda," Alhadj Jumbe Ndaizeye, alisema na kupiga kimya kifupi. Kisha baada ya kulazimisha mate kupita kooni aliendelea kuzungumza: "Wakati wazazi wenu wanafanya makubwa waliyoyafanya sisi ndiyo tulikuwa makinda na watu ambao tulikuwa tunawatazama kama vielelezo. *Comred* Seyunguson katika masuala haya ya kikachero alikuwa ni mwalimu mzuri. Nami nilijifunza kwake pamoja na rafiki zake kina Bihagarason na Rusogotason

"Nakumbuka *comred* alikuwa na misemo yake," Alhadj Jumbe Ndaizeye, alijenga tabasamu hafifu, akarusha macho yake mbali akayatuliza huko kwenye anga lisilo na mwisho. Macho yake yakiwa yametulia huko, alitalii kwenye kumbukumbu za muda, mahali na nafasi. Akakumbuka mengi. Yakamjia kama mkanda wa filamu na kujipekua yote. Yakaamsha hisia zake na kuziteka. Yakasukuma uchungu moyoni mwake. Akalazimisha mate kupita

kooni mana haakutaka zile hisia zilete matokeo machoni mwake.

*Machozi!*

Hapana. Hakutaka yamwagike mbele ya vijana hawa. Watoto wake haswa. Kwa umri wao aliwazaa na kwenye kazi yao, alikuwa sawa na baba pia.

Kwahiyo, Alhadj Jumbe Ndaizeye, alikabiliana na hisia pamoja na maumivu hayo kwa kuyatoa macho yake huko alikokuwa ameyarusha akayapepesea pembeni na kuyarudisha kwa kina Biruse, akayasambaza na kuwatazama kwa chati, ndipo akaendelea kuongea, *"comred* alipenda kusema: Jasusi hatakiwi kulala mahala asipopafahamu, bora alale porini, endapo atakosa mahala anapopaamini.

"Pia alitufundisha kuwa; Jasusi hata akichoka hapaswi kulala ikiwa yupo kwenye hatari kwani muda ambao analala adui zake ndiyo wanaamka. Lakini vilevile, alitweleza, jasusi hapaswi kutembea bila *scanner* ya *hidden cameras* kila mara anapokuwa kwenye misheni. Kwa kweli mafunzo ni mengi nikisema nisimulie yote niliyojifunza kutoka kwake hatuwezi kumaliza."

Biruse na Sasha walijikuta wakishusha pumzi fupi, kutokana na yale yote waliyokuwa wanayasikia kuhusu wazazi wao na hasa huyu mwamba Othuman Seyunguson. Na wakiwa bado hawajazungumza jambo lolote lile, Alhadj Jumbe Ndaizeye, aliuinua mgongo wake kutoka kwenye kiti kile alichokuwa amekalia kisha akasema: *"anyways..."* akaendelea, "sasa turudi kwenye jambo lenu…" alisema akiwatazama usoni kwa macho ya moja kwa moja, "Bihagarason," aliongeza akinena taratibu.

Kina Biruse hawakuyatoa macho usoni kwake. Walitulia wakisubiri nini kitafuata baada ya Alhadj Jumbe Ndaizeye, kulitaja jina lile.

"Sijui kama atakuwa msaada kwa sasa!" Hatimaye alisema kwa mashaka.

"Kwanini?" Sasha aliuliza haraka.

Alhadj Jumbe Ndaizeye, alirudisha mgongo wake kwenye kifua

cha kile kiti alichokuwa amekikalia. Ndipo akasema taratibu; “Ni mgonjwa sana.”

*“Hee!”* Biruse alihamanika.

*“Yes,”* Alhadj Jumbe Ndaizeye, alisema kwa kusisitiza, “naona muda wake wa kwenda kukaa pamoja na baba na baba wa baba zake umewadia.”

“Anaumwa nini?” Sasha alizidi kuchimba.

“Kiharusi.”

*Jesus!*

Sasha alisema kwa hamaniko na ukimya mfupi ulifuata kati yao, na mwishowe, ukimya huo uliondolewa na Alhadj Jumbe Ndaizeye, aliyewaeleza kina Biruse na Sasha kwamba, hata hivyo, kikubwa zaidi ya yote ni kwenda kumuona.

Walikubaliana hivyo, wakainuka na kuliendelea *Landlover* la Alhadj Jumbe Ndaizeye.

*****

Bihagarason, ni miongoni mwa mashujaa wenye historia ndefu kwenye uwanda wa kijasusi katika bara la Afrika.

Sifa na utukufu wake, alivijenga kwa jasho, damu, machozi pamoja na nidhamu aliyoitumia katika maisha yake ya kikachero kwa miaka yote aliyojihusisha na kitengo hicho.

Pamoja na kwamba, kwa asili yeye ni Mnyarwanda, lakini amebahatika kufanya kazi katika nchi nyingi za bara la Afrika hasa Tanzania, na katika utendaji wake wa kazi enzi hizo za utukufu wake, washirika wake wakubwa walikuwa ni Seyunguson na Rusogotason.

Mbali na kushirikiana katika kazi, hawa ndugu watatu, ujamaa wao ulifikia hatua ya kuvuka mipaka na kuwa sawa na udugu. Na kuonyesha walivyoshibana, marehemu Othuman Seyunguson, alivyopata mtoto wa kiume na wa pekee, Biruse, alimpa jina kwa kuchukua herufi za mwanzo kutoka kwenye majina yake pamoja na rafiki zake hao. Bi – akimuenzi Bihagarason, Ru – Rusogotason na

Se – akiwa ni yeye mwenyewe Seyunguson.

Miaka ilipita na miaka ikarudi, sasa ni miaka na mikaka tangu Seyunguson awatoke. Hata hivyo, kwa upande wake pia Bihagarason, alikuwa kwenye saa zake za jioni maana jua la maisha yake kwa sasa laelekea mawio. Lakini pia, afya yake haikuwa timamu. Ni takribani miezi sita sasa toka afikwe na maradhi ya kiharusi na alikuwa akiendelea na matibabu.

Pamoja na hivyo, umri kumtupa mkono, afya kuzorota, bado Bihagarason, alipopata wasaa aliwasiliana na makachero wenzake aliofahamiana nao kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali juu za yale yanayoendelea kwenye ulimwengu huo wa kikachero, lakini pia kutoa msaada kutokana na uzoefu aliokuwa nao pamoja na imani iliyojengwa kwake.

*****

Alhadj Jumbe Ndaizeye, Biruse na Sasha walikaribishwa sebuleni nyumbani kwa Bihagarason na mkewe aitwaye Ingabire. Ilikuwa ni katika jumba mithili ya kasiri, lililojikita kwenye eneo tulivu lililozungukwa na miti mingi. Na baada ya kufahamiana, Alhadj Jumbe Ndaizeye, alieleza shida iliyowafikisha nyumbani pale.

Katika namna ambayo hawakuitarajia baada ya kueleza shida yao, walimwona mwanamama huyo, akizungusha kichwa kwa namna ya kusikitika ama kupoteza matumaini.

Waliyatuliza macho yao usoni kwake kusikia angesema nini! Yule mwanamke alishusha pumzi na kuwaambia:

“Mume wangu hawezi kuwa msaada kwenu kwa sasa!”

Nyuso zao zilisawajika na wakachezesha vichwa kutazamana.

*Hawezi kuwa msaada kwetu kwa sasa?*

Maneno hayo yalijirudia akilini mwa Biruse na akajikuta akikumbuka juu ya mazungumzo yao na Alhadj Jumbe Ndaizeye, walipomweleza nia yao ya kumuona Bihagarason. Hapo alipata utashi wa kumuuliza yule mama mwenye umri wa uzee pia, lakini mwenye mwili ulionekana kuwa na nguvu. Bado anadai, dongo

lake lilikuwa zuri mfano wa chuma cha Mjerumani,; huyu mama asemapo juu ya umri wake watu hubaki vinywa wazi. Umri na mwili haviendani kabisa.

"Kwanini hawezi kuwa msaada kwetu?"

"Ni mgonjwa sana," yule mama alijibu akizungumza taratibu. "Lakini pia," aliongeza, "hayupo hapa, alfajiri ya leo amesafirishwa kwenda India kwa ajili ya matibabu."

Biruse na Sasha walichoka mwili mpaka moyo. Taarifa hizo kwao zilikuwa ni ngumu kumeza. Misheni iliyokuwa mbele yao ilikuwa na *code* nyingi, ambapo katika kila *code* ndipo kulikuwa kuna mwanga wa hatua nyingine inayofuata katika kukamilisha misheni hiyo. Na bila hivyo, ilikuwa ni jambo gumu sana kukabiliana na mtandao ule wa Goma Cartel. Lakini mbali na hivyo, hiyo ni misheni iliyokuwa na saa maalumu za kutakiwa ikamilike. Tofauti na hivyo kuna maafa makubwa yanakwenda kutokea. Sasa vikwazo vilivyotanda kwenye misheni hiyo, ukilinganisha na muda uliobakia, ilikuwa ni sawa na kufananisha ardhi na mbingu!

Biruse alishusha pumzi fupi, akimtazama yule mama kana kwamba alikuwa anahitaji hurma yake katika yale yote yaliyokuwa yanatokea. Kisha akajikuta akimuuliza:

"Hakuna ujumbe wowote aliouacha?"

Yule mama hakujibu mara moja. Akimtazama Biruse, alifinya uso wake kitendo kilichofanya atengeneza ndita kadhaa usoni. Ndipo kana kwamba alikuwa amekumbuka jambo alisema; "oh, nimekumbuka!" akainuka, "kuna jina la mtu na jina la eneo ameandika kwenye kitabu chake cha kumbukumbu na aliniambia ikiwa hata rudi akiwa hai, hayo majina kuna watu siku moja watafika wakiyahitaji. Na kati ya majina ya watu aliosema watafika, moja wapo nimelisikia kati yenu. Biruse."

Hapo kina Biruse walitazama tena.

"Ngoja nije," yule mama alisema na kuanza kupiga hatua kutoka sebuleni pale, akalifuata korido na kuelekea chumbani kwake.

Baada ya takribani dakika nne alirejea huku mkononi ameshika

kipande cha karatasi ambacho alimkabidhi Alhadj Jumbe Ndaizeye.

Alhadj Jumbe Ndaizeye, alikisoma kile kipande cha karatasi: *Nsaku Mboya, Barumbu, Kinshasa. Bokkasa Avenue,* halafu mbele yake kulikuwa na mshale umechorwa kisha likaandikwa jina *Rusogotason!*

Kutokana na uzowefu ambao Alhadj Jumbe Ndaizeye, alikuwa nao kwenye kazi hizo za kikachero aliweza kuelewa ule ujumbe ulikuwa unamaana gani. Ilikuwa ni kwamba, Bihagarason aliwaelekeza kwa huyo mtu aitwaye Nsaku Mboya, kuwa watampata katika mji wa Barumbu, Kinshasa katika mtaa wa Bokkasa naye atawafikisha kwa Rusogotason.

Jambo hilo, lilimfahamisha kutambua kwamba, Bihagarason alikuwa na maelekezo juu ya misheni hiyo na alifahamu kwamba yeye ni sehemu ya msaada wa kuikamilisha na alitarajia ujio wa wanausalama wenzake siku moja.

Na mbali na hivyo, Alhadj Jumbe Ndaizeye, anafahamu hakuna mtu mwingine ambaye angefuatwa juu ya habari za Rusogotason. Kwa kumbukumbu zake anakumbuka mwamba huyo aliingia gizani miaka mingi iliyopita na habari zake zilikuwa ni nadra mno kuzipata na alikuwa akishiriki misheni za siri mno zilizotambuliwa na viongozi wa juu tu wa idara za usalama Afrika. Maisha yake na familia yake yalikuwa ni siri kwelikweli. Na hiyo yote ilitokana na Rusogotason, kushiriki kwenye misheni ya kuuondoa madarakani utawala wa kijeshi wa *FRODEBU,* baada ya mauaji ya aliyekuwa rais wa kwanza wa Burundi aliyechaguliwa kidemokrasia, Melchior Ndadaye.

Toka hapo kwa muda mrefu vikundi mbalimbali vya Watusi vimekuwa vikimtafuta kwa ajili ya kumuua ili kulipiza kisasi kwa yale aliyowatendea!

Hata hivyo, kwa upande wa Alhadj Jumbe Ndaizeye, jambo hilo la ushiriki wa Rusogotason, lilimfariji moyoni mwake na kiukweli aliona fahari ya kazi hiyo ya usalama waliyokuwa wanaifanya. Aliona ni kazi ambayo ukiibeba moyoni basi utaifanya kwa upendo.

Na upendo ulikuwa ni kila kitu katika kazi hiyo kwa sababu misheni moja wakati mwingine ni kama *patten* kubwa ambayo haiwezi kukamilika bila kuunganisha vipande kutoka huku na kule. Na jambo lililompa faraja zaidi ni namna ambavyo *pattern* hizo zilikuwa zikilindwa, kwasababu ili kufanikisha kazi ya usalama kila *patten* ilikuwa na umuhimu mkubwa.

Na huo upendo aliuona hapo kwa Rusogotason. Pamoja na kwamba alikuwa katika wakati mgumu mno wa kupambana na maradhi yaliyokuwa yanamkabili lakini mkono wake walikuwa nao katika misheni hiyo. Jambo hilo lilimfariji sana Alhadj Jumbe Ndaizeye.

Basi, baada ya kuupata ujumbe ule, Alhadj Jumbe Ndaizeye, hakutaka waendelee kupoteza muda katika makazi yale, alimshukuru yule mama, mke wa Bihagarason na akamtamkia kalima za heri kwa ajili ya mumewe kisha akaaga ili wao waweze kutoka.

Huyo mama naye aliwatakia kila lenye heri, wakatoka nyumbani hapo!

# 12

*Dar es Salaam, Tanzania*

Kwa upande wa kepteni Mwambukusi, kichwa chake kiliwaka moto. Katika maisha yake yote akifanya kazi katika vitengo mbalimbali vya usalama, anakili amewahi kukutana ama kuongoza misheni ngumu, lakini misheni hii aliyokuwa anaisimamia mbali na ugumu wake ilikuwa ni misheni ya tofauti sana.

Na utofauti wake ulikuwa ni kwamba; kutokana na unyeti wa misheni hiyo na kuvuja kwa taarifa zake, ulikuwa umefika wasaa ambao anajikuta haliamini jopo la viongozi wa ngazi za juu wa vikosi vya ulinzi na usalama.

Kila ambapo kepteni Mwambukusi alikuwa akijiuliza, taarifa za misheni hiyo, zinawezaje kuvuja hapati majibu sahihi, zaidi ya kuona wazi kuwa taarifa hizo zilikuwa zikivuja kutoka katika kundi hilo la viongozi, jambo lililomaanisha kuwa kuna kiongozi miongoni mwao au viongozi wanashirikiana kwa namna moja ama nyingine na mtandao wa Goma Cartel.

Lakini huyo kiongozi au hao viongozi ni kina nani? Hilo ndilo lilikuwa swali la kumpasua kichwa! Kepteni Mwambukusi aliwajaza wakuu hao wa vikosi kwenye akili yake na kuwatafakari, lakini bado ilikuwa ni ngumu kubaini maana kila mmoja alionekana kuwa mwaminifu kwelikweli.

Hapo kepteni Mwambukusi alifahamu kuna jitihada za dhati ambazo anapaswa kuzifanya ili kubaini ukweli.

Majira ya jioni siku hiyo, wakati kina Biruse na Sasha wakiwa Gasiza, kepteni Mwambukusi alijipanga kufanya jambo moja la hatari lakini ambalo aliwaza kuwa pengine litamsaidia katika

harakati zake za kumbaini mvujishaji wa habari.

Kepteni Mwambukusi jioni hiyo, baada ya kurudi nyumbani kwake akitoka kazini, alioga na kutupia mwilini mwake *tracksuit* nyeusi, kofia nyuesi ya soksi, mikononi alivaa gloves nyeusi za mpira na miguuni alitupia *sneaker* nyeusi zenye urembo mweupe.

Wakati anatoka chumbani alikutana na mkewe Tusekile.

"Hallow…" mkewe alisema kwa hali ya mshangao akimsaili kwa macho kuanzia juu mpaka chini. Hajamuona akiwa kwenye mavazi ya namna hiyo kwa kipindi kirefu. Na ameingia tu sasa anataka kutoka. Hali ya udadisi ilimshika.

"Hello honey…"

"Vipi?"

"Safi."

"Mbona hivi?"

*"Ah!* Naenda kwenye *work-out* kidogo?"

"Upo salama lakini?"

*"Yes baby, why?"*

"Sijakuona namna hii muda mrefu, unanipa mashaka."

*"Relux* baby nipo vizuri." Kepteni Mwambukusi alimsogelea mkewe na kumbusu kwenye paji la uso wake, kisha akamuaga na kutoka ndani ya jumba lake.

Mwanaume huyo, pasipo kuyajali mashaka ya mkewe aliyemuacha akimsindikiza kwa macho yaliyojawa udadisi, moja kwa moja alielekea mpaka eneo la maegesho ya gari na kuingia ndani ya gari yake aina ya Prado. Akatekenya ufunguo na kutoka nyumbani kwake hapo mitaa ya Ununio.

Baada ya kuendesha gari kwa mwendo wa takribani kilometa moja, aliishika njia ya vumbi iliyokuwa inatokea katika kituo cha daladala cha Basihaya. Hapo akaingia kwenye barabara ya Bagamayo, akakanyaga kibati cha mafuta akielekea uelekeo wa Mapinga, lakini kabla hajafika mbali, baada ya mwendo mfupi wa dakika chache, alipofika kwenye kituo cha daladala cha Namanga, kepteni Mwambukusi aliingia mkono wake wa kulia na kushika njia

ya vumbi, akaelekea moja kwa moja mpaka mtaa mmoja uitwao *Second Chance!*

*Second Chance* ni mtaa uliotulia na umejengeka kwa kupangika vyema. Baadhi ya watu wanaoishi katika eneo la mtaa huo ni viongozi wa serikali, wafanyabiashara na wafanyakazi mbalimbali wa taasisi zilizotoa mishahara minono. Kwa lugha nyingine tuseme, mtaa huo haukuwa wa watu hohehahe!

Na katika mtaa huo, ndipo alipokuwa anaishi mkurugenzi wa idara ya usalama, Kamishina Marwa Warioba.

Kepteni Mwambukusi alikwenda na kuegesha gari yake mita takribani mia tano kutoka nyumbani kwa Kamishina Marwa Warioba, kisha akabakia hapo ametulia kwa dakika kadhaa akitafakari jambo. Baada ya kuzama kwenye fikra zake kwa kina, mwisho kepteni Mwambukusi alitoa bastora yake alipokuwa ameichimbia kwenye moja ya droo zilizokuwa kwenye *dashboard,* akaikoki ile bastora na kuisondeka kiunoni mwake.

Kepteni huyo, alichukua simu pembeni ya mahala pale alipokuwa amekaa kwenye kiti cha dereva, akapangusa na kuitafuta namba ya kamishina, kisha aliipigia:

Simu iliita upande wa pili na mwishowe ilipokelewa.

"Kepteni," kamishina Marwa ailiitika.

"Kamishina," kepteni Mwambukusi alizungumza kwa sauti iliyonyongea mno.

"Habari gani huko ndugu, mbona umepoa sana?"

*"Aah!* Mambo ni mengi kamishina."

"Unamaswahibu gani ndugu? Ama shemeji amekwisha korofisha mambo huko nyumbani, maana wake zetu hawa hawapoi!"

*"Ha! Ha! Haaa!"* Kepteni Mwambukusi alijilazimisha kuangua kicheko cha uongo na kweli ilihali hakuwa na hali yoyote ambayo ingemsukuma kucheka.

"Hapana. Sina maswaibu yoyote ila nahitaji kukuona kamishina kama inawezekana." Mwishowe kepteni Mwambukusi alimwambia kamishina Marwa.

Kamishina Marwa alifinya uso wake kitendo kilichofanya ndita kadhaa zijitengeneze usoni: “Unahitaji kuniona?” Akauliza kwa kishindo chenye hofu ndani yake.

“Ndio.”

“Kuna nini kepteni?”

“Nina mazungumzo muhimu sana nawe kamishina.”

Kamishina Marwa alipiga kimya kifupi. Alitafakari kwa sekunde kadhaa, mwishowe akauliza kwa sauti iliyokwaruza: “Na unahitaji kuniona lini?”

“Leo, muda huu?”

“Muda huu?”

“Ndio kamishina.”

“Kepteni una uhakika kila kitu kipo sawa?”

“Ndio kamishina, ni mambo fulani tu hivi ninahitaji kukweleza, tafadhali naomba tuonane!”

“Sasa mimi nipo nyumbani muda huu, itakuwa ni ngumu kutoka? Labda uje nyumbani kwangu tutakaa uani na kuzungumza!”

“Sipo mbali na nyumbani kwako kamishina. Nimeegesha gari takribani mita mia tano kutoka lilipo jumba lako. Nipo hapa kwenye kiwanja hiki chenye mitimiti!”

Kamishina Marwa alijikuta akipiga hatua mpaka dirishani na kufunua pazia ili aweze kuona nje. Kiuhalisia nyumba ya kamishina Marwa ni ya ghorofa. Mtu akiwa ndani, haswa kwenye chumba chake alichotumia kulala na mkewe, akitazama kupitia dirishani alikuwa na uwezo wa kutazama eneo kubwa la nje.

Kwahiyo, alipotazama nje, aliweza kuliona gari la kepteni Mwambukusi, kwenye uwanja wa bwana mmoja, jirani yake, ambao haukuwa umejengwa, lakini ulipandwa miti mingi ya Mwarobaini.

“Sasa kwanini usije nyumbani?” kamishina Marwa alimuuliza kepteni Mwambukusi.

“Hapana kepteni, mazungumzo haya ni nyeti mno, nakuomba tafadhali uje hapa.”

Kamishina Marwa na kepteni Mwambukusi wamefanya kazi

pamoja kwa kipindi kirefu mno. Ni zaidi ya miaka kumi na tano toka wafahamiane na wameshirikiana kwenye mambo mengi mbali na yale yaliyowaunganisha na kazi.

Kimsingi kutokana na kufahamiana kwao kwa muda mrefu, wito wa kepteni Mwambukusi haukumfanya kamishina Marwa ahofie juu ya usalama wake, lakini pia kwa nafasi aliyonayo katika kitengo cha usalama, kwa protoko za kitengo hicho, kamishina Marwa alikuwa na wanausalama wanaohakikisha yupo salama muda wote kwa kuwa naye bega kwa bega. Kwahiyo, kamishina Marwa jambo pekee alilokuwa anahofu nalo, lilikuwa ni juu ya nini kimetokea ama kimempata kepteni Mwambukusi hata anahitaji kumuona muda huo!

Basi kamishina aliafikiana na kepteni Mwambukusi kwamba anatoka ndani ya jumba lake. Na baada ya kukata simu, alivua taulo kisha akavaa pensi na tisheti, ndipo akatoka nje na kuelekea mpaka kwenye gari la kepteni Mwambukusi.

"Nambie kepteni?" Alisema baada ya kuingia kwenye gari na kukaa kwenye siti ya mbele upande wa abiria.

"Salama kamishina." Kepteni Mwambukusi alijibu salamu ile huku akiwa mtulivu kwelikweli.

"Kuna nini kimetokea!"

Kepteni Mwambukusi alijaribu kujenga tabasamu la kulazimisha. Ndipo akamweleza kamishina Marwa: *"Ah!* Mambo yetu tu haya ya kazi kamishina."

"Mambo ya kazi ndiyo yamekuleta huku muda huu? Na ndiyo yanakuzuia usiingia nyumbani? *Come on!* Nini kinaendelea ambacho sifahamu kepteni?"

"Kuna mvujishaji miongoni mwetu, anayeshirikiana na mtandao wa Goma Cartel!" Kepteni Mwambukusi sasa aliamua kupasua jipu.

Kamishina hakuzungumza mara moja alibaki ametoa macho akimtazama kepteni Mwambukusi kwa macho ya pembeni, ambaye naye alikuwa anamtazama kwa macho ya moja kwa moja.

"Unamaanisha nini?" Mwishowe alimuuliza.

"Kamishina, namaanisha nilichosema. Haiwezekani kila mipango tunayoipanga inavuja lazima miongozi mwetu kuna mtu au watu wanaotusaliti. Lakini sijajua ni nani au ni kina nani? Lakini ninauhakika wapo!

"Kamishina," Kepteni Mwambukusi, aliita kwa msisitizo huku ameyakaza macho yake na uso wake ukionyesha hauna mchezo hata kidogo.

"Sisi tunatumia nguvu kubwa kuhakikisha misheni hii inakamilika, lakini wengine kwa manufaa yao binafsi, manufaa ya matumbo yao wanatumia nguvu kubwa kuhakikisha hatufanikiwi. Hapana hili sikubaliani nalo hata kidogo. Nipo radhi kufanya lolote lile lililo ndani ya uwezo wangu kuhakikisha nampata huyu mvujishaji. Na kamishina naapa huyu nitamuua kwa mikono yangu mwenyewe! *I swear it!"*

*"Hey come down!"* Hatimaye kamishina Marwa alizungumza kwa utulivu, mwisho akakaa kimya na kupitisha mawazo mawili matatu kwenye ubongo wake.

Mwishowe akasema; "inabidi tuitishe kikosi cha wanausalama usiku huu."

Kepteni Mwambukusi alijikuta akimrushia macho kamishina Marwa. Maamuzi aliyoyachukua kamishina huyu, kepteni Mwambukusi hakuyategemea kabisa. Yamekuwa ni maamuzi ya ghafla yaliyomshitua pia.

"Usiku huu?"

"Ndiyo kepteni! Hatuna muda zaidi wa kuendelea kupoteza. Kama tukipoteza muda na kuna mtu anavujisha haya, tutegemee kusikia habari mbaya siku ya kesho. Lakini tukililikabili hili leo, kesho mchana wakati ambao waziri wa mambo ya nje atakapokwenda kutembelea Kongo zoezi likamilike kama ambavyo limepangwa katika mpango wa awali."

"Na ukiwaita utawaeleza jambo gani?"

"Tutawaeleza ukweli kuwa tuna mashaka na jopo la juu la usalama

na kuna mwenzetu ama wenzetu ambao wanatusaliti na kurudisha harakati zetu nyuma."

"Unahisi hiyo itasaidia?"

"Ndio. Maana lengo kubwa si kuishia kuwaeleza. Lengo kubwa ni kuhakikisha kila anayeingia katika mkutano huo, simu yake inachukuliwa na bila wao wenyewe kufahamu, inawekewa kifaa maalumu cha kurekodi mazungumzo ambacho pia kina *GPRS,* kitakachotuwezesha kuwafuatilia."

"Wakigundua kamishina?"

"Utakuwa ni mkakati maalumu ndani ya mkakati."

Kepteni Mwambukusi alipiga kimya kifupi na kushusha pumzi fupi. Alichekecha mawazo yake na hatimaye alikubaliana na mawazo ya mkuu wake yule wa kazi kwamba wafanye kama alivyosema. Hilo ndilo likafanyika!

*****

Wakuu wa idara mbalimbali za ulinzi na usalama, walifika makao makuu ya kitengo cha usalama, wakiwa ni wenye maswali mengi juu ya nini kinaendelea.

Ilikuwa ni nadra mno wakuu hao kukutana kwenye kikao cha dharura namna hiyo, na mara chache ambapo imewahi kutokea hivyo, ni pale ambapo kunakuwa na taarifa nyeti za siri zinazohatarisha usalama wa taifa.

*Sasa leo kuna nini?*

Kila mmoja wao alijiuliza kichwani!

Na jambo lililowashangaza zaidi ni protoko za siku hiyo. Hakuna kiongozi hata mmoja, pasipokujali cheo chake, aliyeruhusiwa kuingia na kifaa cha mawasiliano cha aina yoyote ile; ukaguzi ulikuwa ni mkali mno na vifaa vyote vya mawasiliano vilichukuliwa na wanausalama maalumu waliokuwa wamewekwa kwa ajili ya kazi hiyo ya ukaguzi na kuweka *divice* maalumu kwenye vifaa hivyo kwa ajili ya kufuatilia mawasiliano ya kila mmoja wa vigogo hao.

Kwenye ukumbi wa mikutano, vigogo hao wa idara za usalama na ulinzi walikaa kimya wakimsubiri aliyeitisha kikao hicho, Kamishina Marwa Warioba aweze kufika na kuwaeleza kile kilichofanya awakusanye kwa kuitisha kikao cha dharura.

Na kama kawaida, kwenye kikao hicho ukimuweka pembeni mkurugenzi wa idara ya usalama Kamishina Marwa Warioba na jopo la wasaidizi wake, vigogo waliofika kwenye kikao hicho ni pamoja na mkuu wa majeshi, mkuu wa idara ya usalama jeshini *(MI),* mkuu wa idara ya interejensia ya nchi, waziri wa ulinzi, waziri wa mambo ya ndani pamoja na waziri wa mambo ya nje, ambaye alikuwa anatarajia kusafiri siku iliyofuata kuelekea nchini Kongo.

Dakika ziliyoyoma, na hatimaye mlango wa chumba kile cha mikutano ulifunguliwa na akaingia ndani kamishina Marwa akiongozana na wasaidizi wake wawili.

Alipofika kamishina Marwa aliwasabahi wale vigogo wa idara za usalama na ulinzi kisha akaketi kwenye kiti kimojawapo kati ya vile ambavyo vilikuwa wazi na walinzi wake nao waliketi kwenye viti vingine.

Baada ya kuketi, kamishina Marwa alipitisha macho katika nyuso za wale viongozi akiwa ametulia kimya kisha akajikuta akishusha pumzi fupi. Na ndipo alianza kuzungumza nao na kuwaeleza yote yaliyomfanya aitishe kikao hicho.

Kikao kilichukua muda wa takribani dakika arobaini.

Kilipomalizika, vigogo wote walitoka na baadaye kamishina Marwa alikutana ndani ya ofisi yake na kepteni Mwambukusi.

“Wakati kikao kinaendelea kuna mawazo nimepata.” Kamishina Marwa alimwambia kepteni Mwambukusi.

“Mawazo gani kamishina?”

“Nimewaza nawe uende Kongo kesho.”

Kepteni Mwambukusi hakuzungumza mara moja. Kwa sekunde kadhaa alibaki akimtazama kamishina Marwa, na akilini mwake akajikuta anawaza; ni nini hasa kamishina Marwa amefikiria hata amtake yeye aende Kongo! Mwishowe alimuuliza: “umewaza nini

kamishina?"

"Naona kuna haja ya kwenda kuongeza nguvu wakati tunamtafuta huyo mtu wetu."

*"Ohoo,"* kepteni Mwambukusi alisema huku akitikisa kichwa kuonyesha alikuwa anaafikiana na kamishina Marwa, "hakuna shida kamishina. Nimekuelewa vyema wacha sasa niende nikajiandae," aliongeza.

"Sawa."

Kamishina Marwa na kepteni Mwambukusi walishikana mikono kisha kepteni Mwambukusi alitoka ndani ya ofisi hiyo na kufunga mlango nyuma yake!

*****

Majira ya saa kumi alfajiri hivi, mara simu ya kepteni Mwambukusi iliita. Simu hiyo iliita mara kadhaa na hatimaye ikafanikiwa kumuasha kepteni Mwambukusi ambaye alikuwa bado anaogelea usingizini.

Baada ya kushituka, kepteni Mwambukusi aliichukua simu yake na kutazama jina la mpigaji, alikuta ni kamishina Marwa. Kepteni Mwambukusi aliipokea simu hiyo:

"Kamishina…" Aliita akijinyoosha huku akijaribu kupambana na uchovu wa usingizi.

"Kepteni..."

"Simu yako ni dalili ya kwamba kuna mapya," kepteni Mwambukusi alisema akijiinua kitandani pale na kukaa huku anajinyoosha nyoosha.

*"Ah!* We acha tu, ingia kwenye barua pepe yako."

"Kuna nini?"

"We ingia bwana."

"Sawa kamishina."

"Ukifungua utanirejea."

*"Copy that!"*

Simu ilikatwa.

Kepteni Mwambukusi bila kupoteza muda, aliiweka simu juu ya droo ya kitanda kisha akachukua komputa mpakato yake ambayo nayo haikuwa mbali na mahala pale alipokuwa. Haraka haraka akiwa na shauku ya kutazama ni nini alikuwa ametumiwa na kamishina Marwa, aliiwasha komputa yake na kuingia moja kwa moja kwenye mtandao wake wa *yahoo.*

Kepteni Mwambukusi baada ya kufungua alikuta kuna ujumbe kutoka kwa kamishina

Marwa na alipoufungua alibaini ni ujumbe wa *audio.*

Akaifungua na kuanza kusikiliza.

*"Tunapaswa kuwa makini sana! Wamekwishabaini kwamba mtu anayetoa taarifa ni miongoni mwa viongozi wa juu wa idara za ulinzi na usalama! Kwasasa tuingie gizani mpaka pale yale tuliyopanga yatokee Kongo!"*

*"Sawa! Vipi kuhusu Pacel?*

*"Kesho mchana."*

*"Utakuwa umekwishafika."*

*"Ndio."*

*"Ratiba ya kikao."*

*"Haijatoka, ila nimependekeza mchana."*

*"Utanipa muda?"*

*"Lazima."*

*"Haya. Itakuwa vyema. Kama tulivyokubaliana; wakati ukiwa kwenye kikao, na huyo waziri wa madini na nishati, huko Goma tutatekeleza mpango wetu. Na watu wetu watafika kwenye eneo la kikao chako kuhakikisha huyo waziri hatoki na uhai."*

*"Hakuna shida. Ila baada ya hapa tusitafutane. Ratiba ya kikao nitatuma code."*

*"Sawa. Ila ukitoka Kongo pita Rwanda, mheshimiwa rais anahitaji akuone!"*

*"Sawa!"*

Kepteni Mwambukusi aliicheza kwa mara nyingine ile *audio* na kuisikiliza, lakini bado ilikuwa ngumu kubaini sauti zile zilikuwa ni

za kina nani pamoja na kwamba, sauti ya mmoja wa wazungumzaji haikuwa ngeni masikioni mwake.

Akaicheza tena na tena lakini bado hakuweza kubaini.

Ikabidi ampigie kamishina Marwa kama ambavyo walikubaliana.

"Kepteni…"

"Kamishina…"

"Umesikiliza?"

*"Yes!"*

"Umebaini nini?"

"Sijabaini lolote."

"Hata moja?"

"Kuna sauti si ngeni masikioni mwangu lakini nashindwa kubaini ni ya nani."

"Si waziri wa mambo ya nje huyo Amosi Mokiwa!"

*"Yes! Jesus!* Ni waziri ndio, sauti sasa imeniijia *doh!"*

"Mambo haya magumu sana. Hawa watu wamehakikisha wanashika kila sehemu nyeti."

*"Dah!* Tunafanyaje kamishina?"

Kamishina alijenga ukimya wa haja.

*"Hallo!*" kepteni Mwambukusi aliita.

"Nipo kepteni. Natafakari…anyways jiandae kwa ajili ya safari yako nitakutumia barua pepe!"

"Sawa mkuu."

Walimaliza maongezi.

Baada ya kukomesha mazungumzo yale na kamishina Marwa, kepteni Mwambukusi alirudi kwenye mtandao wake wa *yahoo* kisha akaicheza audio ile na kuisikiliza kwa mara nyingine, akiendelea kuisikiliza alijikuta anazungusha kichwa kwa masikitiko na akabwaga kite cha hasira iliyochanganyikana na mfadhaiko.

Baada ya kumaliza kuisikiliza ile *audio*, aliufunga ukurasa ule wa barua pepe na kufungua mwingine. Hapo alimuandikia ujumbe Biruse kisha akatoka kwenye ukurasa huo na kuifunga komputa yake.

Kepteni Mwambukusi, alibaki hapo kimya akitafakari kwa muda juu ya hayo yote, na hakika moyo wake ulikili kuwa mtandao huo wa Goma Cartel, ulikuwa ni hatari na zilihitajika jitihada za makusudi na zenye umakini wa hali ya juu katika kupambana nao!

# 13

*Kinshasa, Kongo.*

BIRUSE na Sasha walifika Kinshasa kwa helkopta maalumu ya usalama. Walipata malazi katika hoteli moja iitwayo Kingdom huko Barumbu, kwa ajili ya kupitisha usiku wa siku hiyo, kabla ya siku iliyofuata kuianza misheni kwa namna ambavyo mipango ilikuwa imepangwa.

Hata hivyo, wakati wanaagana na Alhadj Jumbe Ndaizeye, huko Gasiza, Rwanda, aliwapa tahadhari juu ya taifa hilo la Kongo. Alhadj aliwaeleza, Kongo ni hatari kuliko maeneo yoyote yale waliyopita na wanapaswa kuwa makini katika kila nukta watakayopiga kwenye misheni hiyo.

*"Mashushushu wa Goma Catrel wamejaa chungu nzima, kuweni makini katika kila hatua,"* Alhadj Jumbe Ndaizeye, aliwaambia.

Akiwa katika chumba chake cha hoteli, Biruse baada ya kuoga alipata mawazo ya kutembelea kwenye mtandao wake wa *Yahoo.* Alipata shauku hiyo, kutokana na mambo mawili. Jambo la kwanza, alifahamu ni lazima kepteni Mwambukusi atakuwa amemtafuta kwa ajili ya maelekezo juu ya misheni hiyo. Lakini, sababu nyingine, Biruse alihitaji kuangalia ikiwa mpenzi wake Zinaeda naye amemtafuta baada ya kumtumia ujumbe wake akiwa Kigali, Rwanda.

Kwahiyo, Biruse aliamua kwanda mpaka mapokezi, akamuulizia muhudumu juu ya huduma ya intaneti. Muhudumu yule, ambaye alikuwa ni mdada mfupi, mwenye weupe wa kuchovya, alimuelekeza.

Biruse alikwenda mpaka kwenye chumba kile kulipokuwa kunatolewa huduma ya intaneti kwa wateja wa hoteli hiyo, akakaa na kuanza kufanya mambo yake yaliyompeleka hapo.

Baada ya kufungua alikutana na jumbe nyingi, lakini alijikita kwenye jumbe mbili. Wa kwanza ulikuwa ni wa Zinaeda ambao ulionekana haukuingia saa nyingi zilizopita. Aliufungua:

*Hello B!*

*Thanks for your massage, I missed you so much my love.*

*I'm sorry, I didn't manage to talk anything with my dad about what you asked.*

*I am in Izrael right now. I have come to keep up with my sturdies, but I hope*

*You will get a way for that. I trust you, you are so intelligent and a man of winning.*

*I love you so much B.*

*I hope we will se each other again one day!*

Biruse baada ya kumaliza kusoma ujumbe ule wa Zinaeda, alibaki ametulia kwa dakika chache akijifikiria mawili matatu. Ilimshangaza kusikia msichana huyo amepelekwa Izrael kwa ajili ya masomo! Akajiuliza; *anasomea nini Izrael? Au mambo ya interejensia?* Maswali yalikuwa ni mengi yasiyokuwa na majibu.

Lakini pia Biruse, alijiuliza ni kwanini Zinaeda hajaweza kuzungumza na baba yake juu ya ujumbe wake? Ni kwa sababu yupo Izrael kimasomo ama kuna sababu nyingine nyuma ya hiyo? Ujumbe ule wa Zinaeda ulimfikirisha sana.

Hata hivyo, baada ya kutafakari kwa muda, aliujibu ujumbe huo na kuamua kuachana nao. Akafungua barua pepe kutoka kwa kepteni Mwambukusi ambapo alikutana na *audio* pamoja na maelekezo. Alianza kusikiliza *audio* ile!

Wakati Biruse alikuwa anasikiliza hiyo *audio* alikuwa anasoma pia maelekezo yale aliyokuwa ameandikiwa na kepteni Mwambukusi

juu ya usaliti wa waziri wa mambo ya nje, Amosi Mokiwa!

Habari hizo zilikuwa za kushangaza sana kwa Biruse. Waziri wa mambo ya nje ni mtu ambaye mara zote amekuwa akizungumziwa vyema na wanasiasa pamoja na viongozi mbalimbali kwamba ni miongoni mwa viongozi wa kutazamwa na vijana kutokana na uongozi wake uliotukuka na kuna tetesi kwamba anatarajia kujitupa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania urais wa taifa hilo kwenye uchaguzi ujao.

*Kumbe huyu jamaa ni mshenzi namna hii?*

Biruse alijikuta akizungumza mwenyewe.

Kwenye maelekezo hayo ambayo aliandikiwa, kepteni Mwambukusi alimjulisha pia Biruse kwamba masaa machache mbele atakuwa amekwishafika Kongo kuungana naye kwenye misheni hiyo. Na alimtaka ahakikishe kwenye majira ya saa tano za asubuhi anakuwa kwenye mtandao ili aweze kusoma maelekezo ya nini kinafuata.

Baada ya kumaliza kusikiliza na kusoma hayo yote, Biruse alimuandikia pia kepteni Mwambukusi, ujumbe kuhusu yale yaliyojiri Gasiza na alimpasha juu ya habari za mtu aitwaye Nsaku Mboya!

Biruse alipohakikisha amemaliza shughuri zote alizokuwa amepanga kuzifanya mahali hapo, aliufunga ukurasa wake wa barua pepe na akatoka kwenye mtandao wake wa yahoo kisha akatoka kwenye mgawaha huu wa huduma za kimtandao.

Alitembea kurudi kule kwenye chumba chake. Alipofika mapokezi, alikuta kuna watu wawili wamesimama mahali hapo, ambao walikuwa wamevalia mavazi yanayowaonyesha kuwa ni askari jeshi, wakizungumza na muhudumu wa mapokezi.

Biruse hakujishughulisha nao, aliwapita na kuzidi kupiga hatua. Hata hivyo, kabla hajafika mbali, mara mmoja wa wale askari wawili alianza kupiga hatua kumfuata huku akiita.

"Hey…hey…we bwana…hey…" huyo askari alikuwa anaita huku maneno yake akiyazungumza kwa Kifaransa.

Biruse alivunga kana kwamba alikuwa hasikii ama hana habari kuwa yule askari alikuwa anamuita yeye.

Lakini yule askari alipozidisha kumuita, hakuwa na namna zaidi ya kusimama ili kumsikiliza anahitaji nini.

"Habari yako bwana," yule askari alimsabahi alipomfikia akizungumza kwa Kifaransa.

Biruse alimpasha kwa Kingereza kwamba hawezi kuzungumza lugha hiyo aliyokuwa anamzungumzisha.

Ndipo huyo askari alipomuuliza kwa Kingereza kibovu:

"Wewe ni mgeni?"

Naye Biruse alimjibu: "Watu wote kwenye hii hoteli si wageni?"

"Namaanisha hapa Kongo?"

"Ndio, mimi ni mgeni."

"Umetokea wapi?"

"Tanzania."

"Upo hapa kwa ajili ya shughuri gani?"

Biruse hakujibu mara moja, alimtazama huyo askari kwa macho ya moja kwa moja na akajikuta moyoni mwake anajiuliza; *huyu mjinga ananitaka nini lakini!*

"Nakuuliza!" Akiwa bado yupo kimya, yule askari alimuuliza tena.

Biruse bila kuzungumza neno lolote, alijipapasa mfukoni mwake, akatoa kitambulisho chake na kumuonyesha yule askari huku akiwa amemkazia macho.

*"Oh!"* yule askari alisema akionyesha mshangao, "kumbe mwanausalama! Karibu Kongo mkuu!" yule askari alimrudishia kitambulisho chake kisha akamtaka aendelee na utaratibu wake.

Hata hivyo, kwa upande wa Biruse wakati anapiga hatua, alijikuta akiwaza juu ya tukio hilo la kusimamishwa na huyo askari pamoja na uwepo wao mahala hapo. Kwa namna moja ama nyingine, alilihusisha jambo hilo na masuala ya rushwa. Kwamba huenda hao askari walikuwa wakija kwenye hoteli hiyo kwa ajili ya kubanana na wageni, na kuambulia chochote katika namna ambayo waliifahamu

wao.

Mbali na hilo, kitendo cha huyo askari kufahamu kuwa yeye ni mwanausalama, alikiona kinamuweka yeye na Sasha katika hatari. Kwa namna ambavyo mtandao wa Goma Cartel, ulivyokuwa umejipenyeza kila kona, alifahamu kuna hatari ya kufahamika kwamba wapo mahali hapo jambo ambalo kwa namna moja ama nyingine linaweza kuharibu mipango yote juu ya misheni hiyo. Kwahiyo, Biruse alipata mawazo kwamba hilo eneo si salama kwao tena na Sasha.

Sasa, badala ya kwenda moja kwa moja kwenye chumba chake, alikwenda mpaka kwenye chumba cha Sasha malengo yake ni kwenda kumpasha hayo yaliyojiri ili ikiwezekana pia amtake wajiandae kuhama hoteli hiyo.

Alifika mlangoni na kugonga lakini hakuna aliyeitika ndani. Aligonga tena na tena, lakini kulikuwa kimya! Biruse alipata mawazo ya kurudi chumbani kwake ili aweze kumpigia simu ya mezani, maana alifikiria pengine Sasha alikuwa ameamua kuutumia muda ule mchache waliokubaliana kujiweka sawa hapo hotelini kwa kulala. Lakini, hata alipofika chumbani kwake aliipigia simu ya chumbani kwa Sasha zaidi ya mara tano ila haikupokelewa.

*Ama ametoka na kuzungukia kutazama mazingira?*

Biruse alijiuliza. Hakupenda kuamini kwamba Sasha alikuwa chumbani kwake amelala na hakuwa anasikia simu zile alizompigia.

Kijana huyo, hakutaka kuendelea kubaki ndani ya chumba hicho, maana sasa tayari kuna nuksi anaiona imeanza kunyemelea kwenye misheni yao. Alitoka ndani ya chumba chake akaanza kuzungumza kwenye maeneo mbalimbali ya hoteli ile akijaribu kumtafuta Sasha, lakini kijana huyo alizunguka katika mazingira yote ya hiyo hoteli na wala hakuweza kumpata Sasha!

Biruse alichoka!

*****

Kwa upande wa Sasha, baada ya kuachana na Biruse, saa chache zilizopita, akiwa chumbani kwake alijikuta akipata mawazo ya

kuutumia muda ule wa mapumziko mafupi kwa kutafuta namna ya kuufanya mwili wake *u-relux,* maana mwili wake ulikuwa na uchovu mwingi kutokana na safari pamoja na yale yote ambayo walikuwa wameyapitia katika misheni hiyo.

Ndipo yalipokuja mawazo ya kwenda *spa* kupata huduma ya *massage!* Huduma ambayo mwanadada huyu alikuwa anaipenda kufanya na alikuwa na uzowefu nayo.

Baada ya kupata mawazo hayo, moja kwa moja Sasha alichukua karatasi ambayo ilikuwa juu ya meza yake humo chumbani ambayo ilikuwa inaeleza juu ya huduma za *massage,* zitolewazo katika *spa* iliyopo hotelini hapo, akachukua namba za simu zilizowekwa hapo na kuzipigia kisha akauliza ikiwa anaweza kupata huduma wakati huo. Alijibiwa kuwa inawezekana, ndipo alichukua uamuzi wa kwenda mahala huko.

Aina ya *massage* ambayo, Sasha alikuwa anaihitaji ni ya *body to body massage;* ambapo huduma hii ilikuwa inamhitaji mteja kuvua nguo zake zote kisha kupakwa mafuta mwili mzima na mtoa huduma naye anahitajika kuvua nguo zake zote, kisha naye kujipaka mafuta, ndipo huanza kumhudumia mteja kwa utaalamu wake, ukihusisha kumpapasa, kumkandakanda kwa mikono na kugusanisha viungo vyao. Na Sasha alihitaji huduma hiyo afanyiwe na mwanaume kwa sababu alikuwa anahitaji kupata mguso ambao ungemfanya kwa dakika chache aweze kuiacha nyuma dunia aliyokuwa anaishi ya kikachero.

Baada ya kufika *spa,* Sasha alikutanishwa na mtoa huduma; ambaye alikuwa ni kijana ambaye si mrefu hata avume kwa sifa hiyo na wala si mfupi ukimliganisha na wafupi unaowafahamu; mwili wake ulioonekana kuwa imara kutokana na kunyanyua vyuma vizito. Kijana huyo alikuwa na kifua kipana na mikono iliyojaza. Kichwani nywele zake alikuwa amezitengeneza kwa mtindo wa *dreadlock!*

“Karibu…” alimkaribisha.

“Asante.” Sasha alijibu.

Mwanadada huyo alionyeshwa mahala pa kubadilishia mavazi yake, ambapo alikwenda na kuvua nguo zake zote kisha akajifunika taulo.

Chumba hicho cha *massage,* kilikuwa na kiyoyozi ambacho kilikuwa kinatema hewa safi kila mahala. Kitendo kilichoyafanya mazingira ya chumba hicho kupoa mno. Lakini pia, kulikuwa na mishumaa iliyowekwa kwa ustadi mkubwa kwenye stendi zilizokuwa zinakizunguka kitanda cha kufanyia huduma hiyo ya massage. Na kwa mbali, ulisikika muziki mzuri wa miondoko ya *country,* ambao ulizidisha kunogesha utamu wa mazingira hayo.

Kuta za chumba hicho zilipakwa rangi nyeupe na kulitawala kila mahala mataulo meupe na kulikuwa na baadhi ya picha ukutani za walimbwende ambao walikuwa nusu utupu katika mapozi mbalimbali.

Sasha, alipotoka katika kichumba hicho cha kubadilishia mavazi, alikuta yule kaka naye tayari amekwisha jiandaa kwa ajili ya kazi yake. Huyo kaka alikuwa amejifunga kiunoni taulo nyeupe na kifuani alikuwa wazi.

Sasha alimtazama yule kijana kwa namna mwili wake ulivyokuwa umeimarika na misuli kuchomoka, akajikuta mwili wake unasisimka. Mwanamke huyu kutokana na kazi yake, hakuwa na mahusiano ya kimapenzi ya kudumu. Amejaribu mara kadhaa lakini aliishia kuvunja mahusiano kutokana na wapenzi aliojihusisha nao kuhatarisha kazi yake. Kwahiyo Sasha amekuwa *single* kwa kipindi kirefu na mara kwa mara alipokuwa anazidiwa na mwili kutokana na hisia za uhitaji wa kufanya mapenzi, alikuwa akimaliza haja zake kwa kuwatumia vijana wa kwenye vijumba vya *massage.*

Hata hivyo, siku hii, Sasha jambo kubwa alilokuwa anahitaji ilikuwa ni kupapaswa kila mahala mwilini mwake na kakandwakandwa; hakuwa na uhitaji wa kufanya mapenzi. Lakini alipoyaona maungo ya kijana huyo ya juu, na macho yake yakashuka mpaka kwenye taulo, akajenga fikra za kitu alichokifikiria yeye mwenyewe kichwani katika ulimwengu wake wa mahaba, alijikuta akisisimka

katika namna ya kuhitaji kufanya mapenzi.

"Karibu ulale kitandani," yule kijana alimkaribisha.

Sasha alijilaza katika kile kitanda kidogo, ambapo huduma hiyo ya massage ilikuwa inafanyikia. Alilala kifudifudi. Na baada ya kulala, yule kijana alilitoa taulo ambalo Sasha alikuwa amejitanda naye akatoa lake pia.

*Waoh!* Alijikuta anajisemea moyoni. Sasha alikuwa ameumbwa na kuumbika. Umbo lake jembamba kwa namna fulani, lilimpa chati iliyomfanya avutie kwa wengi na muinuko uliojiumba chini ya mgongo ulimfanya huyu kijana mtoa huduma asimamishe maungo yake ya kiume.

Kijana huyo, alichukua mafuta na kumnyunyizia Sasha katika mwili wake wote. Kisha akaanza kumpapasa kutokea katika maeneo ya mabega mpaka kwenye vidole vya miguu na akawa pia anajiviringisha juu ya mwili wake. Kijana huyo akiendelea na huduma hiyo kwa ustadi wake, ilifika hatua Sasha alizidiwa na ashiki zake. Mwanadada huyo pasipo kutarajia alijikuta akiyashika maungo ya mbele ya kijana huyo na huku akizungumza kwa namna iliyoonyesha wazi alikuwa amezidiwa alimweleza yule kijana atampa kiasi cha pesa anachokihitaji ila tu, ampe huduma aliyokuwa anaitaka kwa wakati huo.

Ya kumsafirisha mpaka mawinguni kisha kumrudisha angani, waelee hapo kwa dakika kadhaa, washuke mpaka chini na kabla hawajajibamiza chini warudi tena mawinguni na waishie kuyagusa mawingu.

Kijana huyo hakuwa na hiyana; alifana kama ambavyo Sasha alihitaji kiasi cha kumridhisha kusiko na kipimo!

*****

"Ulikuwa wapi Sasha? Jesus, unajua nimekutafuta sana?" Biruse alimuuliza Sasha baada ya kukutana naye nusu saa baadaye.

*"Ah!* Nilikuwa *spa* kidogo."

*"Spa?"*

*"Yes!"*

"Kufanya nini?"

"Kufanya *massage.*"

*"Massage* Sasha! *Real?* Tumekuja kustarehe huku?"

"Usijali sana B; akili na mwili wangu vilikuwa vinanihitaji *kurelux* kidogo."

Biruse aliishia kumtazama yule kachero mwenzake pasipo kummaliza; akaishia kujisemea moyoni: *wanawake wana mambo mengi sana!*

Basi, mwisho wa yote; Biruse alimweleza Sasha kile ambacho alikuwa na mashaka nacho na akamtaka mwanadada huyo kufanya hima kwenda kujiandaa ili waweze kuachia vyumba hivyo.

Walitumia takribani muda wa dakika arobaini na mwishowe waliweza kutoka kinyemela na kutokomea mtaani. Ambapo wakati huo tayari kulikuwa kumekwisha anza kupambazuka na walikubaliana kuingia mtaani kumtafuta mtu aitwaye Nsaku Mboya, ambaye waliambiwa kuwa ni maarufu katika maeneo ya Barumbu, katika mtaa wa Bokkasa. Na kumpata mtu huyo; ndipo kungewafanikisha kufika kwa mtu aitwaye Rusogotason!

Katika majira hayo ya saa moja asubuhi, Barumbu ilikuwa bado haijaamka kutoka kwenye usingizi wake. Mitaa ya mji huo ilikuwa bado imelala na watu hawakuwa wengi mitaani.

Hali ya hewa ilikuwa tulivu, vumbi la ukungu lilionekana kwa mbali kwenye ghaya ya macho ya kina Biruse na Sasha, na kutokana na mazingira hayo, walichukua uamuzi wa kuingia kwenye mgahawa mmoja katika mtaa huo wa Bokkasa, kwa ajili ya kupata kifungua kinywa ili pia wasukume muda, wa kulianza zoezi lao la kumtafuta Nsaku Mboya.

Kwenye majira ya saa mbili na nusu hivi, ndipo wawili hao waliweza kuingia tena mitaani. Na wakati huu mitaa ilikuwa imemakinika kwelikweli. Kila mahala kulichangamka, tofauti na muda wa lisaa limoja lililopita, watu walikuwa wanahaha kwenye

hekaheka zao kila mmoja na lakwe!

Huyu kaingilia huku yule kapitia kule, ilimradi ni hekaheka za kupeleka mkono kinywani!

"Kaka samahani…" Biruse alimwambia bwana mmoja ambaye alikuwa kwenye biashara yake ya kuuza vifaa vya magari.

"Sema mozee…" yule jamaa alijibu kwa Kiswahili kibovu.

"Kuna ndugu mmoja namuulizia, sijui kama utaweza kumfahamu!"

"Ndungu?"

"Ndiyo, Nsaku Mboya."

'Nsaku Mboya?" Baada ya Biruse kumtajia yule kijana hilo jina, naye alirudia kulitaja kwa mshangao huku akimtazama Biruse kwa macho ya moja kwa moja kisha akayasambaza kumtazama Sasha.

"Unantafunta hiyo muntu Nsaku Mboya?" huyo kijana alimuuliza tena Biruse.

"Ndiyo."

"Unamjua?"

"Hapana, ila kuna mtu ninayemfahamu anafahamiana naye na ndiye amenielekeza kwake."

Yule jamaa aliangua kicheko.

Hilo lilikuwa ni tukio la kuwashangaza Sasha na Biruse. Walitazamana huku wakijiuliza huyo kijana anacheka kwa sababu gani. Ni jina ndilo linamchekesha ama maelezo ambayo Biruse amemweleza yalikuwa yanafurahisha kiasi kwamba avunjikie kwenye kicheko cha namna hiyo?

"Kwani vipi kaka unamfahamu?" Sasha aliyekuwa kimya kwa muda ilimbidi naye aingilie kati na kuuliza.

"Nyie mmerunkwa ankili, si buye!" Yule kijana mwishowe aliwaambia.

Sasha na Biruse nyuso zao zilihamanika lakini hawakutaka kuonyesha mashaka yao waziwazi.

"Unamaanisha nini?" Biruse alimuuliza yule jamaa.

"Haiwezekani kutafunta Nsaku Mboya!"

"Haiwezekani kivipi?" Biruse alimuuliza yule kijana.

"Nsaku ni mwendawazimu. Muda yote yupo huku na kuye kwa mntaa. Kula yake ni kwa jalala na kulala popote paye. Iwe ngambo ya barabara, kwenye majumba mabovu, nyie mnamtafunta ili awasaidie jambo gani yule?"

Maelezo ya huyo kijana yaliwafanya Biruse na Sasha watupiane macho. Macho yao yalizungumza harakaharaka lakini wao hawakuelewa hata yalizungumza nini, na kisha walirejea kumtazama tena yule kijana. Na wakiwa bado hawajamjibu jambo lolote, mara walimuona akiwa ametoa macho kutazama umbali mfupi kutoka walipokuwa, kisha akaanza kubwabwaja:

"Haya muntu yenyu ile kuye!" Huyo jamaa alikuwa na Kiswahili kibovu kwelikweli. Lakini afadhali kwao walikuwa wanamudu kumuelewa.

Vijana hao waliyarusha macho yao ng'ambo ya barabara, wakaweza kumuona mtu yule waliyekuwa wanaonyeshwa kuwa ndiye Nsaku Mboya!

Alikuwa ni jamaa mmoja mrefu, aliyevaa mavazi yaliyochakaa na nywele zake chafu zilikuwa nyingi kiasi kwamba zilijisokota zenyewe na kumfanya aonekane ametengeneza rasta. Jamaa huyo aliyeonekana ni mwendawazimu alikuwa amebeba furushi kubwa la takataka yupo anakatiza kuelekea upande mwingine wa mtaa. Na mguuni alivaa ndala moja ambayo ilikuwa imekatika upande mmoja wa mikanda na imechoka kusivyo kawaida.

"Huyo ndiye Nsaku Mboya ama unatutania?"

*"Yeh!* Natania miye…nyie mnko vipi!"

Biruse na Sasha walimshukuru yule kijana na wakaamua kupiga hatua hata wakavuka barabara kwenda kumfuatilia yule mwendawazimu.

Walimfuatilia kwa tahadhari sana. Walimaliza naye mtaa wa kwanza wakafuata mwingine, akaingia kwenye uchochoro na kutokea kwenye mtaa mwingine, nao walikula naye sahani moja tu, mpaka alipokwenda kwenye jalala moja kubwa lililokuwa limejikita kwenye mtaa wa pili kutoka huo wa Bokkasa, akaenda kukaa chini

ya mti mmoja wa kivuli, kisha akaanza kupekua kwenye furushi lake lile la takataka.

Biruse na Sasha walipiga hatua taratibu kumuelekea yule mwendawazimu huku wakiwa ni wenye tahadhari kubwa kuliko kawaida.

Walipofika karibu aliinua macho kuwatazama nao walimkazia uso na kuzidi kumsogelea lakini walipomfikia karibu zaidi yule mwendawazimu alisimama akionekana ni kana kwamba alitaka kuwakabili.

Ndipo walipotoa vitambulisho vyao na kuwaonyesha. Mwendawazimu huyo alifinya macho kitendo kilichoufanya uso wake utengeneze ndita kadhaa; kisha akatamka kwa ukali: Gasiza?

Biruse naye alijibu: Bihagarason!

Huyo mwendawazimu alilazimisha mate kupita kooni kisha akawaonesha Biruse na Sasha mahala pa kukaa.

Wakakaa wote.

"Mnatoka wapi?" yule mwendawazimu aliwauliza akizungumza kwa sauti iliyopoa.

Hali aliyokuwa anazungumza nayo sasa ilimtoa kabisa kwenye ule wendawazimu ambao alikuwa anaonekana kuwa nao hapo awali. Anaonekana ni mtu mwenye akili zake timamu.

"Tanzania," Biruse alisema, kisha akamtazama Sasha, akamwambia yule bwana; "huyu anatokea Kenya."

Yule jamaa alitikisa kichwa kana kwamba alikuwa anakubaliana na jambo fulani.

"Karibuni Kongo," aliwaambia.

"Asante." Walijibu.

Kisha kimya kifupi kilitawala.

"Tumeagizwa kwako." Biruse alimwaambia.

"Nafahamu," naye alijibu. "Mmeagizwa na Bihagarason kwa ajili ya kufika kwa Rusogotason."

*"Yes!"* Biruse alisema akifinya macho, akamuuliza: "Umejuaje?"

"Misheni zetu ni *patten,* ili kukamilika lazima kipande kimoja

kiungane na kingine, na kingine na kingine! Suala la kuwasubiri nyie ndiyo misheni pekee iliyonileta hapa Kongo. Imenifanya nikawa mwendawazimu siku zote za kukaa hapa, nikiisubiri kwa hamu na uvumilivu mkubwa hii siku ifike nami niweze kumaliza misheni yangu nirudi kwa familia yangu."

*"Oh!"* Sasha alijikuta anabwabwaja.

Yule jamaa aliinua macho na kumtazama Sasha; "Misheni hii ni ngumu mno. Moyo wangu umefarijika kuona mmefika, maana wasiwasi wangu ulikuwa ni kwamba hamtafika. Kuna kuvuta sana kwa taarifa pamoja na usiri mkubwa uliyopo kwenye misheni hii. Lakini maadam mmekuja, nafahamu ni hatua katika ushindi. Kwa upande wangu kuanzia leo sitaonekana tena maeneo haya nitarudi nilikotoka kwa ajili ya kupangiwa misheni nyingine."

Biruse na Sasha walijikuta wakibaki vinywa wazi kutokana na hayo yote waliyoyasikia. Na kwa yote yaliyokuwa yanatokea, taratibu sasa wanakwenda wanaufahamu ulimwengu waliokuwa wanauishi wa misheni za usalama. Si misheni za kitoto. Zinahitaji maarifa makubwa, kujitoa kwa hali ya juu na kuwa tayari kwa lolote lile. Biruse anakumbuka siku moja, kepteni Mwambukusi alimweleza kuwa, mafunzo aliyoyapata juu ya mambo ya kiusalama yatamsaidia kwenye kazi hiyo, lakini uzoefu wa yale atakayokutana nayo kwenye maisha yake ya kila siku akiwa mwanausalama, ndiyo utakaomsaidia zaidi kudumu katika kazi hizo.

"Unafahamu lolote kuhusiana na Goma Cartel?" Biruse alimuuliza Nsaku Mboya.

Nsaku alizungusha kichwa kana kwamba alikuwa anakataa juu ya jambo fulani ama anasikitika. Ndipo akajibu lile swali la Biruse: "Ninafahamu mambo machache tu," alisema taratibu na kuongeza, "ni mtandao madhubuti ambao umejikita kuhakikisha unachota madini utakavyo na unaziendesha siasa za nchi za maziwa makuu!

"Nasikia asilimia kubwa ya vigogo wa serikali, mashirika makubwa na taasisi, pamoja na wafanyabiashara wakubwa wapo kwenye huu mtandao wa Goma Cartel. Huu mtandao ni kama

Vatican kwa kanisa la Roma, hakuna linaloweza kufanyika katika nchi zetu bila wao kupitisha hayo maamuzi!"

"Haya mambo yanawezekanaje?"

"Lakini ndivyo mifumo ya dunia ilivyo! Siku zote wenye nguvu wanaungana kuwakandamiza wanyonge, lakini huwezi kupata wanyonge wakiungana kupambana na udhalimu wa wenye nguvu."

"Ushasikia ni wanyonge na hawa wananguvu, hata wakiungana unafikiri watafanya nini?"

"Umoja ni nguvu ndugu yangu. Kuna msemo wa Kiafrika unasema, buibui wakiungana wanauwezo wa kumfunga simba na utando wake na akatulia."

Biruse alijenga tabasamu hafifu. Nsaku Mboya alikuwa anazungumza kwa msisitizo uso wake ukionyesha ile imani hasa aliyokuwa nayo kwenye yale anayoyazungumza. Hasa suala la umoja!

Kukawa kimya. Kimya kifupi kikadumu. Hatimaye kikakoma. Aliyekikomesha alikuwa ni Biruse. Alikikomesha kwa kuuliza swali:

"Na vipi kuhusu hii misheni, *una-details* zaidi?"

"Hapana," Nsaku alijibu haraka, *"details* pekee nilizonazo ni kuhusu kipande changu. Kumbuka nimekwambia misheni hii ni *patten,* kila mmoja anahusika na kipande chake alichogawiwa!"

Jibu la huyo bwana lilifanya ukimya mwingine ujengeke kati yao. Na wakiwa bado kimya, Nsaku Mboya, mwanausalama aliyekuwa anaishi katika mitaa hiyo akiigiza kuwa mwendawazimu aliingiza mkono kwenye mfuko wa suruali yake iliyochakaa kwelikweli, kisha akatoa kikaratasi na kuwapatia.

Kikaratasi kile kilikuwa kimechakaa pia kama ulivyokuwa mwonekano wake. Na Biruse baada ya kukishika, alikisoma: *Kabira Avanue. House no. 67.* Rusogotason.

Baada ya kukisoma kile kikaratasi, Biruse aliinua kichwa na kutazama Nsaku Mboya, kisha alimshukuru kwa ujumbe huo aliompa. Baada ya hapo walizungumza mengine machache na sasa

wakamuaga ili kwenda kuendelea na misheni yao. Naye Nsaku Mboya aliwapa mkono wa kwaheri ya kuonana.

Mwishowe kina Biruse waliondoka katika maeneo hayo na huo ukawa mwisho wa kuonekana kwa Nsaku Mboya kwenye mitaa hiyo ya Bokkasa!

*****

Mwanaume mnene na mfupi, ambaye kichwa chake kilijaa mvi kila mahali, aliyevalia tisheti pamoja na pensi, alikaa kwa kujiachia kwenye moja ya masofa yaliyokuwa yanapendezesha sebule lake.

Kwa namna sebule hilo lilivyokuwa limepangiliwa, lilidhihirisha kwamba, mmiliki wa nyumba hiyo, mambo yake hayakuwa mabaya. Si hohehahe. Ungeweza kumuita bwanyenye! Mtu ambaye Mwenyezi Mungu amemkirimia kwa baraka zake tele!

Ukitazama samani zilizotamalaki sebuleni hapo, ungebaki mdomo wazi. Ni samani za bei ya ghali ambazo huwezi kuzipata kwa mtu anayeishi kwa kuganga njaa!

Naye, mwanaume huyo, mweusi, ambaye pamoja na mvi kuenea kichwa kizima bado uso wake haukuonyesha kutekwa na uzee na mwili wake haukuwa umechoka kama watu wa rika lake wengi walivyokuwa, alikuwa akiwatazama wageni waliokaa mbele yake kwa chati; na hiyo ilikuwa ni baada ya kuwakaribisha, kuwapa chakula na sasa alikuwa akifanya mazungumzo pamoja nao.

"Mnanikumbusha mbali sana," huyo mwanaume ambaye ni Rusogotason, aliwaeleza. "Wazazi wenu walikuwa ni mashujaa kwelikweli," aliendelea kumwaga sera, "watu ambao wameondoka lakini hawakwenda na heshima zao, wamezibakiza hapa, hata tunaishi nazo, tunawakumbuka na tunawapenda."

Mzee huyo mwishowe aliyatuliza macho yake kwa Biruse:

"Hii siku niliisubiri kwa hamu mno. Ni siku ambayo nilitamani inikute nikiwa hai," alitulia kidogo na kuzoa glasi yenye maji iliyokuwa mezani mbele yake.

Akanywa funda mbili na kuirudisha glasi ile pale mezani. Ndipo akaendelea kuzungumza: "Miaka miwili nyuma nilipoelezwa juu

ya siku hii, katika mikakati ya kukabiliana na mtandao wa Goma Cartel,hata kuufuta, mikakati ambayo tuliiweka tukiwa makao makuu ya usalama kule Tanzania, baada ya majina yenu kupitishwa kuwa nyie ndiyo mtakuwa vinara kwenye hii misheni, nilimuomba Mwenyezi Mungu anipe uzima niione siku hii maana ni siku ambayo nilifahamu itanirejesha enzi za ujana wangu. Pamoja na rafiki zangu kina Seyunguson, Bihagarason na mama yake Sasha! Bi Farida! Basi, hatimaye siku hiyo imewadia!"

Kimya kifupi kilitawala kwa muda, na yule mzee alikitumia kimya hicho kujitengeneza vyema pale kitini alipokuwa ameketi, akashusha pumzi fupi, ndipo akaendelea:

"Goma Cartel umefika mwisho wao," alisema taratibu, "nchi zetu haziwezi kuendelea kuteseka kwa ajili ya watu wachache. Walafi na wabinafsi. Umefika mwisho.

"Na nyie vijana, mimi nawaasa. Bado mnanguvu. Mnapokuwa mnapata nafasi za namna hii za kupambana kwa ajili ya mataifa yenu, pambaneni kwa uchungu wote. Haya mataifa mnayoyaona yamefika hapa ni machozi, damu na uhai wa watu ambao hawakujali kitawatokea nini ila tu hatima hii ambayo tunayo sasa.

"Nakumbuka wakati wa vita baridi hapa Afrika. Viongozi walinunuliwa, wakalaghaiwa kukawa na vita kila mahala ya Afrika. Lakini wanausalama tulisimama na matokeo yake ndiyo haya. Nguvu zimwekwisha sasa kwetu, wengine wamekwisha lala pamoja na baba na babu zetu. Kijiti tumekitua kwetu. Simameni kwa kukitoa mkiwa na mzigo wa kuwa na mataifa huru.

"Na mnapokuwa katika mapambano haya, jicho lenu lisitazame sehemu moja. Kwamba Tanzania tu, ama Kenya tu, hapana; mmoja wetu akiwa huru na wengine hawana uhuru, bado sote hatupo huru. Uhuru wa kweli na ambao utakuwa na faida na sisi ni wetu sote."

Yule mzee aliongea mengi. Hakika kinywa chake kilijawa na busara za muda, zilizojikita kwenye matukio na kumbukumbu za wapi Afrika imetoka.

Namna anavyozungumza, alama usoni mwake, ishara alizokuwa

anafanya wakati anazungumza, zilidhihirisha mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo dhidi ya Afrika na nchi zake.

Na akisha kuzungumza hayo, hatimaye alisema kwa kimombo; "by the way," akarudi kwenye Uswahili wake, "nimepata taarifa kuwa kepteni Mwambukusi yupo hapa kuungana na nyie."

"Amekwisha fika?" Biruse aliuliza kwa hamaki akikumbuka ujumbe wa kepteni Mwambukusi aliomuandikia kwenye barua pepe yake kuwa majira ya saa tano amtafute.

"Ndiyo. Yupo hapa na huna haja ya kumtafuta, kwa maana hutamuona mpaka mwisho wa misheni hii. Wewe safari yako ni Goma, lakini Sasha yeye atakuwa hapa Kinshasa kwa ajili ya kukamilisha misheni itakayokuwa ikifanyikia mahala hapa ya kumlinda waziri wa madini na ataungana na kepteni Mwambukusi!"

Basi, Rusogotason, alizungumza mambo mengi pamoja na wageni wake Biruse na Sasha. Aliwapa maelekezo juu ya misheni ambazo kila mmoja wao alipaswa kwenda kushiriki, ambapo Biruse alikuwa anakwenda kuungana na kikosi cha jeshi la umoja wa nchi za Afrika *(AU),* kwa ajili ya kupambana na kikundi cha waasi kilichokuwa katika misheni ya kwenda kuchota madini katika mji wa Goma, zoezi ambalo lilikuwa limeratibiwa na mtandao wa Goma Cartel. Kikundi hicho cha M3, kilidhaminiwa kwa silaha za kivita zenye uwezo mkubwa na kilikuwa kimejidhatiti kwelikweli.

Masaa mawili baadaye, gari alina ya *Jeep,* ilifika nyumbani pale kwa Rusogotason, kwa ajili ya kumchukua Biruse tayari kwa safari ya kuelekea Goma.

Wakati wa kuondoka baada ya Biruse kuagana na mzee Rusogotason, alikumbatiana na Sasha kwa sekunde kadhaa. Kisha baada ya kuachiana alimwambia:

"Nakutakia kila la kheri Sasha!"

"Mimi pia Biruse."

"Natumaini tutaonana tena."

Sasha alijenga tabasamu hafifu, "usilegeze mkono, ukilegeza sitakuona."

Biruse naye alijenga tabasamu vilevile, “kuwa makini sana.”

“Kwaheri ya kuonana.”

“Kwaheri.”

Walikumbatiana tena, wakadumu kwenye kumbatio hilo kwa takribani dakika moja.

“Mzee tuondoke.” Miongoni mwa wanajeshi watatu waliomfuata Biruse alimwambia, ikabidi Biruse amwachie Sasha.

Kisha akapiga hatua akifuatana na wale wenzake kuuelekea mlango. Alipofika mlangoni Biruse aligeuka na kumpungia mkono Sasha. Sasha naye alimpungia huku anatabasamu. Biruse alitoka nje na wale wenzake walimfuata nyuma na wakafunga mlango; *PAAH!*

# 14

*Goma, Kongo.*

Goma Cartel, kupitia kundi la wanamgambo wa M3, walikuwa wamejipanga si kitoto, kwa ajili ya misheni yao. Kundi hili lilihitaji kutekeleza misheni hiyo katika namna ambayo haikuwahi kutokea, na hiyo yote ilikuwa ni kutumikia matakwa ya vigogo wa mtandao wa Goma Cartel, ambao ndiyo walikuwa wadhamini wakuu wa kikundi hicho kwa silaha na mambo yote waliyokuwa wanayahitaji.

Kikundi hicho, kikiongozwa na kijana wa Kinyaru, Ndahaye Bhirahise, ambaye toka udogoni mwake, amekulia kwenye mapambano ya msituni, na kupitia uzoefu wake walizishika sehemu kubwa za misitu karibu na machimbo ya madini huko Goma, kasikazini mwa Kivu, kandokando ya Ziwa Kivu.

Wanamgambo hao wakitokea maeneo ya Rwanda, waliingia na ziwa hilo wakipitia Rukaza- Rubaya, wakashika maeneo hayo na kuyaweka chini ya ngome yao.

Kwa upande wa Biruse, baada ya kufika Goma, kwa helkopta maalumu ya wanausalama, iliyotumia mwendo wa takribani saa mbili na dakika ishirini na tano, aliungana na jeshi la umoja wa nchi za Afrika, akapewa misheni namna ilivyokuwa. Na kikubwa mbacho alitakiwa yeye kukifanya ni kujipenyeza mpaka lilipokuwa kundi la M3, kwa kujifanya mwandishi wa habari, na kupenyeza taarifa nyeti ambazo zingelisaidia jeshi la umoja wa nchi za Afrika, kukabiliana na kikundi hicho cha wanamgambo.

Basi Biruse alifanya kama alivyopaswa kufanya. Baada ya kikosi

cha jeshi kumpeleka mpaka pembezoni mwa Ziwa Kivu kwa uangalifu mkubwa, Biruse aliingia kwenye eneo la misitu akiwa shingoni amenig'iniza kamera na begani alivaa kibegi kilichokuwa na vifaa vingine vya kupigia picha na kunasia sauti.

Akizidi kutembea kuingia katikati ya misitu hiyo, akiwa ametembea mwendo wa kukaribia dakika arobaini na tano, mara kuna mahala alifika akahisi chakarachakara kwenye vichaka. Mwili wote ulimsisimka. Akasita kuendelea kutembea. Akasimama kuona nini kinataka kujiri. Akiwa anajipanga ili kukabiliana nacho, na akiwa hajatahamaki, mara alishitukia watu wakiibuka kutoka kwenye vichaka na kufumba na kufumbua alikuwa amekwisha zungukwa na kundi la watu walioshika mitutu ya bunduki mkononi.

Na akiwa bado hajatahamaki tayari baadhi ya vijana takribani watatu walikuwa wamekwisha mvaa na kumminyia chini. Wakamsachi kutazama vitu alivyonavyo na walimnyang'anya kila kitu alichokuwa ameshika mkononi, pamoja na kamera yake na mkoba aliokuwa ameuning'iniza begani.

Walipohakikisha wamechukua kila kitu, walimuinua na kumsimamisha vyema, wakasimama kando yake.

Biruse alipepesa macho kuwatazama njemba wale hata akajikuta moyoni anajisemea: *Wanamgambo wa M3!*

Aliwagundua. Na akiwa bado kwenye taharuki na fikra hizo na kumbukumbu ya kile kilichotukia, mara jitu moja refu na jeusi, lenye makovu mengi usoni na ndevu nyingi, likiwa limejichora sehemu kubwa ya mwili wake, lilipiga hatua na kusimama mbele yake.

"Wewe ni nani?" Lilimuuliza kwa lugha ya kilingara.

Biruse akiigiza kuonyesha hali ya hofu alisema kwa Kingereza kwamba haelewi yale yanayozungumzwa.

Jamaa hilo likafahamu kuwa anafahamu Kingereza ndipo likarudia swali kwa lugha hiyo.

Biruse akajitambulisha kuwa ni mwandishi wa habari wa *BBC*, akatoa kitambulisho chake ambacho kilikuwa kimetengenezwa na

watu wa usalama na kulikabidhi jitu lile.

Lile jitu la miraba minne la kuitwa Bhihumbi Chumi, lilipitisha macho kwenye kile kitambulisho na baada ya kujiridhisha lilimrudishia Biruse kitambulisho chake na likamhoji:

"Shida yako hasa nini?"

"Kufahanya mahojiano na Ndahaye Bhirahise!"

"Kuhusu nini?"

"Mapigano yanayoendelea huku na matakwa yenu ili ifike mahali pa kukomesha mapigano!"

"Nani amekwambia tunahitaji kukomesha mapigano?"

"Nimekuja kufanya mahojiano tu, yale ambayo nitajibiwa yatatosha."

Lile dude lilimtazama Biruse kwa sekunde kadhaa, kana kwamba lilikuwa linasaili jambo, kisha likachukua redio ya upepo na kuzungumza kwa sekunde chache; baada ya mazungumzo hayo, liliwafanyia ishara njemba waliokuwa wamesimama karibu na Biruse kwamba wamkamate na kuambatana naye.

Biruse alichukuliwa moja kwa moja mpaka kwenye kambi ya wanamgambo hao iliyojikita kwenye misitu hiyo ambako ndiko alikokuwa amejichimbia Ndahaye Bhirahise. Biruse alipelekwa mpaka mbele ya kiongozi huyo wa kundi hilo la wanamgambo wa M3.

Ukweli ni kwamba, mazingira ya kambi hiyo, yalikuwa yanatisha na kuogopesha mno na yalikuwa ni ya hatari sana. Kwa yale yote ambayo Biruse alikuwa anayashuhudia, moyoni mwake alikiri kikosi hiki cha wanamgambo kilikuwa hakina mchezo.

Biruse alishuhudia watu wengi, wake kwa waume pamoja na watoto wakiwa wamekamatwa na kufungwa kamba huku wamepangwa mstari mmoja. Watu hao wote waliokuwa wamekamatwa, walikuwa wamevuliwa nguo zao na kubaki kama walivyotoka kwenye matumbo ya mama zao.

Katika muda mfupi ambao Biruse amefika hapo aliona vitendo

vya kikatili mno. Wanawake walikuwa wanabakwa na watoto walikuwa wanalawitiwa. Vijana waliolazimishwa kufanyiwa unyama wa namna hiyo na kuleta ubishi walikuwa wakipigwa risasi kama mchezo. Hakika matukio hayo yalimuumiza mno Biruse na akajikuta nafsi yake inachafukwa mno!

Kwa upande wa majeshi ya umoja wa nchi za Afrika, kila kilichokuwa kinaendelea walikuwa wanasikia kupitia kwenye kifaa maalumu cha kunasa sauti, chenye udogo wa kulingana na punje ya mchele ambacho Biruse alikuwa ameweka ndani ya sikio lake la upande wa kulia. Na zaidi kifaa hicho kilikuwa na *GPRS* iliyosaidia kuwapa muelekeo. Kwahiyo katika wakati huo Biruse akiwa hapo kambini, kikosi kile cha majeshi nacho kilikuwa kinasogea kuielekea kambi hiyo.

Hata hivyo, katika namna ambayo hakuna aliyekuwa anafahamu, katika majeshi hayo ya umoja wa nchi za Afrika, kulikuwa na kijana mmoja ambaye alikuwa amepenyezwa na mtandao wa Goma Cartel kwa ajili ya kutoa taarifa ili lengo la kuuawa kwa wanajeshi wengi wa jeshi hilo liweze kutimia pamoja na kuvujisha mipango ya jehsi hilo. Na huyo kijana, kutoka jeshi la Burundi, alifanikiwa kuwapasha wanamgambo wa M3, kuwa Biruse hakuwa mwandishi wa habari, bali ni shushushu aliyepenyezwa na majeshi ya umoja wa nchi za Afrika.

Biruse akiendelea kufanya mazungumzo na Ndahaye Bhirahise, mara yule kiongozi wa kikosi kilichomtoa kule msituni, Bhihumbi Chumi, aliingia na kwenda moja kwa moja mpaka alipokuwa amekaa Ndahaye, akamnong’oneza.

Kwa mapokeo ambayo Biruse aliyaona usoni kwa mkubwa huyo wa kikosi alifahamu mambo yamekwisha haribika. Akajikuta anameza mate ya baridi na kujipanga kukabiliana na lile litakalojiri. Na akiwa bado kwenye hali hiyo, mara baada ya Bhihumbi Chumi, kumnong’oneza Ndahaye, kiongozi huyo wa wanamgambo aliuchukua mtutu wake wa bunduki ili kumnyanyulia Biruse.

Hata hivyo, Biruse alikuwa amekwisha kiona kitendo hicho na hakutaka kuilaza damu yake. Alikuwa moyoni amekwisha amua liwalo na liwe lakini siyo kuwekwa chini mfano wa kuku anayetaka kuchinjwa.

Kana kwamba alikuwa anaongozwa na mtambo maalumu, Biruse alisimama kwa kasi ya ajabu, kisha akaruka na kumvaa yule jamaa Bhihumbi Chumi, wakagaragara wote mpaka chini.

Biruse alikuwa mwepesi kutokana na umbo lake na mazoea ya kufanya michezo ya sarakasi. Kwa mwendo wa haraka wakiwa chini alimnyang'anya yule njemba bunduki yake na akainuka kama kimbunga na kumkumba kwa kitako cha bunduki Ndadaye ambaye bado alikuwa ametoa macho akishangaa kilichokuwa kinaendelea.

Ndadaye alibwabwaja kwa maumivu makali baada ya kitako kile cha bunduki kumtandika kichwani; *Yalaa!* na ndipo Biruse alianza kumimina risasi, akimpakia yule Bhihumbi Chumi ambaye alikuwa bado yupo chini. Kitendo hicho cha kumwaga risasi, zilizomkata kauli Bhihumbi Chumi pale chini, kikawa kimeitibua kambi hiyo yote, wanamgambo wote wa M3, wakafahamu wamekwisha ingiliwa.

Hayo yote yaliyokuwa yanajiri, yalikuwa yanasikika kwenye kikosi cha wanajeshi wa umoja wa nchi za Afrika; kwa hiyo, kikosi hicho kiliona hakina tena muda wa kusubiri zaidi ya kuvamia kambi hiyo.

Ili kuleta taharuki zaidi, kikosi hicho kilituma mabomu yenye nguvu yaliyoichangamsha kambi ile ya wale wanamgambo wa M3. Ikawa ni patashika kanga kuchanika. Hekaheka zikaanzia hapo. Kila mtu akakazama kujihimu kuokoa nafsi yake. Na kufumba na kufumbua majeshi hayo yaliingia ndani ya kambi hiyo na mapigano ya kutupiana risasi yakatamalaki. Ikawa piga ni kupige!

Kwa upande wa Biruse, alikuwa amemuweka chini ya ulinzi Ndahaye Bhirahise, kwa kumnyooshea mtutu wa bunduki.

"Mwisho wenu umefika," alimwambia Ndahaye ambaye alikuwa

anaugulia kwenye maumivu makali ya kichwa yaliyotokana na kupigwa na kitako cha bunduki.

Baada ya kuambiwa maneno hayo Ndadaye aliinua kichwa, akakusanya mate mdomoni yaliyochanganyikana na damu, akamtemea kwa nguvu Biruse usoni.

Mate yale yalimtia kinyaa haswa Biruse na akiwa ameinua mkono ili ayafute, Ndadaye alitaka kuitumia nafasi hiyo kujinasua kwenye mtego ule uliokuwa umemnasa. Alichomoa bastora yake haraka na kumnyooshea Biruse, lakini Biruse akawa ameona na alikuwa mwepesi zaidi maana kama umeme alihama pale alipokuwa na ile anahama tu, risasi ilimchuna begani, akapepesuka lakini wakati huo anapepesuka alikuwa naye amekwisha achia risasi mbili ambazo zilikwenda moja kwa moja kujikita kifuani kwa Ndahaye Bhirahise.

Kiongozi huyo wa kikundi cha wanamgambo wa M3, alibwabwaja kwa maumivu makali wakati anakwenda chini utasema gunia la mbatata. Baada ya kufika chini alizimika mfano wa mshumaa uliopulizwa na upepo!

Biruse naye alijikusanya kutoka chini alipodondokea akahisi maumivu makali kwenye bega lake la upande wa kushoto. Baada ya kuona amekuwa vyema, alitoka ndani ya chumba hicho kwa tahadhari, na kwenda mpaka nje kuungana na kikosi cha majeshi ya umoja wa nchi za Afrika.

Mapambano nje yalikuwa ni makali mno. Hata hivyo, kundi hilo la wanamgambo wa M3, halikuweza kufua dafu mbele za majeshi yale ya umoja wa nchi za Afrika kutokana pia na viongozi wao kuuawa mapema na wafuasi wao kuingiwa hofu.

Baada ya mapigano ya risasi ya masaa mawili kambi hiyo hatimaye ilikuwa kimya. Wanamgambo wote wa M3 walikuwa wamepukutishwa wakapukutika. Kwenye kikosi cha umoja wa nchi za Afrika, kulikuwa na marehemu mmoja, ambaye ndiye yule mpenyeza taarifa na alipigwa risasi na wenzake baada ya kugundulika alipokuwa anajaribu kuwasiliana na watu wa Goma

Cartel, kuwapasha yaliyokuwa yanaendelea huko.

Kulikuwa na majeruhi wengine watatu ambao hawakuwa na hali mbaya sana, akiwemo Biruse.

Kikosi hicho cha majeshi ya umoja wa nchi za Afrika, kilifanikiwa kuokoa kinamama, watoto na wanaume waliokuwa wametekwa. Lakini, kilibaini chimbo ambapo kulikuwa kumerundikwa madini yaliyokuwa tayari kuja kuchukuliwa na watu wa Goma Cartel!

*****

Tukirudi Kinshasa, kikao baina ya waziri wa mambo ya nje wa Tanzania, Amos Mokiwa, pamoja na waziri wa madini na nishati wa Kongo, Cante Mukolozi, kilikuwa kimepangwa kufanyika majira ya saa nane za mchana wa siku hiyo.

Hata hivyo, kabla ya kufanyika kwa kikao hicho, ndipo taarifa zilitapakaa kwamba Goma ipo magotini. Yaani kikosi cha wanamgambo wa M3, kilichokuwa kimeushika kwa muda mrefu mji wa Goma, kimedhibitiwa.

Baada ya kepteni Mwambukusi kuzipata taarifa hizo, akishirikiana na Sasha, walikwenda mpaka kwenye hoteli aliyokuwa amefikia waziri wa mambo ya nje na kusihi walitaka kuonana naye.

Walipopata hiyo nafasi ya kukutana naye, kepteni Mwambukusi alimtolea bastora waziri na kumwambia awataje watu wake wote anaoshirikiana nao, ambao wapo kwenye mtandao wa Goma Cartel!

Waziri alitoa macho:

“Sikuelewi unachozungumza kepteni!” Amosi Mokiwa alisema akivua miwani yake ya macho.

“Unanielewa,” kepteni Mwambukusi alisema akiwa amemkazia macho.

“Sifahamu chochote na kama mmeelezwa kuwa nahusika nimesetiwa tu.”

“Kepteni huyu anatuchelewesha,” Sasha alizungumza na kutoa bastora yake, kisha akamuwasha waziri Amosi, risasi ya mguu!

*Mamaaaaa!* Waziri alilia kama mtoto mdogo kutokana na maumivu makali aliyohisi.

"Sema waziri kabla sijakuwasha nyingine!"

Wakati huo wasaidizi wake walikuwa wamekwisha ingia na walitahamaki kuona kilichokuwa kinajiri. Walitulizwa kwa mtutu wa bunduki na kepteni Mwambukusi. Kisha akawapasha kuwa wapo kazini na waziri si mtu mzuri kama wanavyofikiria. Wale walinzi iliwadili wawe wapole maana wanamfahamu kepteni Mwambukusi na cheo chake katika kada ya usalama.

"Sema waziri!" kepteni alizidi kumlazimisha.

Baada ya kuona waziri huyo, bado anajivuta vuta Sasha aliinua tena bastora yake lakini kepteni alimzuia kufyatua risasi.

Kepteni Mwambukusi alitoa simu yake mfukoni kisha akaicheza ile *audio* yenye sauti ya waziri Amos ambayo alikuwa akifanya mazungumzo na mtu kutoka kwenye mtandao wa Goma Cartel.

"Mwisho umekwishafika waziri, ni kuchagua uangamie mwenyewe ama uangamie na wenzako!"

Hakika waziri Amos aliona hana tena mahala pa kupetukia hata akiepuke kikombe kile. Maji yamemfika shingoni. Basi hakuwa na namna. Aliwataja watu wote waliokuwa kwenye mtandao huo wa Goma Cartel. Kwahakika ulikuwa ni mtandao mkubwa unaohusisha mawaziri, marais, na makampuni mbalimbali.

Hadi anamaliza kutaja, kepteni Mwambukusi na Sasha walijikuta wanashusha pumzi ndefu. Hakika kuumaliza mtandao huo ni jambo gumu. Lakini kepteni Mwabukusi alijisemea kuwa inawezekana na hiyo ndiyo misheni inayofuata.

Waziri Amosi Mokiwa, alikamatwa na wanausalama tayari kurejeshwa Tanzania kwa ajili ya kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria, na waziri wa madini na nishati Cante Mukolozi, alipashwa yale yaliyojiri na hatari iliyokuwepo dhidi ya maisha yake.

Kepteni Mwambukusi, Sasha na Biruse nao walirejea Tanzania wakiwa ni wenye furaha kubwa kutokana na ushindi walioupata kwenye misheni hiyo. Lakini kepteni Mwambukusi aliwaambia

wawili hao; misheni hiyo ilikuwa ni supu tu, mlo kamili unakuja; nao huo mlo kamili ulikuwa ni misheni inayofuata ya kupambana na vigogo wa mtandao wa Goma Cartel, hasa kumuondosha rais wa Rwanda, Emmanuel Matoe; ambaye ndiye alikuwa nguzo haswa ya Goma Cartel!

*MWISHO WA SIMULIZI HII NI MWANZO WA SIMULIZI NYINGINE TAMU YA KIJASUSI, USIKOSE KITABU KIJACHO!*

## *KUHUSU KITABU CHA OPARESHENI KHARTOUM 01*
## *(Kufa Ama Kupona)*

Kachero Othuman Seyunguson kutoka Tanzania, anatumwa kwenye misheni ya kuinusuru ikulu ya Sudan ambayo ilikuwa inanyemelewa na wadhalimu.

Misheni hii iliyopewa jina la *Oparesheni Khartoum 01,* haikuwa misheni ya kitoto maana adui mkubwa wa taifa la Sudan, Brigedia Omar Al - Bashir alikuwa amejipanga kwelikweli na aliihitaji ikulu ya Sudan kufa na kupona.

Kachero Seyunguson, pamoja na msaidizi wake Farida, kutoka nchini Kenya, aliyepikwa akaiva kwenye mambo ya mapambano ni kana kwamba walitolewa sadaka kwenye misheni hii maana kila waliyekutana naye - hata waliyedhani yupo upande wao, alikuwa ni adui.

JE, UNAKOSAJE KUSOMA KITABU HIKI CHENYE KISA CHA KUKATA NA SHOKA?

*PIGA SIMU* **+255 753 905 099 KUJIPATIA KOPI YAKO.**

